

**UHAKIKI WA MAUDHUI, SIFA, ISHARA ZA MAZIMWI NA FANI KATIKA
NGANO ZA MAZIMWI ZA JAMII YA GĪKŪYŪ**

MOSES KIARIE KAMAU

**Tasnifu hii imewasilishwa katika Idara ya Usomilugha na Mawasiliano ili Kutimiza
Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Laikipia.**

Chuo Kikuu cha Laikipia

SEPTEMBER 2016

UNGAMO NA IDHINI

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawasilishwa na yeyote kwa mahitaji ya kutosheleza shahada katika chuo kikuu chochote kile.

Moses Kiarie Kamau

MK22/2011/12

Sahihi.....

Tarehe.....

IDHINI

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa katika idara ya Usomilugha na Mawasiliano ili kutimiza mahitaji ya shahada ya uzamili kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Laikipia.

Jina: Prof. James Ogola Onyango

Sahihi..... Tarehe.....

Idara ya Usomilugha na Mawasiliano,

Chuo Kikuu cha Laikipia

Jina: Dkt. Nicholas Kamau Goro

Sahihi..... Tarehe.....

Department of Literary and Communication Studies,

Laikipia University

TABARUKU

Kazi hii naitabarukia marehemu wazazi wangu kwa kunilea na kunipeleka shule nikafika nilipofika pamoja na Bw.na Bi. Ng'ang'a, mke wangu mpendwa Mary, watoto wetu Prudence, Shirlyne na Maxwell kwakunitia shime na uvumilivu mwingi waliokuwa nao kipindi chote nilichokuwa masomoni. Nduguzangu na wataalamu na wasomi wote wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Laikipia.

SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na utulivu wakati wote nilipokuwa nikitaalumia shahada hii ya uzamili. Aidha nawashukuru kwa njia ya kipekee wasimamizi wangu: Prof. James Ogola Onyango na Dkt. Kamau Gorokwa kuniongoza na juhudi zao ambazo zimechangia pakubwa kukamilika kwa kazi hii. Naomba pia kuwataja na kuwashukuru wahadhiri wafuatao kwa kukubali kuisoma kazi yangu na kunielekeza kwa ushauri: Prof. Yieke, Prof. J.O. Onyango, Dkt. Gwachi Mayaka, Dkt. Kirigia, Dkt. Rutere na Dkt. Sheila. Ushauri wenu ulikuwa mchango mkubwa ambao ulisaidia kuziba mapengo ambayo yangetokea katika kazi hii.

Nawashukuru wanafunzi wenzangu: Margaret Njeri, Ruth Kung'u, Juddy Mwangi, Pharis Githiomi, Evans Nyachoi na Pauline Wainaina kwa ushirikiano na mchango wao tulipokuwa tukishughulikia kozi hii ya Kiswahili pamoja. Mawaidha yenu yalinitia shime. Nawashukuru nyote kwa msaada wa vitabu pia

Kwa marehemu wazazi wangu, nawashukuru kwa kunipeleka shuleni na kunionyesha umuhimu wa elimu maisha. Namshukuru mke wangu mpendwa Mary na wana wetu Prudence, Shirlyne na Maxwell kwa kunipa mazingira tulivu katika kipindi chote nilipokuwa masomoni. Shukrani tele kwa mke wangu kwa kuwa mhimili mkuu kwangu, jambo ambalo lilinitia moyo sana.

Mwisho namshukuru Erustus Thuo kwa mchango wake mkubwa nyanjani wakati wa kukusanya data na wote walionisaidia kwa njia moja au nyingine nilipokuwa nikishughulikia kazi yangu. Mungu awabariki.

IKISIRI

Ngano za mazimwi ni maarufu sana katika jamii nyingi za Kiafrika. Ngano hizi katika jamii ya Gĩkũyũ hudhihirisha matumizi changamano ya fani na ishara. Suala hili halijafanyiwa utafiti wa kina kulidhibitisha kiusomi. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa nikuhakikimaudhui, sifa, ishara za mazimwi na fani katika ngano za mazimwi katika jamii ya Gĩkũyũ. Aidha ulibainisha sifa za ngano za mazimwi kwa msingi wa fani ambapo vipengele kama msuko nawahusika vilichunguzwa na kisha mtafiti akatathmini umuhimu wa ngano hizi katika jamii. Kigezo kilichotumika kupimia kazi hii ni msingi wa nadharia ya Umuundo na Umuundoleo. Miongoni mwa waasisi wa nadharia ya Umuundo ni Ferdinand de Saussure na kuendelezwa na Roman Jakobson, Rene Wellek. Wana-Umuundowalitilia mkazo miundo ya kiuashiraji na unasibishi wa maana katika kazi ya fasihi. Walieleza hali ya ishara moja kuwa na maana nyingi kwa kuiweka au kuikita maana kwenye muktadha wa kijamii, yaani jamii inakuwa na athari kubwakimaana. Umuundoleo unahusishwa na Jacques Derrida na Michel Foucault ambao wana mawazo kuwa kiashiriwa hakiwezi kuwa funge. Wahakiki hawa wanadahili kuwa katika miktadha mingi ya matumizi ya kiashirii, kiashiriwa chake au maana huhamishwa au huashiriwa ambapo lugha huchukua nafasi kubwa kama jira ya maana halisi au zinazowezezana. Kundi lengwa lilikuwa ngano za Gĩkũyũ katika jimbo la Nyandarua. Data ya utafiti huu ilipatikana kwa kukusanya ngano za mazimwi kwanza kutoka kwa wajuzi wa ngano wenye umri mpevu, kwa kutumia sampuli-tajwa. Ngano zilirekodiwa kwa kutumia tepu-rekoda na kisha ngano tano za mazimwi zikateuliwa kimaksudi ili kuhakiki maudhui, sifa, fani na ishara ya mazimwi. Hatimayezilichanganuliwakwavipengele vya msuko, maudhui, dhimana mtindo. Utafiti huu utakuwamuhimukwa jamii ya wasomi hasa wanafunzi, walimu na watafiti wa fasihi simulizi katika kufahamu dhima ya ngano za mazimwi katika jamii. Aidha utachangia katika kuzihifadhi ngano za fasihi simulizi.

ABSTRACT

The ogre narratives are common among many African communities. The Gikũyũ oral narratives employ complex symbolism of ogres and stylistic devices and the area has not been researched on. This research therefore aimed at investigating the symbolism of ogres and the stylistic devices used in Gikũyũ ogre oral narratives. The objectives of the study were to look at the symbolism of ogres in the Gikũyũ community as portrayed in the Gikũyũ oral narratives, examining the characteristics of these narratives based on the stylistic devices and their roles in the community. The research was guided by structuralism and post structural theory. The proponents of the theory includes: Roman Jakobson Rene Wellek and later influenced by Ferdinand de Saussure. The Post Structuralists are associated with Jacques Derrida among others. Structuralists mainly look at the different parts that form the whole structure. They argued that one symbol can have more than one meaning depending on the social context. The Post-Structuralists emphasized on the role of the language use in analyzing the social structure, meaning and their interpretations in terms of self-consciousness where language is taken as the main axis in giving both the real meaning and the derived one. The data was collected in Nyandarua County. The Oral narratives were first collected from the field from key informants who were elderly and had experience in narrating by Snowball sampling. The narratives were tape recorded using a tape-recorder then transcribed for analysis. A purposeful sample of five narratives whose main characters are the ogre and those that were different from each other with and used various stylistic devices were then chosen from the collected narratives. The data collected finally was analyzed descriptively by studying the themes, character traits and symbols of ogres that they portray in the Gikũyũ oral narratives. The findings of the study will be useful to the students, teachers and researchers of oral literature. They will also be useful in preserving oral narratives in literature and therefore contribute towards understanding of the significance of the ogre oral narratives.

YALIYOMO

MADA YA UTAFITI.....	i
UNGAMO NA IDHINI.....	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI	iv
IKISIRI	v
ABSTRACT	vi
YALIYOMO	vii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

1.1 Usuli wa mada.....	1
1.2 Suala la utafiti.....	2
1.3 Madhumuni ya utafiti.....	3
1.4 Maswali ya utafiti.....	3
1.5 Umuhimu wa utafiti.....	3
1.6 Upeo wa utafiti.....	4
1.7 Maelezo ya Istilahi	5

SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI

2.1 Utangulizi	6
2.1.1Maandishi Kuhusu Ngano za Mazimwi	6
2.2 Maudhui Katika Ngano za Mazimwi	11
2.3 Wahusika Katika Ngano za Mazimwi.....	11
2.3.1 Sifa za Mazimwi	12
2.4 Msuko	13
2.5Dhana ya Fani	14
2.6 Takriri	15
2.7 Taswira	16
2.8 Ishara Katika Ngano za Mazimwi	16
2.9Tamathali za Usemi	17
2.9.1Semi	17
2.9.2Tashbihi	18
2.9.3Chuku	18
2.9.4 Tashihisi.....	18

2.9.5 Balagha.....	19
2.9.6 Nidaa.....	19
2.9.7 Tanakali za Sauti	19
2.10 Msingi wa Nadharia	19
SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI	
3.1 Utangulizi	22
3.2 Mahali pa utafiti	22
3.3 Kikundi lengwa	23
3.4 Uteuzi wa Sampuli	23
3.5 Ukusanyaji wa data	23
3.6 Mbinu ya utafiti.....	23
3.7 Uchanganuzi wa data	24
SURA YA NNE: UCHANGANUZI WA DATA	
4.1 Utangulizi.....	25
4.2.1Uhakiki wangano za mazimwi	25
4.2.1 Maudhui	25
4.2.1.1 Ukatili	25
4.2.1.2 Majuto.....	27
4.2.1.3 Unafiki	28
4.2.1.4 Utu.....	29
4.2.1.5 Ujasiri	30
4.2.1.6 Vitisho	31
4.2.1.7 Ukombozi	32
4.3.Uhakiki waWahusika wa Ngano za Mazimwi	33
4.4. Msuko	38
4.4 Usimulizi	42
4.5 Mtindo.....	43
4.5.1 Ishara za Mazimwi	43
4.5.1.1 Tishio	45
4.5.1.2 Ukatili	46
4.5.1.3 Kifo / Mauti	48
4.5.1.4 Tamaa	49

4.5.1.5 Janga / Baa	50
4.5.2 Tamathali za Usemi	50
4.5.2.1 Misemo	50
4.5.2.2 Tashbihi	52
4.5.2.3 Tanakali za Sauti	54
4.5.2.4 Taswira	55
4.5.2.5 Tashihisi	56
4.5.2.6 Chuku	57
4.5.2.7 Majazi	59
4.5.2.8 Kinaya	59
4.5.2.9 Balagha.....	60
4.5.3 Mbinu Zingine	61
4.5.3.1 Nidaa	61
4.5.3.2 Nyimbo	62
4.5.3.3 Takriri	63
4.6 Umuhimu wa Ngano za Mazimwi	64
4.7 Hitimisho	66
SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI	
5.1 Utangulizi	67
5.2 Hitimisho	67
5.3 Mapendekezo ya Utafiti	69
MAREJELEO	70
VIAMBATISHO	74
Kiambatisho (a): Ngano za Gĩkũyũ	77
Kiambatisho (b): Tafsiri ya Kiswahili	86
Idhini ya Kufanya Utafiti.....	97

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Ngano ni hadithi za kale ambazo ni mojawapo kati ya tanzu maarufu za fasihi simulizi. Ngano ni zao la jamii na hudhihirisha masuala ya kitamaduni ya jamii husika. Kuna aina mbalimbali za ngano za fasihi kama vile: Ngano za mazimwi, ngano za usuli, ngano za mtanziko, ngano za mashujaa, hurafa, hekaya, visasili, mighani, mbazi na kadhalika. Ngano za mazimwi ni maarufu katika jamii nyingi ulimwenguni hazijafanyiwa utafiti wa kina ili kutoa nuru kuhusu mazimwi kwa vile yamesawiriwa yakiwa na sifa mbalimbali. ambao unaweza kuikuza na kuleta uelewa zaidi kuhusu. Madai haya yanaonyesha umuhimu wa kufanya utafiti hasa katika kipera cha ngano ambacho ni maarufu katika kutimiza malengo mbalimbali ya kijamii. Ngano ni zao la jamii husika na hufungamana na mazingira ya jamii, utamaduni wao, itikadi na kadhalika.

Ni muhimu kuziangazia jamii mbalimbali ili kuweza kutambua tanzu zinazopatikana katika jamii hizo kwa kuwa kila jamii ina njia yake ya kuziainisha tanzu zinazopatikana katika jamii yao. Ngano za mazimwi ni ngano za fasihi simulizi ambapo wahusika mazimwi ndio huchukua nafasi kubwa. Kipera hiki kinapatikana katika jamii nyingi sana za Kiafrika na hudhihirisha sifa mbalimbali kulingana na jamii husika ambapo sifa zake nyingi zinaingiliana. Tofauti ya sifa hutegemea jamii na utamaduni wake kwa kuwa jamii mbalimbali huwa na mitazamo tofauti kuhusu mazimwi kama inavyodhihirika kupitia kwa ngano za fasihi simulizi.

Wahusika hawa wamesawiriwa kuwa nasifa mbalimbali kulingana na jamii kama: kuwa binadamu katili, mizimu ya watu wa kale, pepo waletao maovu, viumbe wenye uwezo kuliko binadamu lakini wanaopenda kuwatendea binadamu mabaya na kadhalika. Taswira inayojitokeza kuhusu mazimwi ni kuwa, wahusika katika ngano za mazimwi ni wa kidhahania na huweza kuashiria jambo fulani. Inaaminika pia kuwa mazimwi ni wahusika wanaowakilisha binadamu wa kawaida wenye tabia fulani katika jamii zetu.

Ngano za mazimwi katika jamii ya Wakamba zinasawiri mazimwi yakiwa roho za watu waliokufa zamani sana kiasi cha kutoweza kukumbukwa na hujitokeza katika ulimwengu wa kiroho. Aidha mazimwi haya yanadhibitisha kuwa mazimwi hupewa sifa na wanajamii

ambamo ngano hizi zinatokana hufanya shughuli kama watu wengine kama vile kulima, kufuga mifugo na hata kuwa na familia. Watu huyaogopa kwa kuwa ni waharibifu na kwaukatili wao wa kuwala na kuwaua watu. Huwameza watu na hatimaye wanaposhindwa na mashujaa, huwaeleza jinsi ya kuwarejesha wote wale waliomezwa hapo awali.

Mazimwi yalionekana kuishi pamoja na binadamu au karibu na binadamu na kutenda mambo yaliyotendwa na watu kama kuoa, kufuga, kuwa na jamii zao. Wakati mwingine mazimwi yalitenda wema na kuwasaidia watu waliokuwa na shida lakini kwa nia fulani. Katika jamii zingine yanasemekana kuwakilisha watu wenye sifa fulani kama wageni, watu wenye tabia hasi, au watu ambao hawakupendwa na jamii husika.

Kutokana na Maelezo ya wasomi wengi, inaelekea basi kuwa ngano hizi zinadhihisha na kuwakilisha dhana fulani kwa kuwa vile mazimwi haya yanatumika kupitisha ujumbe maalumu kutokana na sifa mbalimbali zinazojitokeza. Maswali yanayoibuka ni je, kwa nini ngano za mazimwi zinapatikana karibu katika jamii zote? Kwa nini yakasawiriwa kuwa na sifa hasi na yenye uwezo uliozidi wa binadamu? Ngano hizi zina dhima gani katika jamii husika na jamii pana ya wasomi na wanafasihi? Kwa nini mazimwi yakasawiriwa kuwa na maumbile ya kiajabu?

Maswali haya na mengine yanatufanya kutaka kuangazia kipera hiki cha ngano na kukichunguza kwa kina ili kutambua umuhimu wake katika jamii na wasomi wa fasihi simulizi. Utafiti huu ulinuia kuhakiki ngano za mazimwi ili kubainisha ishara mbalimbali zinazodhihirika katika ngano za mazimwi katika jamii ya Gĩkũyũ kwa kurejelea kipengele cha maudhui, wahusika na umuhimu wake. Sifa zinazosawiriwa kuwa nazo zinaonyesha kuwa wahusika mazimwi wanawakilisha watu wenye sifa fulani hasa hasi kama inavyoonekana katika ngano hizi katika jamii za Kiafrika. Maana hizi za kijazanda ndizo zinadhihirisha kuwa ngano hizi ni muhimu katika jamii ya leo na wala hazijapitwa na wakati. Uwasilishajujumbe wa ngano hizi hufanikishwa kutokana na matumizi ya mbinu changamano ambazo zimebainishwa katika kitengo cha fani.

1.2 Suala la Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuhakiki maudhui, sifa za wahusika mazimwi, ishara mbalimbali za mazimwi kama zinavyodhihirika katika ngano za mazimwi za jamii ya Gĩkũyũ. Ngano za mazimwi za Gĩkũyũ zimedhihirisha matumizi changamano ya ishara za mazimwi na fani ambazo zimefanikisha maudhui na dhamira katika jamii. Ishara hizi zinaibua matumizi mbalimbali ya neno zimwi katika jamii. Kipengele cha fani kina nafasi kubwa katika

kufungamanisha yaliyomo na malengo ya jamii kupitia kwa ngano. Aidha utafiti huu umepambanua umuhimu wa ngano za mazimwi katika jamii kwa vile mazimwi ni viumbe dhahania waliopatikana katika hadithi nyingi za jamii za Kiafrika.

1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu umedhamiria kutimiza malengo yafuatayo:

- (i) Kubainisha sifa za ngano za mazimwi za jamii ya Gĩkũryũ kwa msingi wa fani.
- (ii) Kupambanuamaudhui na dhima ya ngano za mazimwi katika jamii.
- (iii) Kuhakiki fani na ishara ya mazimwi katika ngano za jamii ya Gĩkũryũ.

1.4 Maswali ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu ni kuhakiki fani na ishara ya mazimwi katika ngano teule za mazimwi. Katika kutimiza haya, maswali yafuatayo yanatuongoza:

- (i) Je, ngano za mazimwi katika jamii ya Gĩkũryũ zinadhihirisha sifa zipi?
- (ii) Je, ngano za mazimwi za jamii ya Gĩkũryũ zinadhihirisha maudhui gani na zinaumuhimu upi katika jamii?
- (iii) Je, ni mbinu gani zinazojitokeza katika ngano za mazimwi katika jamii ya Gĩkũryũ na mazimwi yanaashiria nini?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu umechochewa na ukweli kwamba utanzu wa ngano katika jamii nyingi ni kipengele muhimu katika fasihi. Ngano ni kipengele cha fasihi simulizi kilicho kikongwe na ambacho kimefanyiwa utafiti mchaheikilinganishwa na vipera vingine vya fasihi simulizi kama ushairi, methali, drama na vitendawili. Pili, wakongwe waliokuwa hazina kubwa katika fasihi simulizi mfano katika kuwatambia watoto na vijana hapo kale, siku hizi wamekabiliwa na shughuli za ainambalimbali kutokana na mabadiliko katika mfumo wa maisha ya kileo.

Masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa yamewafanya watu kutopata muda wa kutosha hasa nyakati za jioni ambao ndio uliokuwa wakati mwafaka wa kupokezana amali za jamii kupitia kwa vipera mbalimbali vya fasihi simulizi mojawapo kikiwa ni: kurithisha vizazi vijavyo. Ni dhahiri kuwa utamaduni wa jamii huhifadhiwa katika lugha na kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na ngano hizi zisipopokezanwa kwa kusimuliwa kama ilivyokuwa zamani, zitapoteza baadhi ya sifa zake na hata kusahaulika.

Kipera cha ngano za mazimwi kinapatikana katika jamii nyingi za Kiafrika na hivyo basi kuonyesha kuwa kina umuhimu mkubwa katika jamii zetu. Neno mazimwi limekuwa na maana pana hata katika jamii ya kisasa kwa kuwa kinachosawiriwa ni tofauti na kinachorejelewa. Mazimwi yalitumika kuwakilisha dhana mbalimbali kwa hivyo ni kiashiria cha mambo tofauti Jambo la kusikitisha ni kuwa kipera hiki kinaelekea kusahaulika kutokana na mabadiliko katika maisha ya kisasa yanayoegema katika utamaduni sawa wa ulimwengu unaochochewa na utandawazi. Sera zilizobuniwa kuhusu mfumo wa elimu zilifisha matumizi ya lugha za kwanza katika shule za msingi. Aidha juhudi kubwa ilitiliwa katika kuikuza lugha ya Kiingereza kuliko lugha nyingine za kwanza.

Hivi karibuni suala la uhuru wa vyombo na kuchipuka kwa vituo vinavyopeperusha habari na kutangaza kwa lugha za kwanza kumefufua umuhimu wa kushughulikia fasihi yetu hasa kupitia kwa vipindi vya watoto. Aidha mjadala kuhusu kufunza watoto katika lugha zao za kwanza limeibuka na utafiti huu utakuwa njia moja kuu itakayochangia kuendeleza fasihi kwa kuwafunza ngano na tanzu zingine kwa na kuzilinganisha na jamii zingine.

Aidha utafiti huu utakuwa mchango mwafaka katika kuhifadhi ngano zilizoko kuhusu mazimwi kwa vile umechangia katika kukusanya ngano ambapo chache zimeteuliwamiongoni mwa ngano zingine na kutumiwa katikakuzichambua ngano za mazimwi katika jamii ya Gĩkũyũ. Utafiti huu pia utakuwa hatua muhimu kwa wasomi ambao watanuia kufanya utafiti zaidi kuhusu ngano za mazimwi hasa katika jamii zao na katika fasihi kwa jumla kwa kuzilinganisha na za jamii zingine. Utafiti huu utachangia katika kuongeza hazina ya ngano za mazimwi katika elimu hasa katika uwanja wa ngano.

1.6 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika kaunti ya Nyandarua nchini Kenya. Kaunti ya Nyandarua hupatikana katika eneo la katikati mwa Kenya ambapo kusini imepakana na kaunti ya Nakuru, kaskazini imepakana na kaunti ya Laikipia, na upande wa kusini wa kaunti ya Kiambu na Mashariki kauli ya Nyeri. Kaunti ya Nyandarua. Mtafiti anayafahamu maeneo ya kaunti hii kama Mugenda and Mugenda (1999) wanasema kwamba ni vizuri mtafiti afanye utafiti wake katika sehemu anayoifahamu vizuri ili aepuke matatizo ya kisaikolojia. Jambo hili ndilo limemfanya mtafiti kuchagua eneo hili.

1.7 Maelezo ya Istilahi

Ishara bia - Ishara zinazoweza kutambuliwa na watu wengine popote walipo

Ishara za kitaashira - Ni ishara za kiurejelezi au za kiutamaduni.

Ishara zisizo bia – ishara ambazo maana zake hueleweka katika muktadha wa kazi inayohusika

Kiashirii - Ishara ya neno au jinsi linavyowasilishwa kimaandishi

Kiusababishi – Hali ya tukio moja kusababisha jingine

Taashira - Neno au jina kuchukua nafasi ya neno au jina lingine linalohusishwa nalo

Ukiamaumbile – Kuwa katika hali iliyopita uhalisia

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI

2.1Utangulizi

Sura hii inahusutafiti ambazo zimefanywa na zinazohusiana kwa njia moja au nyingine na utafiti huu. Ameonyesha kufanana kwa tafiti hizo na utafiti wake na vilevile tofauti iliyoko na tafiti nyingine. Pengo la kielimu linalotakikana kuzibwa litaangaziwa kwa kuzingatia nadharia na mikabala kuwa msingi wa utafiti huu. Aidha sifa, muundo, msuko, wahusika, mtindo na maudhui yameangaziwa ili kudhihirisha fani ilivyotumika kuwasilisha ujumbe.

2.1.1Maandishi Kuhusu Ngano za Mazimwi

Ngano za fasihi simulizi zimekuwa zikipokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kigine katika hali yake ya asilia. Katika kuziainisha ngano za fasihi simulizi, Finnegan (1977) anasema kuwa ngano zingine zinaweza kuitwa za kutisha. Hizi ni ngano ambazo shujaa hung'ang'ana na mazimwi ambao hujaribu kummeza. Hadithi hizi ni maarufu katika jamii za wabantu wanaopatikana Afrika. Wahusika katika ngano hizi huwa na sifa kama vile: mguu mmoja, midomo miwili, nusu mnyama na nusu binadamu, majitu, na hata pepo katika Afrika ya Magharibi. Wengine huamini kuwa mazimwi yana maumbile ya ajabu na wanakaribia wanyama au majini hasa jamii zilizo na imani ya dini ya Kiislamu. Jamii zinazoishi katika maeneo ya pwani ya Afrika Mashariki ndizo zilizo na ngano za mazimwi yaliyo na sifa za viumbe dhahania ya majini. Majini haya yanasawiriwa yakiwa na tabia zilizokiuka hali ya binadamu wa kawaida na kuwa na sifa hasi licha ya uwezo wao.

Naye Matteru (1987) amesainisha tanzu za fasihi simulizi katika viwango vitatu, navyo ni Nathari, ushairi na semi. Ametaja aina mbali mbali za ngano kama hekaya isticara, kharafa na kuainisha ngano za kubuni na kihistoria. Yeye anaainisha vipera mbalimbali vya ngano za fasihi simulizi bila kuzama sana katika kila kipera kwa undani. Ngano za mazimwi ziko katika tapo la hadithi za kubuni. Jamii hubuni kazi kazi zake kulingana na mahitaji yake yanayooanishwa na mazingira wanamoishi na utamaduni wao. Ngano huainishwa kwa kuzingatia sifa mbalimbali mojawapo ikiwa ni wahusika wake.

Jamii ya Gĩkũyũ ni miongoni mwa jamii zinazounda Wabantu. Ingawa hakutaja kuhusu jamii zingine kama wanailoti, waandishi wengine kama Kabira na Mutahi (1988) wanatoa mfano

wa mhusika Arikon aliyezaliwa na mwanamke aliyetengwa na jamii yake na kisha akawa kijana jasiri aliyeilinda jamii yake dhidi ya mazimwi. Ngano hizi pia zinapatikana katika jamii ya Wamarakwet na zinajulikana kama 'Kimagetoi' kudhihirisha kuwa kipera hiki hakiko katika jamii ya wabantu pekee.

Fasihi simulizi hubadilika kama vile jamii inavyobalika kwa kuwa hakuna jamii ambayo haibadiliki. Kuhusu wahusika, Bukenya (1991) anasema kuwa fasihi simulizi hutumia wahusika wa kila aina si binadamu, si miungu, si viumbe dhahania, si mimea, si vitu ambavyo hutumiwa kuashiria hali, maadili muhimu na kadhalika. Lugha inayotumiwa huwa ni ya kiishara kwa kuwahuwa haina uhusiano wa moja kwa moja na maana ya kiashiriwa. Mwandishi huyu anakubali kuwa wahusika katika kazi ya fasihi huwa ni kiashiria cha mambo fulani katika jamii na hutumiwa ili kuwasilisha ujumbe unaokusudiwa na jamii husika. Madai haya yanaenda sambamba na nadharia ya Umuundoleo inayoeleza hali ya ishara moja kuwa na maana nyingi kwa kuikita kwenye muktadha wa kijamii.

Ndungo na Wafula, (n.d) wanasema kuwa tungo za fasihi simulizi hutegemea muktadha wa mazingira na zimejikita katika utamaduni wa jamii zinamoibuka. Msanii kwa mfano anapodhamiria kutoa picha ya kuogofya huchora mazingira yanayoogofya. Anaweza kutimia mazingira ya misitu na wahusika kama vile majitu ili kuleta dhana ya hofu. Kutokana na maelezo yao tunapata kuona umuhimu wa kuyachunguza mazingira ya jamii ambayo ndiyo husana utamaduni wao. Mazimwi yatasawiriwa kuwa na sifa fulani tofauti na ngano za jamii nyingine na hata uteuzi wa mbinu hutegemea dhamira ya ngano husika. Mawazo ya wasomi hawa yanafumbata ukweli kwa kuwa mazingira wanamoishi mazimwi yanaibua Taswira ya mazimwi na tabia.

Bukaayi akinukuliwa na Ndungo na Wafula, wanasema mazimwi katika ngano za jamii ya Wasoga yanadhihirisha binadamu wa kisasa katika jamii hiyo na ngano ni uhakiki na uchambuzi wa watu kujihusu na mazingira yao. Ngano hugusia masuala mbalimbali ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Masuala ya kijamii yanaangazia maadili kwa pakubwa. Anaongeza kusema kuwa, jamii ya leo inakumbwa na migogoro ya kimsingi ya kibinadamu ambayo huelekezwa kwa wanyonge na wenzao. Ngano hizi huwa zinaangazia yale yote yanayotukia katika jamii na kuyaweka wazi mambo yote yasiyofaa. Wahusika watasawiriwa kwa namna ambavyo jamii itaona mwafaka ili kupitisha ujumbe unaotakikana.

Msanii wa ngano za mazimwi huonekana kujitambulisha na wanyonge, waliokataliwa na waliodhulumiwa. Kulingana na Kabira na Mutahi (1988) anasema kuwa ni kutokana na haya tunapatamazimwi mara nyingi yakishindwa katika vita na maadui zao wanaokabilina nao kwa mfanokijana mdogo anayepigania jamii yake. Mfano mwema katika fasihi simulizi ni katika jamii ya Wamaasai ambapo kijana Arikon anapigana na zimwi na kulishinda. Kijana huyu anazaliwa na mwanamke aliyetengwa na kukataliwa lakini hatimaye analinda jamii nzima. Hapa katika kisa hiki, kijana aliyetengwa au kubaguliwa ndiye mnyonge na kule kulishinda Zimwi kunamfanya kusherehekewa.

Mazimwi husawiriwa kama viumbe wanaoishi miongoni mwa watu, wanaosemezana na kutagusana nao, lakini kwa njia ambayo si ya kirafiki kwa kuwa uhusiano wao huwa ni wa kuwanyanyasa wasio na nguvu kama watoto na akina mama. Kila mara mazimwi huwa katika harakati za kutafuta watu wa kuangamiza kwa kubuni mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutumia ujanja, kujidai kuwa binadamu wa kawaida na kuwatega wahasiriwa wasio na uwezo hasa wanapohitaji msaada kwa kuwafanya windo rahisi. Watoto huonywa dhidi ya kuingiliana na watu wenye tabia kama za mazimwi. Maoni haya yanalingana na yaliyo katika Makala ya Semina ya Fasihi Simulizi ya TUKI yanayoafiki kuwa wahusikahuchorwa kusimamia tabia, dhana au wazo.

Maelezo haya yanadhihirisha wazi kuwa ngano za mazimwi huwakilisha watu katika jamii walio na sifa na tabia fulani hasa hasi zinazokashifiwa na jamii. Mazimwi sio wahusika ambao wanapatikana katika mazingira maalumu bali huwa ni ishara za watu wenye tabia zisizopendeza na aghalabu wenye uwezo au mamlaka lakini wasio na utu. Adagala na Kabira (1985) anakariri kwamba wahusika wowote wale hutumiwa kuashiria hali halisi ya jamii kuonyesha wema uovu au mambo chanya na hasi ya binadamu. Mazimwi huwa na sifa za kula watu, katili, waharibifu, wapumbavu, wanaotumia nguvu zaidi kuliko akili, wasiotangamana vyema na watu wa kawaida na kadhalika.

Okech (2013) akimrejelea Mghanga (1984) aliyezihakiki ngano za Kidawida anaonyesha umuhimu wa kutumia lugha inayovutia katika kuwasilisha ujumbe katika ngano. Katika ngano hizi, alishughulikia maudhui ambayo ni msingi wa fasihi yoyote ile. Msimuliziwa ngano za fasihi simulizi au msanii hutumia lugha kwa njia ambayo itamwezesha kuwasiliana na wasomaji ama wasikilizaji wake kwa njia ya kuwavutia na ambayo itawafanya wasome ama wasikilize ujumbe wake. Lugha ndio malighafi ya kuumba sanaa ya fasihi na matumizi ya

lugha ama mtindo. Kwa msingi huu, kipengele cha mbinu za lugha na za kisanaa kinapewa uzito katika uhakiki wa ngano za mazimwi kutokana na sifa zake tofauti na aina zingine za ngano za fasihi simulizi.

Vipengele mbalimbali vinaingiliana na kukamilishana ili kufanikisha lengo la ngano hizo. Mfano msuko wa ngano unajengwa na jinsi wahusika mbalimbali wanavyokuzwa na kusawiriwa. Majukumu wanayopewa na migogoro inayoibuliwa na mwingiliano wao hukuza maudhui mbalimbali kupitia kwa mbinu mbalimbali za lugha na sana. Aidha zinawasilisha ujumbe kwa njia inayovutia hadhira.

Nandwa na Bukenya (1983) wakimnukuu Mbithi wanasema kuwa katika jamii ya Wakamba, mazimwi yanaaminika kuwa roho za watu waliokufa zamani sana kiasi cha kutoweza kukumbukwa na hujitokeza katika ngano. Wanasema wao hupatikana katika ulimwengu wa kiroho. Mazimwi hawa huishi katika nyumba kama binadamu wa kawaida au mapangoni. Anaongeza kusema kuwa wao hufanya shughuli kama watu wengine kama vile kulima, kufuga mifugo na hata kuwa na familia. Watu huwaogopa kwa kuwa ni waharibifu na huwala na kuwaua watu. Huweza kula kiasi kikubwa cha chakula na hata kuwameza watu na hatimaye wanaposhindwa na mashujaa huwaeleza jinsi ya kuwarejesha wote wale waliomezwa hapo awali.

Kulingana na jamii ya Wataita, hawani viumbe ambao wana uwezo mwingi kuliko binadamu wa kawaida na huweza kufanya kazi na kwenda kwa kasi sana. Wanaamini mazimwi hung'amua siri za binadamu kwa urahisi na hivyo kusawiriwa kuwa na sifa ya kiroho au iliyopita hali ya uhalisia. Huwa vigumu sana kwa binadamu kuwaua. Baaadhi ya jamii huamini kuwa mazimwi huweza kufanya mambo ya kiajabu kama kufufua wafu na kutema moto. Kuna mazimwi ambayo hufanya urafiki na binadamu na hata kuwasaidia wakati wa shida au hata kuoja wasichana.

Katika upande wa fani, wataalamu na wahakiki wa fasihi wanakubaliana kuwa fani ni jumla ya viambajengo vya kazi ya kifasihi vinavyotumiwa na msanii katika kupitisha ujumbe wake kwa hadhira. Wataalamu kama vile Wamitila (2003), Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa fani hutumiwa kueleza muundo au mpangilio wa kazi fulani ya kifasihi au hata sehemu zake. Wanahoji kuwa fani hueleza mbinu na mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo au maudhui.

Wamitila (2003) anasema kuwa ishara ni kitu fulani katika kazi ya fasihi ambacho huwakilisha kingine kutokana na uhusiano uliopo kati ya vitu hivyo viwili au uwezo wake wa kuibua fikira fulani katika akili ya msomaji. Kuna 'ishara bia' na 'ishara zisizo bia'. Ishara bia huweza kutambuliwa na watu wengine popote pale walipo. Kwa mfano, mto kutumika kama ishara ya kuonyesha mpito wa maisha, mlima kuashiria matatizo, mvua kuashiria neema, pete kuashiria ndoa n.k. Ishara zisizo bia ni zile ambazo maana zake hueleweka katika muktadha wa kazi inayohusika.

Ishara zinazotokana na muktadha wa ngano ndizo zitakazochunguzwa kwa vile ngano zinaeleweka vyema kwa kurejelea muktadha na jinsi wahusika wanasawiriwa ili kuwasilisha ujumbe. Kezilahabi (2007) katika kazi ya Dunia uwanja wa Fujo, ndege anayeruka kwa shida anaashiria kuvunjika kwa ndoto za Tumaini pamoja na hatima yake ya kujiendeleza kibinafsi na kuifikia furaha.

Mbatia (2001) anasema kwamba dhana ya fani ina maana mbili. Kwanza ni jumla ya vipengele vya kimitindo na kisanaa katika kazi ya kifasihi vinavyojenga kiunzi cha kubebea ujumbe au maana mahususi. Pili ni kategoriaya fasihi, yaani utanzu kama ushairi, drama na riwaya. Kupitia kwa wataalamu hawa tunaona ya kwamba wote wawili wanaelekea kukubaliana katika kijejezi cha kwanza kuwa fani ni vipengele vyakimitindo na kisanaa vinavyojenga kiunzi cha kubebea ujumbe na maana mahususi. Kijejezi hiki kina maana kuwa fani ni zile mbinu ambazo msanii anatumia ili kuifikishajumbe wake kwa hadhira lengwa. Uhakiki wa ngano za mazimwi hautaweza kukamilika bila kuchunguza kipengele cha fani ili kuweza kuzifahamu na kuweza kutambua umuhimu wa ngano hizi katika jamii.

Kimsingi, kazi za kifasihi huwa zimegawika katika sehemu mbili kuu. Maudhui na fani. Maudhui ni masuala mbalimbali yanayozungumziwa na mtunzi katika kazi ya kifasihi. Maudhui pia hujulikana kama yaliyomo. Kwa upande mwingine fani huwa ni vipengele vya kisanii vitumiwavyokuyawasilisha maudhui. Mbali na kuyawasilisha maudhui, fani pia huwa na uamilifu wakuupa utungo wa kifasihi umbo mahususi.

Umbo katika kazi za fasihi linaweza kuwa la ndani au la nje. Kuhusu ngano zilizochambuliwa, umbo la ndani hujengwa kwa matumizi ya lugha, wahusika, usimulizi na kadhalika. Uhakiki wetu haujishugulishi na umbo la nje kwani hushughulikiwa zaidi katika tungo za kishairi ambapo umbo la nje hujengwa kwa vipengele kama vile beti, mishororo,

vina, mizani na kadhalika. Wataalamu wa nadharia ya umuundo wanasisitiza na kutilia mkazo uhakiki wa kifani katika kufasiria matini na kupimia kufana au kutofana kwa mtunzi katika kazi yake ya usanii. Uhakiki wetu unaangazia pia kipengele cha fani kwa pakubwa pamoja na umuhimu wa ngano hizi katika jamii.

2.2 Maudhui Katika Ngano za Mazimwi

Maudhui ni masuala mbalimbali yanayozungumziwa na mtunzi katika kazi ya kifasihi. Maudhui huwa ni yaliyomo au masuala yanayojitokeza katika kazi ya fasihi. Njogu na Chimera (1999) wanasema maudhui ni sawa na ujumbe na huwa si changamano sana katika ngano kama katika riwaya au tamthilia. Hii ni sababu mojawapo muhimu ya kutosahaulika kwa ujumbe katika ngano na umegandamana na vipengele vya fani mfano katika nyimbo, methali hasa mwishoni mwa hadithi.

Ujumbe katika ngano za mazimwi huwa unatokana namatendo ya mazimwi ambao ni wahusika wakuu kama ilivyo katika ngano zingine za fasihi simulizi ambazo hugusia masuala mbalimbali ambayo huibua maudhuimbali kulingana na hadithi inayosimuliwa na dhamira inayoniwa. Maudhui mbalimbali yamechunguzwa yaliyojitokeza katika ngano za mazimwi zilizochagulia ili kudhihirisha masuala ya kijamii yaliyoshughulikiwa. Maudhui haya yatachangia kuelewa dhamira na dhima ya ngano za mazimwi katika jamii ya Gikũyũ.

Makala ya TUKI (1983:22) yanaeleza kuwa jamii aghalabu hudumisha yale mambo iyaonayo kuwa na manufaa kwake na yale yasiyo na manufaa au manufaa yake yamekwisha hufa na kupotea. Kutokana na mahitaji haya, fani mbalimbali hubuniwa na jamii husika ili zatumike kutimiza mahitaji ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ya jamii hizo. Masuala haya ndiyo huibua maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika kazi za fasihi. Ngano mbalimbali za mazimwi zimeangazia maudhui tofauti ingawaje maudhui mengi yamejirudia hasa yanayohusu masuala ya kijamii.

2.3 Wahusika Katika Ngano za Mazimwi

Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya kifasihi; matendo ya viumbe hawa hufanana na yale ya binadamu. Kulingana Njogu na Chimera (1999), huweza kuwa binadamu, mazimwi, pepo au vitu visivyoo hai kama mawe. Wanaongeza kuwa mhusika mkuu katika ngano anaweza kuwa jitu katili lisilopenda mabadiliko na hivyo likaangamizwa. Kwa

upande mwingine, mhusika akiwa mdogo wa umbo, akili yake huwa kubwa sana na kuitumia barabara na kuishinda mijitu mikubwa mikubwa au mazimwi na kuiangamiza.

Wamitila (2003) anasema kuwa ni kiumbe wa kisanii ambaye ameumbwa makusudi ili kutekeleza majukumu fulani ya kisanaa anayodhamiria msanii. Wahusika huweza kuwa watu, wanyama, ndege, wadudu miti, mashetani, majini n.k wanaotumiwa na watunzi katika utendaji na upitishaji wa ujumbe. Matendo, mienendo, maneno, vionjo (furaha, kero, machukizo), uhai na ufu wake vinadhitiwa kwa kiasi kikubwa na dhamira na lengo la msanii.

Wahusika hawa huingiliana kwa njia nyingi na katika mahusiano yao tunapata mwanga na kuweza kuelewa jamii kama mfumo wa maumbo uliokamilika. Ni muhimu kuangalia wahusika kama viwakilishi vya binadamu katika jamii halisi kwani kila mhusika huwa na sifa nzuri au mbaya zinazopatikana katika binadamu wa kawaida. Kulingana na Njogu na Chimera (1999), kutokana na sifa walizosawiriwa nazo ili kuendeleza maudhui na dhamira, tunapata aina mbalimbali za wahusika kulingana na nafasi zao.

Mwangi (1970:17), anasema kuwa wahusika wema huwakilisha maadili mema kama:ustahimilivu, usamehevu na ukarimu bali wahusika wabaya husawiriwa wakiwa na sifa hasi kama: wivu, ukaidi na ukatili. Wahusika wema hutuzwa ilhali wabaya huadhibiwa

2.3.1 Sifa za Mazimwi Katika Ngano za Mazimwi.

Maelezo ya wasomi mbalimbali, yanadhihirisha sifa mbalimbali zinazojitokeza katika ngano za mazimwi katika jamii mbalimbali zilizo na ngano ambazo wahusika wake ni mazimwi. Baadhi ya sifazinazojitokeza ni kama zifuatazo:

Nandwa na Bukenya (1983) wanaeleza kuwa ngano hizi za mazimwi husawiri wahusika wake kuwa na maumbile ya ajabu na wanakaribia wanyama au majini hasa jamii zilizo na imani ya dini ya Kiislamu Wahusika wake huweza kujigeuza wakachukua sura ya binadamu; nusu binadamu, nusu mnyama au akachukua umbo jingine la ajabu kama vile kuota mkia, macho matatu, midomo miwili na kadhalika. Mazimwi hutenda mambo kama binadamu katika shughuli za kawaida kama kuoa, kulima, kudhulumu na hata huweza kutuza wanaowatii.

Finnegan (1977) Husawiriwa kama wahusika mahasidi wenye tamaa na uovu katika jamii. Kwa mfano, wanaweza kumeza kijiji kizima na kuangamizana wenyewe kwa wenyewe. Mazimwi huwa adui wa binadamu na huwahangaisha sana kwa kuwala, kuwatisha, kuwaibia, kuwaharibia mali na kuvuruga amani katika jamii.

Nandwa (1983) anatoa sifa kama mazimwi kuwa na uwezo wa kujibadilisha kimaumbile kutoka umbo moja hadi jingine. Kama vile; mti, msichana mrembo, kisima, ndege maridadi au mnyama fulani na kadhalika. Anasema kuwa wanaohangaishwa sana na mazimwi ni wanawake, watoto na watu wanaotembea usiku au kwenda katika maeneo fulani. Aghalabu mazimwi hushindwa nguvu na kufa. Kwa mara nyingi watu walioliwa au kumezwa na mazimwi hutokeza kabla ya kifo chao. Huwa na wahusika majitu walio na uwezo wa ukiamambile. Kwa mfano uwezo wa kula watu katika kijiji kizima.

Kulingana na Kabira (1988), mazimwi hushindwa katika nyingi ya vita na maadui zao wanaokabilina nao hadithi za mazimwi na kwa hivyo ngano hizi huishia kuwa na mwisho maalumu mzuri wenye kutoa matumaini kwa jamii.

Mwangi (1970), anasema mazimwi kwa kujumla huashiriwa upande muovu wa binadamu na ngano za mazimwi hutufunza kuhusu: uaminifu, kufuata ushauri na kutokuwa wabaya.

Jamii mbalimbali huwa na ngano zilizo na sifa za kipekee ingawa nyingi ya sifa hizi zinajitokeza katika ngano nyingi.

2.4 Msuko

Msuko ni mtiririko au mfululizo wa matukio yanayojenga hadithi na namna matukio hayo yanavyosababishana kama wasemavyo Njogu na Chimerah (1999) Wanaendelea kueleza kuwa msuko unaweza kuelezwa kama mtiririko wa vitendo na namna vitendo hivyo vinavyozuana. Kwa ujumla msuko hurejelea mpangilio wa matukio yanayopatikana katika ngano na huhusisha matendo ya mhusika mkuu na jinsi yanavyoathiri wahusika wengine katika kazi ya kifasihi. Kwa kawaida msuko hueleza jinsi ambavyo matukio yanavyoingiliana.

Wamitila (2003) anasema kuwa msuko ni mfuatano wa matukio yanayopatikana katika kazi ya kifasihi kwa kutegemea uhusiano wake kiusababishi. Ni kipengele muhimu cha kimuundo katika hadithi yoyote ile. Muundo huu ndio anaouita msuko. Kwenye sehemu ya kitangulizi, panazuka mvutano wa usimulizi ambao unaendeleza mgogoro kati ya wahusika walioko na

harakati zao hadi kilele cha usimulizi au upeo na hatimaye mwisho wake. Mfuatano huu wa matukio huleta taharuki msisimko na mshangao. Msuko huweza kuwa sahili au mwepesi au ukawa changamano mfano katika riwaya. Utafiti katika kipengele hiki ataangalia jinsi matukio ya ngano za mazimwi yalivyopangika kuanzia mwanzo kwenye kitangulizi hadi mwisho.

Kimsingi kuna aina mbili za msuko: Msuko sahili na msuko changamano. Msuko sahili ni aina ya msuko ambao ni wa moja kwa moja. Hoja hii ina maana kuwa msuko sahili huwa na matukio yanayotiririka kuanzia mwanzo hadi mwisho. Matukio hufuatana kiwakati na kiusababishi. Msuko sahili hauna urejelezi wa nyuma. Aghalabu msuko wa aina hii hupatikana katika tungo fupi kama ngano na mashairi.

Kwa upande mwingine, msuko changamano ni aina ya msuko ambao huenda mbele na nyuma. Hoja hii ina maana kuwa msuko wa aina hii hutumia mbinu rejeshi kwa wingi. Kutokana na hali hii huwapa wasomaji hamu ya kuendelea kusoma zaidi na zaidi ili wapate kufuatilia hadithi husika na kupata maana. Kulingana na Ngara (1985) msuko changamanohujulikana kama msuko wa kioo. Wanasema msuko wa aina hii huwa na kipengele cha wakati na vipengele kama wahusika na usimulizi ambapo lazima kuwepo na mahusiano ya vipengele hivi na matukio ambayo yanatendwa katika nyakati tofautitofauti.

2.5 Dhana ya Fani

Kulingana na wataalamu na wahakiki wa fasihi kama Wamitila (2003), Njogu na Chimerah (1999), fani ni jumla ya viambajengo vya kazi ya kifasihi vinavyotumiwa na msanii katikakupitisha ujumbe wake kwa hadhira. Vipengele vya fani vinavyotumika sana katika ngano ni kama vile: ishara, chuku, tanakali za sauti, taharuki, nyimbo, taswira miongoni mwa tamathali za usemi nyingine. Fani hueleza mbinu na mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo au maudhui.

Mbatiah (2001) anasema kwamba dhana ya fani ina maana ya vipengele vya kimtindo na kisanaa katika kazi ya kifasihi ambavyo imegawika katika sehemu mbili kuu yaani maudhui na fani. Vipengele hivi vinaingiliana na kutegemeana. Maudhui ni masuala mbalimbali yanayozungumziwa na mtunzi katika kazi ya kifasihi ilhali fani huwa ni vipengele vya kisanii vitumiwavyo kuyawasilisha maudhui. Fani pia huwa na jukumu la kuupa utungo wa kifasihi umbo mahususi ambao hujengwa kutokana na muingiliano baina ya vipengele

mbalimbali vya kifani kama vile usimulizi, msuko, wahusika na matumizi ya lugha. Kwa hivyo muundo wa ndani ndioumezingatiwa kwa kuwa unaingiliana sana na msuko, yaani mfuatano wa matukio na mahusiano yake kiwakati na kiusababishi.

Fani ni zile mbinu ambazo msanii anatumia ili kuufikisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Wamitila (2003) anaeleza fani hueleza mbinu na mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo au maudhui. Naye Mbatiah (2001) anasema kwamba dhana ya fani ina maana ya vipengele vya kimtindo na kisanaa katika kazi ya kifasihi vinavyojenga kiunzi cha kubebea ujumbe au maana mahususi.

Kimsingi, kazi za kifasihi huwa zimegawika katika sehemu mbili kuu: Maudhui na fani. Fani huwa ni vipengele vya kisanii vitumiwavyo kuyawasilisha maudhui. Mbali na kuyawasilisha maudhui, fani pia huwa na uamilifu wakuupa utungo wa kifasihi umbo mahususi. Umbo lenyewe linaweza kuwa la ndani au la nje ambapo umbo la ndani hujengwa kwa matumizi ya lugha, wahusika, usimulizi n.k. Wataalamu wa nadharia ya umuundo wanasisitiza na kutilia mkazo uhakiki wa kifani katika kufasiria matini na kupimia kufana au kutofana kwa mtunzi katika kazi yake ya usanii. Wataalamu na wahakiki wa fasihi wanakubaliana kuwa fani ni jumla ya viambajengo vya kazi ya kifasihi vinavyotumiwa na msanii katika kupitisha ujumbe wake kwa hadhira.

Mbinu mbalimbali za lugha na za sanaa zilizojitokeza na kuchanganuliwa ni pamoja na ishara, taharuki, majazi, tashihisi, tashbihi, tanakali za sauti, chuku, takriri, nyimbo, taswira, misemo miongoni mwa mbinu nyingine.

2.6 Takriri

Hii ni mbinu ya kurudiarudia. Msokile (1992:61) anaeleza kuwa; “Takriri ni urudiaji wa silabi, maneno, mistari au vifungu vinavyolingana katika kazi ya sanaa”. Lengokuu la msimulizi kurudiarudia maneno au vipengele hivyo ni kulitilia mkazo jambo linaloelezwa. Urudiaji ni wa aina nyingi kama wa neno na mtindo au usambamba. Hujitokeza kupitia kwa nyimbo zinazorudiwarudiwa na pia katika mtindo ili kuisisitiza, kusaidia katika kukumbuka au kuibua hisia.

Usambamba ni aina maalum ya urudiaji katika matumizi ya lugha ambao hupatikana katika kiwango cha kirai, kishazi au sentensi. Kuna aina mbalimbali za usambamba. Miongoni mwa

aina hizi ni usambamba wa kimuundo na usambamba wa kisintaksia. Usambamba wa kimuundo ni aina ya urudiaji ambao hujengeka katika urudiaji wa muundo ulio sawa. Urudiaji wa aina hii hupatikana sana katika nyimbo za ngano na katika ushairi wa Kiswahili ambapo muundo sawa wa baadhi ya mishororo hurudiwa katika beti mbalimbali.

Aidha kuna taswira za kimaelezo zinazounda picha za kiishara zinazoashiria jambo fulani au zinazoficha ujumbe mwingine. hujengwa kwa matumizi ya tamathali za usemi kama tashibiha na sitiari. Sababu moja ya kutumia taswira ni kumfanya au msikilizaji au msomaji aelewe ujumbe kwa njia inayokusudiwa.

2.7 Taswira

Taswira ni picha ambazo humjia msikilizaji akilini anaposikiliza au anapoisoma kazi fulani ya kifasihi. Picha hizi hujengwa kwa maelezo fulani. Wamitila (2003) anasema kuna aina tofauti za ishara kutegemea aina ya picha inayoundwa akilini kama vile taswira: taswira sauti, taswira uoni, taswira harufu, taswira mguso, taswira mwendo, taswira joto, taswira mwonjo, taswira za kimaelezo, taswira za kiishara na taswira za usikivu.

2.8 Ishara Katika Ngano za Mazimwi

Wamitila (2003) anasema kuwa ishara ni kitu fulani katika kazi ya fasihi ambacho huwakilisha kingine kutokana na uhusiano uliopo kati ya vitu hivyo viwili au uwezo wake wa kubua fikira fulani katika akili ya msomaji. Kuna ‘ishara bia’ na ‘ishara zisizo bia’. Ishara bia huweza kutambuliwa na watu wengine popote pale walipo. Kwa mfano, mto kutumika kama ishara ya kuonyesha mpito wa maisha.

Griffen (1997) alisema kuwa ishara ni kitu tunachokumbana nacho moja kwa moja na huweza kuashiria kitu kingine tofauti. Katika kazi ya kifasihi, ishara huelezea kitu fulani kinachowakilisha kingine kutokana na uhusiano uliopo kati ya vitu hivyo viwili au pia kutokana na uwezo wake wa kuibua fikira fulani akilini mwa wasomaji au msikilizaji. Ishara huwa ni kiashirii cha kitu kingine.

Kulingana na Aston na Savona (2005) ishara hushughulikiwa katika kipera kinachojulikana kama semiotiki ya kijamii. Huhusisha itifaki za kuelekeza mawasiliano, mazoea yanayodhibiti majukumu ya mawasiliano ya kijamii. Huwa zimegawanywa katika vikundi viwili ambavyo ni: ishara za utambulisho kama vile bendera, na, ishara za kihulka au za

kitabia. Kwa mfano, salamu, hali ya sauti, matusi na hata ujielezaji waliongeza kuwa ishara na sitiari hutumika kama vifaa vya kumfikirisha mtu. Ishara za kijamii ni ishara za ambazo huhusiana na ishara za kiuajumi, kiutamaduni na za kihistoria. Huwa ni ishara maalum.

Wana-Umuundoleo wanaieleza hali ya ishara moja kuwa na maana nyingi kwa kuiweka au kuikita maana kwenye muktadha wa jamii. Baadhi ya ishara za jadi kama vile 'bundi' huweza kuwa na maana zaidi ya moja kiishara. Katie (2001:380) alisema kuwa miongoni mwa Waingereza 'bundi' ni ishara ya hekima. Hata hivyo, kwa Waafrika wengi bundi huashiria nuksi au mauti kama alivyosema Wamitila. Ishara za jadi ni aina ya ishara za kijamii.

Waasisi wa nadharia ya Umuundoleo wanadahili kuwa ishara haziwi na maana ya ndani bali huipata maana yake kupitia kwa lugha inayohusika. Mazimwi huwakilisha dhana mbalimbali kulingana na msuko wa ngano na usawiri wa wahusika.

2.9 Tamathali za Usemi

Holman na Harmon (1986) na Kuhenga (1977) wanasema kuwa tamathali za usemi ni dhana ya kifasihi ambayo hutumiwa kuelezea aina ya ukiushi wa kimaksudi katika matumizi ya lugha ya kawaida au iliyozeleka. Huwa ni fungu la maneno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine. Tamathali ya usemi huwa ni mbinu ya kupimia usemi wa mtunzi. Ubunifu lazima ujitokeze katika matumizi ya tamathali mbalimbali za usemi.

Huwafanya wasomaji kutafakari kuhusu wanayoyasoma na kulinganisha na mazingira na mandhari yao. Huvutiawasomaji na kuwapa hamu ya kutaka kusoma zaidi. Tamathali huchukuanafasi muhimu katika kazi za kifasihi na hasa ngano. Tamathali hizi ni kama: sitiari, tashbihi, kinaya, chuku, maswali ya balagha, nidaa, usambamba, tashihisi na taashira.

2.3.1 Semi

Wamitila K. (2003) anakubaliana na kauli hii kwa kueleza kuwa semi ni neno lenye upana ambalo hutumiwa kuelezea matamko fulani yanayoelezea ukweli fulani. Aidha, semi ni kauli za maneno kadha yenye maana iliyofichika. Utanzu huu unahusishwa vipera kama: misemo, nahau, methali, mafumbo, lakabu n.k. Misemo ni matumizi ya maneno ya kawaida kwanjia

iliyofichika au isiyokuwa ya wazi. Misemo huhitaji mtu kufikĩrĩa kwanza ndiposa afichue maana ya maneno husika.

Misemo katika jamii moja hutofautiana na jamii nyingine. Hii ni kwa sababu baadhi ya misemo hutungwa kutokana na mazingira pamoja na itikadi za jamii. Misemo hutumika kwa lengo la kusetiri maana na pia kumfanya msomaji kutafakari ujumbe uliopo. Misemo mingine hutokana na kisa au tukio fulani katika jamii husika na hivyo basi, ili kujua maana na matumizi yake inampasa mwanajamii kufahamu asili yake.

2.3.2 Tashbihi

Tashbihi ni mbinu ya mlinganisho wa vitu viwili au zaidi vyenye sifa zinazolingana, tashbihi hutumia viungo vya ulinganishaji. Msokile (1992) anafafanua kuwa aina hii ya tamathali hutumia ulinganisho wa mamboama vitu kwa kutumia maneno kama: ja, kama kwamba mithili ya, mfano wa, sawa na na kama na kadhalika. Mtunzi hutumia ulinganishi huu kuisitiza sifa fulani na pia kujenga picha ya aina fulani akilini.

2.3.3 Chuku

Ni mbinu inayotumika kueleza hali ya kukikuza kitu mtu au hali kupita kiasi au kwa kutia chumvi. Chuku pia hujulikana kama udamisi. Matumizi ya mbinu hii hudhamiriwa kuisitiza sifa hiyoya ukubwa au udogo. Kauli zinazotumika katika mbinu hii huwa ni za kutiliwa chumvi ili kuisitiza na pia kuifanya kazi ivutie . Kwa kutumia chuku, sifa za kawaida za kitukinachohusika hukiukwakwa kudunishwa au kukuzwa zaidi kuliko kawaida yake. Matukio mengi huwa yamepigwa chuku katika ngano kupitia kwa wahusika wakekwa upande wa matendo, sifa, majukumu, maumbile n.k.

2.3.4 Tashihisi

Wales (2001:349) anafasili tashihisi kuwa; ‘Ni tamathali ya usemi ambapo kitu kisicho na uhai, mnyama, kisicho binadamu au chenye sifa zakidhahania kinapewa sifa zabinadamu.’ Tamathali hii hutumiwa kuleta mvuto wa kisanaa na athari fulani za kihisia. Tashihisi hutumika sana katika uhusika wa ngano za fasihi ambapo vitu visivyo hai, wanyama, ndege, sadudu n.k. hupewa sifa za binadamu za kusema na kutenda.

2.3.5 Balagha

Hii ni mbinu ya kutumia maswali yasiyohitaji majibu kwa nia ya kusisitiza au kuibua hisia. Mbinu hii hutumiwa sana na msimulizi kuteka hisia za hadhira.

2.3.6 Nidaa

Hii ni mbinu ambayo hutumika kuonyesha hisia fulani kama vile mshangao, furaha, hasira au kukataa jambo fulani. Alama ya mshangao hutumiwa kuleta hisia iliyokusudiwa. Mbinu hii pia hutumika sana katika ngano za fasihi simulizi ili kuibua hisia zinazodhamiriwa na msimulizi.

2.3.7 Tanakali za Sauti

Tanakali ni neno ambalo huiga sauti fulani, jinsi kitu kiangukavyo au kilivyo. Msingi mkuu wa matumizi ya mbinu hii ni kumwezesha msomajikupata taswira kamili na hisia za mlio wa kitu kinachozungumziwa Wamitila (2003) anathibitisha kauli hii kwa kusema kuwa tanakali sauti hutumiwa kurejelea sauti ambayo inaigiza jinsi kitu fulani kiangukavyo, kiliavyo, kilivyo n.k. Katika uhakiki, wataalamu wanatofautisha kati ya tanakali sauti inayotuletea hisia za mlio wa kitu fulani na tanakali sauti inayotukumbusha maneno yanayohusiana na neno fulani maalum.

2.10 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Umuundo na Umuundoleo ambao umetumika katika kuchanganua vipengele mbalimbali vya ngano za mazimwi zilizoteuliwa. Nadharia hii inabainisha jinsi vipengele mbalimbali vinaungana na kuunda umbo la kazi nzima. Nadharia ya umuundo inahusishwa na wanaisimu wa shule ya Prague walihusika na Urasimu wa Kirusi. Kuzuka kwa shule ya isimu ya Prague kulihusishwa sana na urasimu na hasa kikundi kimoja cha wanaisimu wa Moscow. Mawazo ya mwanaisimu wa ki-Swizi, Ferdinand de Saussure yalikuwa na athari kubwa katika ukuaji wa nadharia hii. Roman Jakobson, Mukarovsky, Trubetzkoy, Boris Tomasevsky na Ren Wellek waliendeleza.

Wahakiki hawa baadaye walichunguza sanaa wakiilinganisha na hali za jamii au hali za kijamii pamoja na jinsi kazi za kifasihi zinavyoashiria uhalisi uliopo nje ya mawanda ya lugha. Wasomi hawa waliathiriwa na mawazo ya Ferdinand de Saussure kuhusu dhana za kiisimu za 'Langue' na 'Parole'. Saussure alibaini kuwa Parole ni lugha ya kimatumizi

ilhali 'Langue' ni mfumo lugha ulio na jumla ya taratibu za lugha ambazo msemaji wa lugha hizo anazifahamu. Kulingana na Saussure 'Langage' huundwa kwa "Langue na Parole."

Kwa kurejelea dhana hizi, wana-Umuundo walielezea kuwa fasihi inaweza kuangaliwa kama mfumo wenye kanuni zake ambazo kila msanii anahitaji kuelewa na pia aelewe jinsi ambavyo mfumo huo unavyoweza kutumiwa katika mawasiliano na hata kimuundo. Walisisitiza kuwa ili kuelewa mfumo wa kazi ya kifasihi, lazima mhakiki achunguze matumizi ya lugha katika maandishi au mazungumzo, vipashio vyake na mahusiano ya vipashio hivyo. Kwa mantiki hii, wanaumuundo walielekea kuashiria kuwa fasihi ni mfumo unaojisimamia kama 'Langue' kwa kuwa na kanuni zake.

Umuundoleo hutumiwa kuelezea mikabala ya uhakiki iliyozuka kuyapinga au kuyaendeleza mawazo yaliyokuwako kwenye umuundo. Mikabala hii inahusishwa na kazi za Jacques Derrida, Julia Kristeva, Michel Foucault, Jacques Lacan na Louis Althusser. Umuundoleo unavyazwa na mawazo mbalimbali ya kinadharia na misingi mbalimbali inayoishia kuyadadisi baadhi ya mawazo yanayohusishwa na isimu-muundo ambayo kitovu chake ni Ferdinand de Saussure ambaye aliieleza lugha kama mfumo wa ishara ambazo huungana na kuunda 'mkufu wa ishara.' Kila ishara huwa na sehemu mbili kuu: kiashirii na kiashiriwa. Maana za ishara ni za kihusiano nasaba tu na ishara moja hupata maana kutokana na ishara iliyopo kati yake na ishara nyingine.

Wana-Umuundoleo walieleza hali ya ishara moja kuwa na maana nyingi kwa kuiweka au kuikita maana kwenye muktadha wa kijamii, yaani jamii inakuwa na athari kubwa juu ya maana. Wana-Umuundoleo wana mawazo kuwa kiashiriwa hakiwezi kuwa funge. Wahakiki wanadahili kuwa katika miktadha mingi ya matumizi ya kiashirii, kiashiriwa chake au maana huhamishwa au huashiriwa. Lugha huchukua nafasi kubwa katika kuuhakiki na kuuchanganua mpangilio na muundo wa kijamii wa maana pamoja na nguvu au uwezo na ung'amuzi au urazini wa kibinafsi ambapo lugha huangaliwa kama jira maana halisi au zinazowezezana, aina ya mipangilio ya kijamii pamoja na matokeo yake huelezwa. Mkabala wa ki-Umuundoleo unashikilia kuwa maana huundwa katika lugha na kwa hivyo inaweza kusemwa kuwa inafumbatwa na kuahidiwa na msemaji

Hivyo kazi ya kifasihi inafaa kuangaliwa kwa mujibu wa kanuni za utunzi zinaoitawala. Kwa mfano katika uhakiki wa ngano za mazimwi za Gĩkũyũ, tunastahili kuchunguza lugha

ilivyotumika pamoja na kaida zinazotawala utunzi wa hadithi na kutathmini ikiwa mtunzi anatekeleza kaida hizo. Mazimwi kulingana na mkabala huu huweza kuwa ishara ya jambo fulani kwa kuwa maana halisi hueleweka katika jamii kwa vile ni ishara ya kile kinachokusudiwa.

Wafula na Njogu (2007) wakiwanukuu Leech na Short (1981) wanaeleza kwamba, “Fasihi ni umbo lenye viungo viwili, maudhui na fani na kwamba viungo hivi vyaweza kutenganishwa. Hapa muundo unafananishwa na mtindo ukimaanisha lugha inayotumika katika maandishi au mazungumzo ya kifasihi”. Kauli ya Short ni kwamba wazo kwanza huota katika fikra za mwanasanaa au msemaji yeyote wa kifasihi. Wadhifa wa mwanasanaa ni kuainisha na kutumia lugha inavyofaa kuelezea wazo.

Wanaeleza pia kuwa umuundo huleta pamoja vipengele mbalimbali vya lugha na kuvipa umbo moja lisiloweza kugawika kwani viungo hivyo haviwezi kutenganishwa na kujisimamia kisha vikaleta maana. Kazi hii ni muhimu sana kwani itatuelekeza vizuri kuhusu nadharia itakayotumia inavyobainisha lugha katika vitengo viwili yaani lugha dhahiri na lugha dhahania na jinsi ambavyo matawi mbalimbali ya lugha hayawezi kufasiriwa nje ya mipaka ya muundo yaani lugha ni mfumo wa muundo unaojitosheleza na unaojieleza.

Nadharia hii husisitiza vipengele vya kazi ya sanaa jinsi vinavyohusiana kuikamilisha kazi hiyo kama vile: maudhui, ploti, wahusika, muktadha na lugha. Huangalia namna sehemu mbalimbali za kazi ya sanaa zimefungamana. Wamitila (2002) anasema wanamuundo wanaamini kuwa matini ya kifasihi huwa na mpangilio wa viwango mbalimbali. Ni dhahiri kuwa nadharia ya Umuundo utatumiwa kwa kiwango kikubwa kuhakiki ngano za mazimwi kwa kuwa inaangazia mtindo na umbo la kazi ya fasihi nayo ya Umuundoleo ana katika kuhakiki ishara ya mazimwi katika ngano.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii imejumuisha mpangilio uliofuatwa katika utafiti ili kukusanya data. Aina ya data ambayo ilikusanywa ni ngano za mazimwi, ili kuhakiki ishara ya mazimwi na fani katika ngano hizo za mazimwi katika jamii ya Gĩkũryũ. Katika sehemu hii, mambo yafuatayo yalishughulikiwa; mhali pa utafiti, walengwa wa utafiti, uteuzi wa sampuli. Aidha, ukusanyaji data pamoja na jinsi data hiyo ilivyochanganuliwa ni suala jingine lililoshughulikiwa katika sura hii.

3.2 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu umeshughulikia ngano tano za mazimwi ambazo wahusika wake ni mazimwi. Katika jamii ya Gĩkũryũ, ngano za kubuni zinajulikana kama za mazimwi. Ngano hizi za mazimwi zina sifa mbalimbali ambazo zimejitokeza katika hadithi tofauti na ilibidi kuteua ngano tano ambazo zina wahusika ambao ni mazimwi ili kupata sifa na ishara za mazimwi katika ngano hizo. Ngano zilizoteuliwa na kuhakikiwa ni:

- (i) Zimwi na Msichana
- (ii) Mama Aliyefungua na Zimwi
- (iii) Mvulana na Zimwi
- (iv) Njiru na mvulana
- (v) Vijana Watatu na Zimwi

Ngano hizi ziliteuliwa miongoni mwa nyingine za mazimwi kwa kuchagua zile zisizokaribiana katika sifa zake kwa kuwa nyingi zina sifa zinazokaribiana ili kuepuka na urudiaji wa sifa na msuko. Uchambuzi wa ngano hizi umefanywa kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti huu. Ili kufanikisha uhakiki huu, nadharia ya umuundo na Umuundoleo imetumiwa. Aidha mbinu wanazozitumia wasanii katika uwasilishaji waujumbe zimechanganuliwa.

Ngano hizi tofauti zimeangazia hali mbalimbali na mtagusano wa wanajamii katika shughuli mbalimbali na maeneo tofauti ya kijiografia katika maeneo ya Mlima Kenya yanayosakiniwa

na jamii ya Gĩkũryũ. Utafiti uliangazia eneo la kaunti ya Nyandarua ambalo ni mojawapo ya sehemu wanamoishi jamii ya Gĩkũryũ.

3.3 Kikundi Lengwa

Utafiti huu ulilenga ngano zote za mazimwi katika jamii ya Gĩkũryũ. Utafiti ulifanywa katika kaunti ya Nyandarua eneo la katikaki mwa Kenya. Ngano zilizolengwa ni zile zilizo na wahusika ambao ni mazimwi kwa vile ngano zote za kubuni zinajulikana kama ngano za mazimwi. Mazimwi ndiyo wahusika wakuu au wahusika wadogo mradi ngano hizo ziwe zinazohusu mazimwi. Ngano hizi zilikusanywa kwa nia ya kubaini ishara ya mazimwi pamoja na fani iliyotumika katika ngano hizo.

3.4 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli katika utafiti huu ilituliwa kimaksudikwa kutumia sampuli-tajwa (Snowball sampling) ambapo wahojiwakumi na watano (15) wenye tajriba na weledi wa ngano walihojiwa kutoka jamii ya Gĩkũryũ katika eneo la Nyandarua. Kumi na watano walichaguliwa kwa kuwa idadi hii ni jumla ya wahojiwa watano watano kutoka kwa maeneo matatu makuu yajamii Gĩkũryũ yaani Kiambu, Muran'ga na Nyeri. Wajuzi hawa walipatikana kwa kutumia sampuli –tajwa ambapo wajuzi walitambuliwa na wanajamii wengine wanaowafahamu. Ngano asili za mazimwi za jamii ya Gĩkũryũ zilikusanywa na kurekodiwa kwa kutumia tepu-rekoda na kisha kuteua sampuli huru ya ngano tano (5) kati ya ngano zilizokusanywa ili zifanyiwe uchunguzi na uchanganuzi kubainisha vipengele vya fani na ishara katika ngano hizi.

3.5 Ukusanyaji wa Data

Data katika utafiti huu inayohusiana na ngano za mazimwi ilikusanywa kwa njia ya masimulizi kutoka kwa wahojiwa walioteuliwa kwa kutajwa na wahojiwa wengine kuwa na ujuzi wa kusimulia ngano. Mtafiti alizipata ngano za mazimwi kutoka kwa watu walioteuliwa kutokana na ujuzi na tajriba yao pana Ngano za mazimwi nyanjani zilirekodiwa kwa kutumia tepu rekoda. Ngano hizi kisha ziliandikwa na kutafsiriwa kwa Kiswahili na hatimaye kutumiwa katika Uchanganuzi.

3.6 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulifanywa nyanjani kwanza kwa kukusanya ngano kwa kutumia tepu rekodazilizokuwa na wahusika mazimwi kutoka kwa wajuzi waliopatikana kwa kutumia

sampuli tajwa ambapo wajuzi walitambuliwa na wanajamii wengine wanaowafahamu. Kisha zikateuliwa ngano tano kati ya zile zilizokusanywa hii ni kwa kuwa ngano Ngano nyingi zilifananana kujirudiarudialicha ya tofauti ndogondogokutokana na wasimulizi na maeneowanayotoka pamoja na mpito wa wakati. Aidha ngano zilizodhihirisha matumizi changamano ya fani zilipewa kipaumbele na kuteuliwa ili kumwezesha mtafiti kuchambua fani, ishara ya mazimwi, sifa za mazimwi, muundo, msuko na umuhimu wa ngano hizo katika jamii

3.7 Uchanganuzi wa Data

Data ilikayokusanywa ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi elezi. Uchanganuzi huu ni wa kiuthamano ambapo mtafiti alichanganua taarifa kwa mpangilio ili kupata ruwazailiyoonyesha uhusiano wa vipengele mbalimbali katika ngano. Katika uchanganuzi huu, mtafiti alipata taarifa kuhusu vipengele vya fani na ishara aliyotaka kuchunguzakwa kutokana na ruwaza na uhusiano kutoka kwa ngano hizi.

Jambo hili lilimwezesha mtafiti kutathmini ishara za mazimwi kama zinavyojitokeza katika ngano za mazimwi na dhima ya ngano hizi katika jamii. Uchanganuzi huo wa data ulifanywa kwa mintaarafu ya madhumuni ya utafiti huu. Ngano zilizoteuliwa za mazimwi pia zilichanganuliwa katika upande wa vipengele vya kimtindo vilivyovitumika kama vile: msuko, wahusika, maudhui na mbinu zilizotumika kwa mfano majazi, chuku, takriri, tashbiha na kadhalika. Matokeo yalitathminiwa kutegemea malengo na maswali ya utafiti.

SURA YA NNE

UCHANGANUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia mtindo wa ngano za mazimwi huku msisitizo ukiwa katika, msuko, wahusika na mtindo ambao unabainisha mbinu mbalimbali. Kwa kuchunguzauumbuji wa vipengele hivi, mtafiti amebainisha jinsi msuko wa ngano na jinsi anavyowasawiri wahusika wake kwakutumia mbinu mbalimbali kufanikisha malengo yangano. Uhakiki huu unahusu kuchanganua vipengele muhimu vya ngano pamoja na mbinu za kimtindo zilizotumika ikiwepo ya ishara ya mazimwi.

4.2 Uhakiki wa Ngano za Zimwi

4.2.1 Maudhui Katika Ngano za Mazimwi

Masuala yaliyojitokeza katika ngano za zimwi zilizoteuliwa yanaegemea sana katika kukuza maadili na kukashifu maovu. Mazimwi yanaendeleza maudhui hasi yaani mambo yanayoenda kinyume na maadili ya jamii kama vile: ukatili, ulaghai, ujinga, unafiki, tamaa, ubinafsi, vitisho na kadhalika. Kwa upande mwingine, wengi wa wahusika ambao si mazimwi wanakuza maudhui chanya kama: ujasiri, utu, ushirikiano, ukombozi, matumaini na kadhalika.

Wahusika ambao wanakaidi matakwa ya jamii hujuta na kuwa funzo kwa wale wasiofuata maadili mema. Kwa kuwa jamii ilidhamiri kutoa mafunzo yaliyoandamana namatakwa ya jamii, maudhui mengi yaliyowasilishwa na mazimwi yalikuwa hasi.

4.2.1.1 Ukatili

Ngano zote zilizoteuliwa zimeangazia maudhui ya ukatili kupitia kwa wahusika wanaotenda maovu dhidi ya binadamu. Maudhui haya yameendelezwa kwa pakubwa na mazimwi wanaowaua, kuharibu mali na kuwala watu au kutenda matendo ya kinyama kwa mazimwi mengine. Hadithi ya Zimwi na Msichana inaonyesha ukatili wa mazimwi inaonyesha kuwa mazimwi yalikuwa yakiwaua na kula watu kwa kuwa zimwi lilipokaribia nyumbani, lilikimbia ili kuondoa mifupa ya watu waliokuwa wameliwa awali ili wasichana wasije wakajua kuwa lilikuwa zimwi.

Msichana aliyekuwa amejitoa kwa moyo wake wote na kulipenda zimwi kwa dhati licha ya kukanywa, alipangiwa njama na zimwi lilo hilo kuangamizwa. Ni kitendo cha ukatili kulipa mema kwa maovu kama inavyodhihirika katika hadithi hii. Zimwi lilimkataza msichana hata kwenda haja na hata baada ya kumruhusu linamfunga kwa kamba kiunoni ili asije akatoroka.

Ngano ya Njiru pia inadhihirisha ukatili pale ambapo mbuzi aliyekuwa zimwi kumla kijana aliyekuwa akimchunga. Huku ni kukosa shukrani baada ya kutendewa wema. Isitoshe, Zimwi liliwameza watu katika kijiji kizima isipokuwa mama mmoja aliyejificha. Fauka ya hayo, mama alipokwenda kuomba moto kwanza akapewa masharti ya kunyolewe kwanza na alipokubali, zimwi lilimnyoa kikatili kwa kumkata na kula vipande vya nyama za kichwa chake. Ni jambo la kawaida mtu kutoa msaada bila masharti wala manufaa ya kibinafsi mtu anapoonyesha uhitaji.

Kupitia kwa wimbo uliokuwa ukiimbwa na zimwi, ni wazi kuwa lilifurahia kutenda maovu kama vile kula watu na mali yao. Linasherehekea kuweza kula watu na mifugo yao na kuwamaliza wote fyu! Linajitapa kwa kufanikiwa kuwaangamiza watu katika kijiji pamoja na mali yao wakati ambapo watu walihuzunika. Zimwi liliharibu maghala kabla ya kushambuliwa na vijana waliokuwa wamejivizia.

Sio tu mazimwi yaliyokuwa katili mbali hata binadamu kama vile mmoja wa vijana wawili waliotuzwa na wanajamii kwa kuikomboa jamii kutokana na dhuluma ya zimwi. Kijana huyu aliwalaghi watu baada ya kufuja mali yake yote. Alijifaidi kwa kutumia ujanja baada ya kupata msaada kama vile kumchomeka mbuzi wake kwenye pembe za fahali aliyekuwa mnono na mkubwa kuliko wote na kudai afidiwe kwa kupewa huyo fahali.

Kijana huyo hakukomea hapo baada ya kufidiwa kwa fahali. Aliwachinja wanakijiji fahali huyo akinuia kupata mali nyingi zaidi. Alijitajirisha kwa mali ya haramu huku wanakijiji wakipoteza mali yao. Watu walitozwa zaidi kuliko vile ilivyostahili. Kwa mfano aliyekula mbuzi alitozwa mbuzi thelathini na aliyenusa harufu ya nyama alilipa mbuzi kumi na akatajirika sana kutokana na kitendo kile cha haramu.

Maudhui ya ukatili yanaendelea kujitokeza katika ngano ya Vijana Watatu waliokwenda kutafuta wachumba. Walipokwenda kuomba moto kwa mama mzee ili wachome nyama walizokuwa wamechinja, zimwi likiwa mfano wa nyanya liliwaua vijana wawili na kuwarusha uchagani. Lilikuwa likimdanganya kila aliyetumwa kuleta moto na alipoingia kwa

nyumba ili apewe chakula na apae makaa, lilimongona na kumuua na kisha kumtupa uchagani ili mwingine akiingia asije akagundua.

Zimwi liliweza kuwaua vijana wawili isipokuwa mmoja Thome aliyeweza kukwepa mtego wa lile zimwi lililojibadilisha kuwa nyanya. Ni ukatili kumuua mtu aliyekwenda kutafuta msaada badala ya kumsaidia kama lilivyofanya zimwi. Thome alitambua hila za lile zimwi na akalipa uovu kwa uovu kwa kumkanyaga huyo nyanya mguu uliokuwa na kidonda na kisha kwenda zake.

Kando na mazimwi, wahusika kama wakweze na mkewe Thome waliokuwa katili kwa kitendo cha kutaka kumpa sumu ili wapate utajiri wake. Walijaribu mara kadhaa kumpa sumu kwa kutumia uji aliopolekewa. Alinusura kupitia kwa Ndama-mtu, aliyemwarifiwa kuhusu njama hiyo.

Thome aliwafanyia Ndugu zake kitendo cha ukatili alipobeba nzi kwenye ziaka ili wasile nyama. Uaminifu wao uliwafanya kuona njaa sana hivi kwamba walidhoofika kiafyakaribu washindwe kuendelea na safari yao. Thome alisababisha kuteseka kwao kwa muda kwa vile alijua kuwa wenzake hawangekula nyama kama walivyokuwa wameafikiana.

Ngano ya Mvulana na Zimwi inaonyesha maudhui ya ukatili ambapo zimwi lilimuua babake mvulana na ndugu zake wote na kunyakua mali yao yote. Haya ndiyo maudhui ambayo yanayojitokeza katika ngano zote kwa dhahiri zaidi.

4.2.1.2 Majuto

Majuto hutokea baada ya kufanya jambo ambalo linamfanya mhusika kusikitika kwa kuwa halikuwa sahihi. Wasichana katika ngano ya Zimwi na Msichana inaonyesha maudhui ya majuto kwa vile baada ya kukataa kufuata ushauri waliopewa na kuamua kufuata kijana wasiyemjua, baada ya kwenda naye waligundua kuwa lilikuwa ni zimwi. Walipofanya uamuzi huo walijua kuwa uamuzi wao ulikuwa kinyume na matarajio ya wengi. Walikuwa wanabahatisha na kuhatarisha maisha yao kwa sababu ya tamaa na mapuuzo ya kutotilia maanani ushauri.

Mumewe mama mjamzito alipopata taarifa kuhusu mateso mkewe aliyoyapitia kupitia kwa ndege, alionekana kuwa na majuto kwa kuwa alikuwa amemuacha mkewe kwa muda mrefu

bila kumshughulikia. Zimwi liliporejea kutoka kichakani, lilishuku ujasiri aliokuwa nao mama mjamzito na hata likamuuliza kama mumewe alikuwa amefika. Kwa sababu ya mapuuza, halikutafuta kwa makini ili kuhakikisha kuwa mwenye nyumba hakuwako. Lilipoanza kushambuliwa, lililia kwa majuto na kusema “ Si nilisema” kuoyesha kuwa lilijuta kwa kutomakinika.

Ngano ya Njiru inaangazia maudhui haya ambapo babake mvulana aliyechunga mbuzi aliyelitwa Njiru aliishi kupuuza yale aliyoambiwa kuhusu kuongea kwa mbuzi. Lau angalichukua hatua alipoarifiwa, janga la zimwi kumeza kijiji kizima halingetokea. Majuto hayo yalitokana na kupuuza mambo yaliyoonekana madogo lakini hatimaye yakaleta maafa makubwa sio tu kwa jamaa yake mbali kwa jamii nzima.

Wanakijiji katika ngano ya Vijana Watatu walijitia kitendo cha ukarimu wao wa kuwakaribisha wageni kama walivyomfanya Thome. Wote waliomkaribisha walihisirika kwa kupoteza mali yao kutokana na ujanja wake. Kilele cha yote, jamii yote ilipata hasara kubwa kwa kuwa walipokwenda kushukuriwa kwa wema wao, walikula nyama au wakasikia harufu ya nyama waliyolipia vikali wakidhani ni Mungu aliyekuwa akitoa hukumu kwa yeyote aliyehusika moja kwa moja au kwa mbali.

Maudhui haya yalijitokeza kwa wahusika kupuuza mambo fulani kama vile ushauri wa wazazi kwa watoto wao au kwa kutochukua hatua baada ya kupewa habari muhimu. Wahusika walipata funzo baada ya kuathirika na hivyo basi kuwa na majuto baadaye. Hali hiyo ilikwenda sambamba na methali isemayo majuto ni mjukuu huja baadaye.

4.2.1.3 Unafiki

Hii ni hali au tendo la kujifanya kuwa mkweli au kujifanya kuwa ni rafiki na hali ni adui. Maudhui haya yanayojitokeza katika ngano zilizoteuliwa kupitia kwa wahusika mazimwi na baadhi ya wahusika binadamu. Unafiki kwa pakubwa uaendelezwa na mazimwi bali hata kwa wahusika binadamu ambao wanajifanya wazuri lakini wanatenda kinyume na wanayosema. Mfano ni katika ngano ya Vijana Watatu ambapo mhusika Thome alibeba nzi katika podo yake huku akifahamu kuwa walikuwa wakienda kutafuta mahali kusikokuwa na nzi. Alijifanya kubaki nyuma ili ale nyama walizokuwa wamechinja ilhali wenzake walikuwa karibu kufa kwa njaa kwa kutokula nyama iliyokuwa na nzi kwa vile waliokuwa wameafikiana.

Mazimwi yalijifanya binadamu wema na hata kuwasaidia watu waliokuwa na shida ili kuwalaghai na kuwapata kwa ujanja ili wawaangamize. Suala hili linajitokeza katika ngano kama: Njiru, Mama na Zimwi na Mvulana na Zimwi. Zote zinayasawiri mazimwi kama wahusika wanafiki waliotoa msaada wao kwa binadamu kwa lengo la kuwafanya windo lao.

Mama aliyetaka kupewa moto bila kujua ni zimwi katika ngano ya Njiru, alijipata pabaya aliponyolewa kichwa huku akikatwa kichwa vipande na kuliwa. Mwanzoni hangeweza kutambua kuwa lilikuwa zimwi. Mama aliweza kugundua baadaye hakuwa akitakiwa mema na mama mwenzake aliyekuwa zimwi na akaanza kupanga mikakati ya kuliua zimwi hilo.

Unafiki unadhibika wazi katika hadithi ya Mama Aliyejifungua. Zimwi lilipata nafasi nzuri ya kumdhulumu mama alipohitaji mtu wa kumsaidia. Lilimsaidia wakati wa unyonge wake hata kama lilikuwa na mpango pamoja na wenzake kumla baada ya muda fulani. Msaada uliotolewa na zimwi ulikuwa si wa dhati mbali wa kinafiki. Kama wasemavyo akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki, urafiki wa zimwi na mama haukuwa wa dhati mbali wa zimwi kujifaidi mama alipoumia.

Mvulana alipotumwa na mamake kuuza ng'ombe wao wa pekee, zimwi lilimpunja na kumpa maharage kidogo. Mvulana alidhani zimwi lilikuwa likimsaidia bila kujua kuwa zimwi hilo lilikuwa likifurahi uhitaji wao na ndilo lilo hilo lililokuwa limenyakua na kujilimbikizia mali ya jamaa yao. Mkewe zimwi alikuwa mnafiki kwani alimdanganya kila zimwi liliposhuku jambo katika nyumba. Alitoa maelezo ya uongo na hata kumlamba kisogo mumewe. Aidha ndiye aliyetoboa siri kuhusu milki ya jamaa ya mvulana.

4.2.1.4 Utu

Maudhui ya utu yamejitokeza katika baadhi ya ngano. Maudhui haya yanaangazia hali ambapo wahusika wanadhihirisha matendo ya ubinadamu kama kuwa na huruma, ukarimu na kadhalika. Yanaendelezwa na wahusika kama ThuugiWaiya na Njaranga katika ngano ya Msichana na Zimwi waliokwenda kumuokoa msichana aliyekuwa katika hatari ya kuangamizwa na zimwi. Waliposikia sauti ya dadake Thuugi aliyetaka msaada hawakusita mbali walikimbia na kubeba silaha zao na kulishambulia zimwi na kumnusuru msichana.

Mkewe zimwi katika Mvulana na Zimwi alitenda kinyume na mazimwi mengi kwa kuonyesha utu. Kwanza alimkaribisha kwake bila kuwa na nia mbaya kama mazimwi mengine, alimficha mvulana ili asije akaliwa na mumewe au kudhuriwana mumewe na hata kumfichulia siri kuhusu asili yao. Huyu ndiye mhusika wa pekee zimwi aliyekuwa na utu. Hakutaka mvulana aangamizwe. Katika ngano iyi hiyo, Mama mzee aliyemwambia mvulana kuhusu mali yao na jamaa yao pia anaendeleza maudhui ya utu.

Mumewe Mama Aliyejifungua alipopashwa habari kuhusu zimwi lililomzalisha mkewe, alifanya kitendo cha utu kwa kuondoka mara moja bila kukawia kabla ya kudhuriwa na zimwi. Alipofika nyumbani kwake alimpata mkewe akiwa amedhoofika kwa njaa na jambo la kwanza alilofanya kama mtu mwenye utu ni kumshughulukia kwa kumpa chakula na baadaye akapanga vile angeliua zimwi.

Ngano ya Njiru inakuza maudhui haya pale ambapo watu walimkaribisha Thome na kumpa mahali pa kulala na hata mahitaji yake kama mgeni. Ukarimu wao ulionyesha jamii yao kuwa na utu. Vijana walipoua zimwi na kuikomboa jamii nzima, waliwatuza walioua zimwi na kuwapa zawadi mbalimbali. Watu wasiothamini mashujaa huwa hawana shukrani kwa mashujaa wa jamii zao.

4.2.1.5 Ujasiri

Maudhui haya yanahusu kufanya jambo bila kuogopwa. Kutokana na jinsi mazimwi yalivyosawiriwa kimaumbile, yanaonekana kuwa makubwa na sura za kutisha na uwezo wa kujibadilisha. Kukabiliana nayo kunahitaji ujasiri na werevu mwingi. Hadithi ya Njiru imewasawiri vijana waliokuwa mapacha kuwa wenye ujasiri kwa kuliua zimwi lililokuwa limewaua watu katika kijiji kizima pamoja na mifugo yao. Zimwi liliposikia sauti ya mama akiimba lilianza kujishaua vile lilivyomeza watu na mifugo.

Zimwi lilikuwa na nguvu za kuweza kuyang'oa maghala moja baada ya jingine kwa mikono. Vijana waliweza kuliua na liliposhindwa likaanza kukiri na kuwaeleza walikate vidole kimojakimoja ili watu waliomezwa waweze kutoka. Hatimaye watu wote walikombolewa na wakataka kujua waliowaokoa ili wawatuze kutokana na ujasiri wao.

Ngano ya Msichana na Zimwi inaonyesha vijana waliokuwa na ujasiri na wanakabiliana na adui yao vilivyo bila uwoga na kumuokoa dadake Thuugi aliyekuwa hatarini kwa

ushirikiano. Thuugi Waiya na Njaranga waliitikia mwito na wakapanga mpango na dada yao kwa wimbo. Matendo yao ni kielelezo cha matarajio ya jamii kwa vijana katika kulinda jamii zao. Walitimiza wajibu wao kwa ushirikiano na busara.

Mvulana pia alionyesha ujasiri katika ngano ya Mvulana na Zimwi. Aliupanda mti uliokuwa mrefu sana kwa ukakamavu mpaka akatokea katika nchi ngeni. Hakuogopa alipomuona jimama lililokuwa na sura ya kutisha. Ujasiri unazidi kuonekana alipochukua vitu mbalimbali na kisha kurudi kwa zimwi huku akijua hatari iliyomngoja. Ilitaka mtu mwenye ujasiri mkubwa kukubali kuwa na mpango na zimwi na kujificha ndani ya nyumba ya zimwi. Chochote kingeweza kutokea kwa vile mazimwi hayakuaminika.

Hatimaye Mvulana aliyekuwa mdogo aliweza kuliua zimwi kwa kushuka mbio na kuukata mti kabla ya zimwi kufika chini. Kitendo hiki kilifanya zimwi kukiri kuhusu umiliki wa mali haramu na mwishowe mama na mwanawe wakaweza kurejeshewa mali yao kwa sababu ya ujasiri wa mvulana kulikabili zimwi katili.

Mumewe mama aliyekuwa amejifungua alijificha uchagani akiwa na silaha zake baada ya kupanga na mkewe vile angefanya ili kulikasirisha. Zimwi lilipokuja na kufanya kama kawaida, mumewe alitokeza kutoka mafichoni na kuliua kabla halijamla mkewe likiwa na mazimwi mengine.

4.2.1.6 Vitisho

Vitisho ni maudhui mengine yanayojitokeza katika ngano hizi kutokana na: sura, umbo la mazimwi na mazingira ambamo mazimwi yanaishi. Fauka ya hayo, matendo yao ya kikatili yaliwati wanajamii uoga. Mazimwi yaliogopwa kwa kuwa na umbo kama:kuwa na vinywa viwili jicho utosini, maungo makubwa kuliko ya binadamu ya kawaida, uwezo wa kunusa na kujua alipo mtu na kadhalika.

Mfano unaodhibitisha kuwepo kwa maudhui haya ni katika ngano ya Msichana na Zimwi ambapo msichana mmoja aliweza kudhibitisha kuwa kijana waliyeandamana naye hakuwa mti mbali zimwi kwa kuona kinywa kilichokuwa kisogoni kila aliporuka na nywele kuondoka. Maumbile yale yalimfanya kutafuta njia ya kujinusuru na akarudi nyuma na kutoroka. Mwenzake aliyeendelea na safari alipofika nyumbani kwa zimwi, aliona kichwa

cha binadamu mvunguni mwa kitanda pamoja na mifupa ya watu walioliwa na zimwi. Taswira hiyo ya mafuvu ya vichwa vya watu na kinywa kisogoni yanatia hofu.

Mvulana mdogo alipopanda mti wa haragwe na kufika nchi ngeni, alishtuka kuona juso lililokuwa na sura mbaya la janajike lililotoka ndani ya nyumba ya zimwi. Tunaelezwa kuwa alikuwa na jicho utosini. Ukubwa wake pia ulitisha kwa vile hakuwa ameona mtu mwenye ukubwa kama ule hapo awali. Alijaribu kutoroka lakini likamkamata na kumwambia lingemfanya mtumishi wake.

Vitu vilivyokuwa katika nyumba ya zimwi vilitisha. kwa mfano, kuku aliyetaga mayai ya dhahabu, kinanda kilicholia kilipochukuliwa na mtu mwingine. Isitoshe, lilipolala lilikoroma kwa sauti ya kutisha.

Thome alitumia ujanja kuwatisha wanakijiji ili aweze kulipwa ng'ombe na mbuzi wengi. Wazee waliozikwa chini ya ardhi waliposema kuwa alipwe, watu wote walishtuka sana wakidhani ni Mungu aliyekuwa akunena. Walikubali kumlipa kwa mbuzi na ng'ombe bila hata kuuliza swali na wakakimbia nyumbani mwao ingawa waliona kuwa walidhulumiwa. Matumizi ya Mungu katika hadithi hii ilikusudiwa kutisha wanakijiji.

4.2.1.7 Ukombozi

Ngano za mazimwi zinaishia kwa furaha na matumaini. Hii ni kutokana na jamii kujinasua kutoka kwa minyororo ya mazimwi. Matumaini na maisha mapya yanaanza pale mazimwi yanashindwa kwa kutumia ujanja au kuyakabili moja kwa moja na kuyaua. Wanajamii wanaonekana kuishi maisha ya starehe bila kudhulumiwa tena na wahusika hawa katili.

Ngano ya Mvulana na zimwi ilileta ukombozi pale alipochukua hatua na kuamua kupigania haki yao. Waliishi katika hali ya umaskini hata wasiweze kupata chakula wakiwa na mama yake. Alipoliua zimwi, aliweza kupata mali yao yote na wakaishi raha mstarehe. Isipokuwa ni ukakamavu wa mvulana huyo, wangeishi kwa umaskini daima.

Ndugu mapacha katika ngano ya Njiru, walipambana na zimwi na kulishinda lililokuwa limemeza wanakijiji kizima pamoja na mali yao. Vijana hawa walitumiwa kuikomboa jamii yote hata wao wakaona ni vizuri kuwatuza kwa kazi yao nzuri. Licha ya kuweza kudhulumu watu wote, kuna mama mmoja mja mzito aliyebaki aliyetumiwa kuikomboa jamii yao.

Thome katika ngano ya Vijana Watatu alikabiliwa na changamoto ya kwanza alipoweza kuepuka mtego wa kuuawa kama ndugu zake wawili. Alilikanyaga zimwi mguuni na kutoroka lililokuwa mfano wa mama mzee. Nyanya huyo alikuwa amewaangamiza watu na kuwarusha uchagani. Ukombozi wa pili ulikuwa dhidi ya wakwe zake waliotaka kumpa sumu afe ili wapate mali yake. Ilibidi afanye uamuzi wa kuwamaliza wakwe zake ili aishi kwa amani. Alitafuta watu, wakazingira maadui zake na kuwaua wote.

Msichana aliyedangayika na kulifuata zimwi akidhani ni kijana ambaye angemuoa, alitanabahi akiwa mikononi mwa zimwi. Ilibidi awaze kwa haraka na asionyeshe dalili ya mshtuko ili zimwi lisikisie kuwa alikuwa na mpango wa kutoroka. Hii ilikuwa ndiyo hatua ya kwanza ya kujikomboa kisha ikafuatwa na hatua ya pili ambapo msichana alikimbia huku akiomba msaada kutoka kwa nduguye na marafiki. Nduguye na rafiki yake ndio walioleta ukombozi kwa kuliua zimwi na kumuokoa dadake.

Zimwi lilimkandamiza Mama Aliyejifungua kwa muda lakini mumewe alipopata ujumbe kupitia kwa ndege, alichukua hatua na kumuokoa kabla hajaliwa na mazimwi. Ngano hizi zote zinaishia kwa kuleta matumaini baada ya wahusika kudhulumiwa na mazimwi au kupambana na mazimwi na kuyashinda au kuyaua. Ushindi wa wadhulumiwa unaashiria ushindi wa jamii dhidi ya maovu. Dhuluma na unyanyasaji huweza kutawala kwa muda lakini haudumu.

Mtu yeyote Yule anaweza kutumiwa kuikomboa jamii bila kujali umri, hadhi au jinsia. Aidha ili ukombozi upatikane, lazima wanajamii wawe tayari kulipia gharama wala si lelemama. Kama ilivyo amani, ukombozi haupatikani kwa urahisi.

4.3 Uhakiki wa Wahusika wa Ngano za Mazimwi

Wahusika ni viumbe wa kazi ya kifasihi na hufanana na binadamu kwa kiasi fulani. Kulingana na Propp, (1968:79) wahusika huweza kuwa picha, taswira ama ishara za binadamu na pia ulimwengu halisi. Aidha huweza kutumika kiishara kuashiri kitu fulani. Kwa mfano, jembe kuashiria mkulima. Majukumu wapewayo huwa ni kipengele cha methodology ya kisemiotiki. Wahusika huwa ishara za akili za wanafasihi na hutumiwa kupitisha ujumbe fulani kwa kuashiria maana ya ziada.

Wahusika katika ngano hizi wamegawanywa katika makundi mawili makuu kwa msingi wa maadili; wema na wabaya. Wale wabaya wanaadhibiwa kwa kuishia kujuta au kuangamia mwishoni mwa ngano ilhali wale wazuri wakatuzwa na kuwa mashujaa wanaotambulika na kuheshimiwa na jamii husika.

Mazimwi huchukua nafasi kubwa na muhimu na ndio sababu ngano hizi zikaitwa ngano za mazimwi. Huwakilishabinadamu waovu au wabaya au viumbe vinavyofanya mabaya dhidi ya binadamu. Wahusika wote waovu hatima yao ni mauti au maangamizi na hawapewi nafasi ya kutamalaki na kuendelezwa uovu wao.

Wahusika mazimwi katika ngano hizi wamedhihirika katika hali mbalimbali. Mazimwi yana uwezo wa kujibadilisha kutoka hali moja hadi nyingine. Katika ngano ya Zimwi na Msichana, wamesawiriwa kama vijana watanashati wenye usiri. Hali hii inawafanya wasichana kudanganyika kwa urahisi. Baada ya kufaulu kuwaghilibu wasichana wanabadili sura zao na tabia zao na kutaka kuwala. Nandwa na Bukenya (1983) wanasema kuwa tabia ya kubadilikabadilika ilitumiwa na wanajamii kuwatahadharisha walengwa dhidi ya kuwaamini wageni au watu wa jamii zingine.

Ngano za Mama Aliyefungua, Mvulana na Zimwi na Njiru zinasawiri mazimwi kama viumbe katili wanaowanyanyasa binadamu. Ukatili wao unaonekana pale ambapo yanaua watu wengi na kuwameza na kuchukua mali yao bila huruma. Sifa hii imejitokeza katika ngano ya Mvulana na Zimwi na ya Njiru. Tunapata kuona kwamba baada ya zimwi kuuawa watu wengi wanatoka tumboni mwa zimwi.

Mazimwi husawiriwa kama viumbe walioishi miongoni mwa watu kama Bukenya (1991) wanavyosema huku wengine wakiishi mapangoni kama inavyodhihirika katika ngano ya Njiru na Vijana Watatu waliokuwa wamejificha pangoni na wakapatwa huko na zimwi. Mazimwi yaliishi mbali na watu ili yasiweze kujulikana mienendo yao. Hadithi ya Mvulana na zimwi, hapana mahali maalumu ambapo tunaweza kuonyesha kwa kuwa Mvulana alipanda mti uliokuwa mrefu sana na hatimaye kujipata katika nchi ngeni kulikojaa mali nyingi.

Mtagusano wa mazimwi na watu huwa mwema lakini kwa muda tu yakiwa na nia ya kuwahadaa ili watekeleze maovu yao. Baadaye uhusiano huu hubadilika punde tu

wanapofanikiwa kuwanasa binadamu. Wanaolengwa zaidi ni wasichana, watoto na akina mama ambao huwa wepesi wa kushawishika. Ni wahusika wanafiki na wasiri kwa vile hawajulikani mapema wanapoingiliana na binadamu wa kawaida. Tunaona yakiwa na midomo miwili lakini ule wa nyuma ulifichwa sana ili usionekane ila ulionekana zimwi lilipokuwa likimeza nzi. Hali hii ilitokana na tabia yao ya kuwa na usiri mwingi.

Mazimwi yanadhihirisha sifa ya upumbavu kwa kudanganyika kwa haraka na kutochunguza kwa undani. Katika ngano ya Mvulana na Zimwi, linapouliza kama kulikuwa na binadamu katika nyumba, liliambiwa ni harufu ya mbuzi na kuku na likaridhika bila kuchunguza zaidi. Mwangi (1970) katika kutoa sita za mazimwi anaseema kuwa yanadhihirisha upumbavu kwa kiasi kikubwa. Mfano wanachota maji kwa vyombo vilivyotoboka au vyenye matundu. Jina hili ni la kimajazi kwa kuwa mazimwi yanasawiriwa yakiwa makubwa lakini yanayodanganyika kwa urahisi.

Aidha mazimwi yana uwezo mkubwa wa kunusa na kupata harufu hasa ya binadamu. Sifa hii inaonekana vyema katika ngano nyingi za maziwi kwa mfano katika ngano ya Mvulana na Zimwi, lilipoingia nyumbani lilitambua kuwa kulikuwa na binadamu katika ile nyumba. Mkewe zimwi aliposema ni nyama ya mbuzi aliyopikiwa liliridhika kwa haraka bila hata kufanya uchunguzi. Inadhihirika kuwa mazimwi yanashawishika kwa urahisi na kwa hivyo ni mapumbavu kama jina linavyoonyesha.

Mazimwi katika ngano za jamii yamedhihirika kuwa na sifa zinazokiuka uhalisia. Mazimwi yamesawiriwa kuwa na uwezo wa kujigeuza kutoka kwa mnyama hadi kwa binadamu. Mengine hata yana uwezo wa kufanya miujiza kama inavyodhihirika katika hadithi ya Mvulana na Zimwi. Lilikuwa na kuku aliyetaga mayai ya dhahabu na gitaa iliyoweza kuongea kama binadamu. Isitoshe, mbegu zake zilikuwa kwa usiku mmoja na kuwa mti mrefu ajabu ambapo kilele chake kilikuwa nchi nyingine.

Njiru alikuwa mbuzi aliyeweza kujigeuza na kuwa zimwi na hata kuongea na kijana aliyemchunga na hata kumeza watu kijiji kizima. Mazimwi pia yanasawiriwa kama wahusika walio na uwezo wa kujifanya warembo kama inavyoonekana katika ngano ya Msichana na Zimwi ambapo zimwi lilibadilisha kuwa kijana mtanashati aliyewavutia wasichana. Pia liliweza kuwa na sura mbaya au wakongwe kama katika ngano ya Vijana Watatu wapokuta zimwi likiwa mfano wa nyanya..

Hii ni kuwasawiri wahusika na ambayo huwapa sifa za kimaumbile zisizokuwa za kawaida. Kwa mfano, kuwa na jicho kubwa kupindukia, pua ndefu, miguu au sehemu za mwili zenye maumbile yasiyokuwa ya kawaida. Wamitila, (2010:466-8). Anawaita wahusika wa aina hii kerekecha ambao hutumiwa kuzumgumzia uovu, hila, ubaya au uozo ulio katika jamii husika.

Katika ngano ya Mvulana na Zimwi na Njiru na Mvulana yamesawiriwa kuwa na sura ya kutisha na kuogofya. Njiru alikuwa mbuzi aliyekua kwa haraka kuliko mbuzi wengine wa kawaida na isitoshe alikuwa na upembe mmoja kichwani. Taswira ya Njiru ni ya kutisha na isiyo ya mbuzi wa kawaida kwa kuwa alikuwa zimwi lililowameza watu kijiji kizima.

Wahusika hawa wameonyeshwa kuwa wa jinsia zote mbili ya kike na ya kiume. Mazimwi mengi ni ya kiume kuonyesha kuwa wengi wanaodhulumu na walio na uwezo ni wanaume ikilinganishwa na wanawake. Ngano ya Njiru na mvulana, Mvulana na Zimwi na ya Vijana Watatu kuna mazimwi ya kike ilhali katika ngano mbili zinazobaki ni ya kiume yenye sifa hasi. Wahusika wa kiume ndio wamedhibiti wanawake na kuendeleza maovu dhidi ya binadamu wenzao.

Ngano ya Mvulana na Zimwi ilionyesha tofauti ndogo na ngano zingine kwa kuonyesha mkewe zimwi akiwa na wema kwa kumficha mvulana asiliwe na mumewe na kumwambia siri kuhusu familia yao na mali ya jamaa zake. Kwa kiasi kikubwa, mazimwi ya jinsia ya kiume ndiyo yanayoonekana kuwa katili na kuendelezwa matendo hasi katika jamii.

Kwa kijumla wahusika mazimwi wamesawiriwa wakiwa katili, wanafiki, walafi, wabinafsi na wenye tamaa, wapumbavu, wasirinawaovu wanaoendeleza uovu katika jamii. Hatima yao ni maangamizi na kuondolewa katika jamii. Wanawakilisha watu waovu katika jamii ambao hawapewi nafasi na wanaishia kushindwa na kuondolewa na jamii. Hatima ya mazimwi inaonyesha vile maovu yanashindwa na wema katika jamii.

Aghalabu mazimwi yalishindwa na kuuawa na watu waliotumia ujanja na ambao walikuwa wadogo au wasiokuwa na uwezo na nguvu nyingi kama mazimwi. Wahusika wadogo wanawakilisha watu wema na wanaotenda yanayotakikana na jamii. Wanawaangamiza wanaotenda maovu kwa kuyaua mazimwi. Hawa ni wahusika nguli ambao wanatenda kadri

ya matakwa ya jamii wanaotumiwa kupigana na wahusika hasidi wanaowakilishwa na mazimwi.

Kando na mazimwi, kuna wahusika wengine ambao ni binadamu, ndege, mbuzi na ng'ombe waliotumika katika ngano zilizoteuliwa. Katika ngano ya Mama Aliyejifungua, ndege anamasaidia binadamu kwa kuwapasha habari muhimu na kuepusha maangamizi. Si wanyama wote waliotumika kwa manufaa ya binadamu. Katika ngano ya Njiru, zimwi lilikuwa limejigeuza kuwa mbuzi na katika hali hiyo liliweza kuwala watu. Ndama alitumika kama mwokozi wa mhusika mkuu dhidi ya hila na njama za mkewe aliyetaka kumwangamiza ili achukue mali yake.

Kuwepo kwa wahusika wa aina mbalimbali ni sifa mojawapo ya ngano za fasihi simulizi. Ngano hizi zimetumia wahusika mazimwi, wanyama kama ndama, mbuzi, ndege na binadamu. Mazimwi yamechukua nafasi kubwa na kuwa wahusika wakuu pamoja na binadamu na wakati mwingine watu wakichukua nafasi ya wahusika wadogo. Binadamu wanawakilisha maadili mema huku mazimwi yakichukua nafasi ya uovu.

Ngano za mazimwi ni muhimu hasa kwa watu walio na tatizo la kukabiliana na maovu ua mazingaombwe. Mazimwi au majitu, mizimu na mashetani ya kila aina kila mara huashiria uovu na ukatili. Ngano hizi husawiri mazimwi kuwa ya jinsia ya kike au ya kiume. Yanapokuwa ya kike, hidhihirika kama wasichana warembo. kwa mfano, katika jamii ya Waluhya wakati mwingine huwasawiri mazimwi kama wasichana au wanawake warembo ambao huwahadaa wanaume. Ngano hizi zilitumiwa kuwaonya watu dhidi ya kuwahukumu wengine kwa jinsi wanavyoonekana kwa nje kwa mfano kwa sababu ya urembo. Ngano hizi zilitumiwa kuwaonya watu dhidi ya kuwahukumu wengine kwa jinsi wanavyoonekana kwa nje kwa mfano kwa sababu ya urembo. Aghalabu hujitokeza kama ya kiume yanayo watisha wasichana msituni wanapochuma matunda mwituni au kutafuta kuni. Wao hutumia ujanja au miujiza ili kuwakamata.

Licha ya wao kuwa wajanja, katika ngano zingine huchorwa kama wahusika wapumbavu wanaodanganyika kwa urahisi. Kwa mfano kuna mama aliyewapikia mazimwi panya badala ya wanawe wa kiume wawili katika ngano za Gĩkũryũ. Wana maumbile ya kutisha ingawa wanasifika kwa kujigeuza na kuchukua maumbo tofauti ya vitu kama: visiki, mawe, ndege au

vitu vinginevyo wanavyochagua. Ngano za Gĩkũyũ zinawasawiri wakiwa na midomo miwili; mmoja mbele na mwingine nyuma. Kwa Wakamba na Wabaluhya, wanaaminika kutoa moto kutoka kinywani. Kwingineko wanaaminika kuwa na mkia na wenye uwezo wa kusababisha kiangazi na njaa na majanga haya yanapotokea hudai kafara ya binadamu ili kuondoa hali hiyo.

Mazimwi katika jamii zingine hurejelea watu wasiojulikana au watu waliokuwa wa jamii tofauti. Zilitumiwa kuwatahadharisha wasichana na watoto dhidi ya kuwa na uhusiano na wageni. Wageni walijumuisha hata majirani ambao hawakuwajua. Kwa jamii ya Waluhya mazimwi yalitumiwa kurejelea wanaume waliofaa kuogopwa na wanawake na hata kuwaambaa kutokana na tabia zao zisizopendeza.

Ngano hizi zilikuwa na maana fiche kwa kuwa mazimwi yalionyeshwa kama yaliyoweza kuoia na kupata watoto lakini maswali tunayopaswa kujiuliza ni je, mazimwi ni watu? Kama ni watu ni, watu wa aina gani? Wanaweza kuwa wanawakilisha binadamu waovu katika jamii? Mazimwi wanaweza kuashiria mauti kwa kuwa wanaweza kumeza kijiji kizima lakini hatimaye wakashindwa na mpiganaji mchanga ambaye huwakomboa wote. Kupitia kwao binadamu huonekana kucheza na mauti. Kifo kila mara kilidai kafara ya binadamu hususan msichana mrembo kama inavyodhihirika katika hadithi ya Wacici. Ngano nyingi za mazimwi zilikuwa na miishio mizuri ambayo ilileta utulivu wa kisaikolojia.

4.4 Msuko

Njogu na Chimera (1999) wanasema kuwa msuko ni mtiririko au mfululizo wa matukio yanayojenga hadithi na namna matukio hayo yanavyosababishana. Njogu na mwenzake wanaendelea kueleza kuwa msuko unaweza kuelezwa kama mtiririko wa vitendo na namna vitendo hivyo vinavyozuana. Msuko wa ngano zilizoteuliwa ni sahili ambapo matukio yamepangwa katika uhusiano wa kiusababishi na kiwakati. Matukio yanachangia katika muwala na mtiririko wa ploti na usimulizi kwa jumla.

Msuko huu sahili unajitokeza katika ngano zote zilizoteuliwa. Wahusika mazimwi wanaonekana kuwa kama binadamu wa kawaida mwanzoni. wanatangamana na kuingiliana vyema na wanajamii lakini kadri muda unavyopita, wahusika hawa huanza kudhihirisha na kuonyesha hulka zao halisi. Matukio yamefuatana na yanaendelea kujenga matukio mengine

hatua baada ya hatua mpaka kilele cha hadithi kinafikiwa ambapo mazimwi yanajulikana kuwa ni mazimwi wala si binadamu wa kawaida.

Migogoro inazuka pale ambapo mazimwi yanaanza kutenda matendo ya kikatili na katika harakati za kupambana na binadamu. Katika kujikomboa na kupambana na maovu, wahusika binadamu wanazua mbinu mbalimbali za kuwaua mazimwi kwa kutumia nguvu au ujanja. Upeo wa ngano unafikiwa pale zimwi linauawa na jamii kupata amani au kurejeshewa mali na watu wao walioangamizwa.

Kuna migogoro kati ya wahusika mbalimbali na pia katika akili ya mhusika au wa kimawazo ambapo mhusika ana mivutano ya ndani kwa ndani. Mgogoro wa aina ya pili unaonekana katika ngano kama vile ya Msichana na Zimwi pale ambapo msichana aliamua kutofuata ushauri wa wasichana wengine licha ya kuonywa. Wamitila (2002:12) anasema mgogoro huu unatokana na mtazamo alionao kuyahusu maisha. Huishia kwa kitendo chake cha kujiua. Katika hadithi hii msichana anaishia kuhatarisha maisha yake na kunusurika kifo.

Katika hadithi ya Zimwi na Msichana, mazimwi yalijumuika na vijana wa kike na wa kiume katika densi. Ngoma iliwafanya wasichana kutangamana na wavulana na shughuli hiyo ikawafanya wasichana kushawishika kufuata wavulana waliokuwa mazimwi kwa kuwa walijidai na hawanbetambulika kwa urahisi. Baadaye wanatambua kuwa ni zimwi na mmoja anarudi na mwenzake anaanza kutafuta njia ya kujiokoa na hatimaye anafanikiwa kutoroka. Mgogoro unaibuliwa ambapo wasichana wanajaribu kujinusuru kutoka kwa zimwi kwa njia ya ujanja.

Mkondo wa ngano unabadilika na mapambano yanaanza kati ya binadamu na mazimwi. Uadui unaanza kudhihirika badala ya urafiki, chuki nayo inachukua nafasi ya mapenzi. Binadamu anaishia kuibuka kuwa mshindi baada ya mapambano hayo kwa kuwa anatumia ujanja na msaada wa wenzake kuliua zimwi. Binadamu anaathirika kutokana na hayo lakini anajifunza funzo fulani hasa kwa kupuuza ushauri au kwa kutokuwa makini katika masuala ya maisha. Ngano zote zinaishia kwa matumaini na furaha baada ya mazimwi kuangamizwa.

Matukio katikahadithi yameibua migogoro mbalimbali kutokana na mambo wanayoyapitia wahusika kama: tamaa, wema dhidi ya uovu, kujikomboa n.k. kama katika ngano ya Msichana na Zimwi aliyetaka kuolewa, ya Vijana Watatu ambapo Thome alitaka

kujifaidikwa kula nyamahuku wenzake wakiumia. Migogoro mingine inatokana na shida wahusika wanazozipitia wakitafuta afueni kama inavyodhihirika katika ngano ya Mvulana na Zimwi ambapo umaskini wao na mamake unamfanya kubadilisha ng'ombe wao wa pekee na maharagwe machache ili wapate chakula. Mvulana anapotambua kuwa mali iliyokuwa na zimwi ilikuwa yao katika ngano hii ya Njiru, wanaanza harakati za kupigania haki yao.

Msuko wa ngano umekuwa muhimu katika kuibua maudhui na mbinu mbalimbali kama taharuki, sadfa n.k. Kwa mfano tunataka kujua hatima ya hawa wasichana wawili baada ya kugundua kuwa walifanya uamuzi mbaya, watakavyojiokoa kutoka kwa zimwi. Katika ngano hizi zilizoteuliwa, msuko umeibua taharuki ambayo inatufanya kufuatilia hadi mwisho. waliongeza kuwa ishara na sitiari hutumika kama vifaa vya kumfikirisha mtu. waliongeza kuwa ishara na sitiari hutumika kama vifaa vya kumfikirisha mtu. Aidha msuko umekuza wahusika katika ngano na kusaidia katika kuwasawiri na kufichua sifazile zilizofichika hasa za mazimwi kwa kuwa mwanzoni mwa ngano mazimwi yanajidai kuwa binadamu wazuri. Mwanzoni mwa ngano zote mazimwi huwa na hulka mzuri na tabia zao zinadhihirika kadri wakati unavyopita kutokana na mtukio yanavyozidi kukuzwa. Mtindo wa ngano unafanana jinsi matukio yanakuzwa na kufanikisha kutoa funzo kwa wanajamii.

Mwisho wa ngano zote unaishia kwa furaha ambapo mazimwi yanauawa na kurejesha mali na watu walioangamizwa mfano katika ngano ya Njiru na Mvulana na Zimwi. Wahusika ambao ni wadogo kwa umri wanaliua zimwi na kuikomboa jamii nzima au mali ya jamii zao. Ngano ya vijana watatu pia inaishia kwa furaha baada ya zimwi kuuawa na kuondoa maadui waliowasumbua.

Ngano zote zinafuata fomula fulani inayofuata hatua kadhaa kabla ya kufikia kilele chake binadamu anaposhinda mazimwi yanayowakilisha maovu. Hatua ya kwanza ni pale ambapo mazimwi yanajificha yasijulikane yakiwa miongoni mwa binadamu na kufanya matendo mema ili yapate nafasi ya kuwanasa. Hapa mazimwi yanatangamana vyema na binadamu na kufanya matendo mema. Yamesawiriwa kuwa na nafasi bora zaidi kuliko binadamu kwa upande wa umbo, hali ya kiuchumi na kijamii.

Hatua ya pili ni pale ambapo watu wanaingia katika mtego wa mazimwi wa kutaka msaada kutoka kwao au kujipata katika hali au mahali ambapo mazimwi yana nafasi nzuri ya kuwaangamiza watu kutokana na makosa waliyoyatenda ya kupuuza, kukaidi au

kudanganyika. Katika ngano ya Njiru, babake alipoambiwa kuhusu mbuzi aliyekuwa akiongea alipopelekwa malishoni, alipuzilia madai hayo na hatimaye huyo mbuzi akaishia kuwa zimwi lililowameza watu kijijini na kuleta maangamizi.

Hatua ya tatu inayojitokeza katika msuko wa ngano za mazimwi ni ile inayoonyesha harakati za kupambana na ukatili au dhuluma dhidi ya mazimwi. Wahusika au wanajamii wanaungana kupambana na mazimwi ili kukomboa jamii zao au watu wanaohusiana nao. Wasichana, watoto na akina mama ndio walioathirika pakubwa kwa kushawishika kwa urahisi. Mazimwi yanaishia kushindwa katika mapambano hayo kwa kuuawa. Kifo chao kinaashiria mwanzo wa jamii mpya. Hii ndiyo sababu ngano hizi huishia kwa furaha kama anavyosema Mwangi (1970).

Usahiliwa ngano hizi hizifanya kuwa rahisi kufuatika kwa vile matukio huwa hayana utata. Elegwa (1996), anasema Wepesi huu hufanikisha kipengele cha kupitisha ujumbe kwa wanaokusudiwa hasa watoto na vijana walioelekea kubaleghe. Aidha huleta burudani kwa kuzifanya zivutie zinaposimuliwa. Hadhira inayolengwa na ngano ndiyo huzifanya kuwa sahili.

Wanyama na ndegemara nyingi huja kuauni wahusika walio katika hatari au shida. Mfano katika ngano ya Mama Aliyejifungua na Zimwi ambapo ndege alitumwa na Mungu kumjulisha mumewe kuwa mkewe alizalishwa na zimwi na alikuwa akiteswa kwa kunyimwa chakula.

Kama ngano nyingine za fasihi simulizi, ngano hizi zinatumia nyimbo kwa sababu mbalimbali kama vile: kuburudishakutokana na kubadilisha mtindo mmoja kwa kipindi kirefu, kama kiliwazo katika hadithi ya kitanzia, kupitisha habari muhimu kwa hadhira na kuficha ujumbe huo maadui ambao kwa muktadha huu ni mazimwi. Mfano ni katika hadithi ya Mama Aliyejifungua na Zimwi, Msichana na Zimwi na Njiru. Katika ngano ya Msichana na Zimwi, zimwi lilitumia wimbo kutoa vitisho kwa msichana na pia msichana aliyetaka kuliwa na zimwi alitumia wimbo kuomba msaada kutoka kwa nduguye na rafikiye.

Kwa jumla ngano hizi zimetumia msuko sahili unaofuatika kwa urahisi na kibua taharuki inayomfanya msikilizaji kutaka kujua yatakayofuata na kuzua maudhui mbalimbali yanayofungamana moja kwa moja na mahitaji ya jamii. Maudhui mengi yanalenga kukuza

maadili katika jamii kulingana na mila na desturi kama vile: utiifu, uvumilivu, ushirikiano, kutoshawishika kwa urahisi na pia kukashifu maovu kama tamaa, ukatili, uzandiki n.k.

4.4 Usimulizi

Usimulizi wa matukio katika ngano za mazimwi umefanywa kwa nafsi zote tatu. Yaani, nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu kulingana na ngano. Nafsi ya kwanza imetumia kiwakilishi nafsi huru 'mimi' au kiambata 'ni'. Mfano katika ngano ya Msichana na Zimwi, msichana mmoja aliyeamua kuolewa na kijana ambaye hakunjua alimwambia mwenzake kuwa ni lazima angekwenda na mvulana aliyemvutia katika densi. Alikuwa akimwambia mwenzake kwa nafsi ya kwanza akimweleza aliyokuwa ameamua. Mazungumzo ya wasichana hao wawili yalifanywa kwa nafsi ya kwanza.

Aidha zimwi lilijibizana na msichana kwa kutumia nafsi ya kwanza. Msichana aliposema kuwa alitaka kwenda haja, zimwi lilimwambia kuwa huko hakuna mtu aliyekubaliwa kutoka nje. Msichana naye alimjibu kuwa wao hawaruhusiwi kwenda haja ndani ya nyumba. Mazungumzo haya yote yalifanyika kwa nafsi ya kwanza wingi na umoja.

Msimulizi pia anatumia nafsi ya tatu inayotumia kiwakilishi 'a' na 'yeye' ambapo anasimulia yaliyofuata baada ya wasichana kumfuata kijana aliyekuwa zimwi baada ya densi. Mazungumzo kati ya wasichana wawili waliofuata zimwi bila kujua yalikuwa katika nafsi ya kwanza na ya pili inayotumia kiwakilishi cha nafsi 'u' au 'wewe'. Aidha katika ngano ya Mama Aliyejifungua na Zimwi, imetumia tumia nafsi zote tatu kwa kuwa wahusika wote wanawasiliana wao kwa wao lakini katika matukio tofauti.

Usimulizi wa nafsi ya tatu huwa na matumizi ya 'a' na 'yeye' katika viwakilishi vya nafsi. Ni mtindo ambao hupendelewa sana na wasomi. Hadithi huelezea matukio yanayohusu mtu mwingine. Msimulizi huwa nje ya hadithi akisimulia juu ya mhusika fulani. Wellek na Warren (1949) wanasema kuwa katika tenzi, mtunzi husimulia kisa kama msimulizi wa nafsi ya tatu. Wakati mwingine huwapa nafasi wahusika wake kuzungumza moja kwa moja.

Matumizi ya nafsi zote tatu zimetumika katika ngano zilizoteuliwa ingawa nafsi ya tatu imetumika sana. Pia kipengele cha toni hudhihirika katika usimulizi msanii atakaowasilisha.

Katika ngano teule za Gikūyū tulizohakiki mtunzi ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu na amefaulu sana katika matumizi ya mbinu hii.

4.5 MTINDO

4.5.1 Ishara za Mazimwi

Aguilar, J. (2008) katika makala kuhusu 'Ishara katika Fasihi', akieleza maana ya ishara, anatoa mifano ya ishara kwa kuonyesha hali mbalimbali kama: Kifo cha mume aliyemdhulumu na kumdhibiti mke wakehuwa ni ishara ya uhuru kwa mke. Mke hupata uhuruwa kufanya atakacho baada ya kuishi maisha ya dhiki aliyokuswa na mumewe. Ndoa huchukuliwa kama kuwa katika kifungo cha maisha kwa kuwa mke huwa hana hiari ya kufanya atakacho.

Ingawa kuna ishara za kibia na zisizo za kibia, ishara huweza kuwa na uashiriaji wingi au wingi maana wa ishara au neno fulani, unaotokana na fasiri tofautitofauti za wasomaji ambazo zinakubalika kwa sababu, kama asemavyo Iser katika Maclean(1986: 122) "Hakuna fasiri mbaya katika kazi ya kifasihi."Kulingana na Chandler, ishara huchukua muundo wa maneno, picha, sauti, harufu, ladha, vitendo au vitu halisi. Anaongeza kuwa kitu chochote hakiwezi kuwa ishara kama hakitafasiriwa kama ishara.

Mfanomwingine nikifo kwa mtu anayeteseka sana labda kwa ugonjwa suguhuwa ni ishara ya faraja. Kuna jamii ambazo humlambisha mtoto anapozaliwa asali na shubiri kama ishara ya yale mtoto huyo anatarajia kukumbana nayo maishani. Asali huwa inaashiria mema ulimwenguni ilhali shubiri ambayo ni kali sana huashiriwa mabaya atakayokumbana nayo maishani. Kwa kawaida kifo huogopwa sana lakini inapotokea kuwa mtu anapitia hali ngumu sana ya maisha, wengi wao hutamauka na kuona kifo kama suluhisho la matatizo yao. Kifo huchukuliwa kama pumziko la mateso ya ulimwengu.

Hali nyingine ni uwepo wa baba kwa mtoto anayeogopa ni ishara ya ulinzi. Mtoto akiwa na babake huwa hana woga hata kama babake hana silaha zozote yeye huamini kuwa ana uwezo mkubwa wa kukabiliana na adui au hali zote. Wamitila (2003) anaeleza ishara kama kitu fulani katika kazi ya fasihi ambacho huwakilisha kingine kutokana na uhusiano uliopo

kati ya vitu hivyo viwili au uwezo wake wa kuibua fikira fulani katika akili ya msomaji au msikilizaji.

Kuna 'ishara bia' na 'ishara zisizo bia'. Ishara bia huweza kutambuliwa na watu wengine popote pale walipo. Kwa mfano, mto kutumika kama ishara ya kuonyesha mpito wa maisha. Mazimwikatika ngano za mazimwi ni wahusika waliopewa nafasi kubwa na muhimu. Kwanza, mazimwi yanapatikana katika ngano za jamii nyingi duniani na pia nyingi ya sifa za mazimwi zinashabihiana katika jamii tofauti licha ya kuwa katika mazingira tofauti.

Kama asemavyo Wamitila (2003), nadharia ya Umuundo huweka mkazo mkubwa kwenye unasibishi wa maana. Maana nasibishi ya neno ni maana inayohusishwa na neno hilo wala sio kile kinachorejelewa. Neno 'jogoo' kwa mfano lina maana husishi, kuku wa kiume anayewika. Maana yake nasibishi ni mwanamume anayependa wanawake sana.

Wanaumuundoleo wanaieleza hali ya ishara moja kuwa na maana nyingi kwa kuiweka au kuikita maana kwenye muktadha wa jamii. Kutokana na maelezo haya, ni muhimu kuchunguza ishara mbalimbali zinazojitokeza katika ngano za mazimwi katika jamii tofauti. Waasisi wa nadharia ya Umuundoleo wanadahili kuwa ishara haziwi na maana ya ndani bali huipata maana yake kupitia kwa lugha inayohusika. Mazimwi huwakilisha dhana mbalimbali kulingana na msuko wa ngano na usawiri wa wahusika.

Kilanga (2015) akimnukuu (Hawkes 1977) anasema, iwapo msomaji atalielewa neno katika kazi ya kifasihi itamlazimu kuliangalia katika muktadha fulani. Kwa mfano, moshi ni ishara ya kiwakati inayoashiria kuwepo kwa moto. Ishara za kitaashira nazo, huwa ni tukio la kiutamaduni. Huwa hazina mfanano wa uhusiano kati ya ishara na kiashiriwa bali huwa jambo au kitu cha makubaliano au kikanuni. Kwa mfano, njiwa kutumika kuashiria amani. Ngano mbalimbali hutoa ishara tofauti tofauti kulingana na maudhui na dhamira inayokusudiwa na jamii husika. Kwa mujibu wa ngano zilizoteuliwa, ishara zifuatazo zimeweza kudhihirika:

4.5.1.1 Tishio

Kulingana na Kamusi Kuu ya Kiswahili, tishio ni jambo au kitu kinachomtia mtu hofu ya kutokuwa salama katika maisha yake au kushindwakutekeleza jambo fulani. Kwa mujibu wa sifa za ngano zilizoteuliwa, mazimwi yanajitokeza kama taashira ya mambo mbalimbali katika jamii. Mazimwiiyamesawiriwa wakiwa na maumbile mbalimbali wakati mwingine kama ya binadamu wa kawaida napiawahusika hawa wamesawiriwa wakiwa na maumbile ya kutisha. Mfano wamesawiriwa na midomo miwili, umbo kubwa na uwezo wa kufanya miujiza kama inavyodhihirika katika ngano ya Mvulana na Zimwi.

Masimulizi ya ngano za mazimwi yaliibua hisia za kuogofya. Zilibua hofu na hali ya kutisha hususan kwa watoto navijanawaliolengwa na jamii kupata ujumbe. Wahusika wanaonekana kuogopa kukutana na mazimwi. Mvulana alipopanda mti uliokuwa mrefu na kujipata katika nchi nyingine, alipobisha na kuona janajike lililokuwa na sura mbaya alianza kutoroka lakini akakamatwa. Tukio hilo linaibua hisia na taswira ya kitisho.

Wanawake na watoto ndio walioathirika pakubwa kama inavyodhihirika katika ngano nyingi. Ziliwatisha ili kuwafanya watahadhari kabla ya kuolewa au kuwaamini watu wasiowajua. Katika ngano ya Zimwi na Msichana mmoja wao alionekana kuvutiwa na mwanamume baada ya densi lakini akaonekana kuogopa kwenda naye. Uamuzi wa kwenda na kijana asiyemjua ulitokana na tamaa na ukaidi kwa vile alionekana kuwa na ati ati alipokuwa akifanya uamuzi wa mwisho kwa sababu alijua ilikuwa ni kinyume cha matakwa ya jamii yao.

Msichana alipofika ndani ya nyumba, aliona mafuvu ya watu mvunguni mwa kitanda hali ambayo inaibua hisia za hofu. Aidha katika ngano ya Njiru, mbuzi alikuwa na upembe mmoja kichwani na aliongea kama binadamu. Zimwi liliweza kumeza watu katika kijiji kizima pamoja na mifugo yao.

Ishara ya kutisha inajitokeza kutokana na mazingira yanayosawiriwa katika ngano. Ndungo na Wafula, (n.d) wanasema kuwa tungo za fasihi simulizi hutegemea muktadha wa mazingira na zimejikita katika utamaduni wa jamii zinamoibuka. Jamii kwa mfano inapodhamiria kutoa picha ya kuogofya huchora mazingira yanayoogofya. Imewezakutumia mazingira ya misitu

na wahusika kama vile majitu ili kuleta dhana ya hofu na vitisho. Ngano ya Njiru inatokea katika mazingira ya msituni na mapangoni ambayo ni ya kutisha.

Ngano hizi zinatoa dhana ya kutisha kila mazimwi yanapotajwa na kuelezwa na zilitumiwa kufanikisha matakwa ya jamii ya kushauri, kukanya au kuonya na kadhalika. Toni ya nyimbo zinaposimuliwa huimbwa kwa sauti ya kitetemeshi na sauti nzito. Sifa hii inadhihirika vyema ngano inaposimuliwa bali si katika maandishi. Maandishi yanadhihirisha toni ya kutisha kutokana na maneno yanayosemwa na mazimwi mfano “ Nitakukata ng’we! ng’we!” katika ngano ya Zimwi na Msichana.

Vifaa vinavyotumiwa na mazimwi ni vikubwa na vya kutisha. Mfano k tunaona zimwi likiwa na jisu lililjulikana kama “Kienji” lililorushwa na kufyeka sehemu kubwa lilipokuwa likimfuata msichana aliyetoroka. Ukubwa na ukali wa ala hizi pia unachangia katika kuendeleza ishara ya kutisha.

Taswira ya nyumbani kwa mazimwi inaogofya na kutia hofu kwa vile mafuvu na mifupa ya binadamu walioliwa inaonekana ikifichwa ili windo lisione na kutoroka. Mwangi (1970), anasema mazimwi yalikuwa na uchu wa kula binadamu. Ngano hizi zinaposimuliwa zinaibua hisia za kutisha na hivyo kuwa chombo cha jamii kupitisha mafunzo na maadili ya jamii.

4.5.1.2 Ukatili

Ukatili ni hali ya kutokuwa na huruma na upendo, uonevu au udhalimu. Zimwi linapotajwa, wazo la kiumbe au kutokuwa na huruma hujengeka akilini. Kutokana na masimulizi mbalimbali yanayorejelea viumbe hawa, matendo yao mengi maovu katika jamii yanafanya watu kuyamasibisha na ukatili. Ngano za mazimwi ziliyasawiri yakiwa katili na yasiyo na huruma. Mazimwi yalitumia fursa na uwezo wao kuwadhulumu binadamu waliotangamana nao wakitaka msaada wao au hata bila kutaka msaada.

Mazimwi yameumbwa yakiwa na umbo la kutisha na yanayotumia uwezo na nafasi zao kutekeleza maovu dhidi ya binadamu. Katika ngano ya ‘Mama Aliyejifungua na Zimwi’, tunaona zimwi likienda kuishi kwa mama mja mzito na kumnyanyasa kwa kumpa chakula kidogo punde tu baada ya kujifungua. Huku likingoja kumla na kusherehekea na wenzake.

Mazimwi wakati mwingine huwa na sifa chanya kama anavyosema Wamitila (2010) yanaposaidia anayeteseka. Mwanzoni zimwi lilionyesha huruma kwa kutomla Mama Aliyejifungua na kuamua kumshughulikia mpaka akajifungua. Msaada huu ulikuwa wa kinafiki kwa vile ulikuwa kwa manufaa ya zimwi na wenzake. Chakula anachopewa mama kinafaa kulipiwa ghali na mama baada ya muda fulani kama yalivyopanga.

Kitendo cha kumsaidia mama mja mzito alipokuwa na hajana kumpangia mabaya ni kitendo kinachoenda kinyume na matarajio ya jamii na ubinadamu. Mtu yeyote yule anatarajiwa kutoa msaada bila hata kuulizwa aonapo mtu mwenye haja. Fauka ya hayo, zimwi linapomsaidia kwa kumpa chakula, linakula chakula kile cha Mama Aliyejifunguana kumfanya adhoofike kiafya. Zimwi lilifurahia upweke na unyonge wake wakati alihitaji msaada zaidi.

Zimwi linawakilisha watu dhalimu wanaofurahia unyonge wa wenzao kuwakandamiza. Mwangi (1970), anakubaliana na hayaanaposema kuwa, ngano hizi zinahusu watu ambapo mazimwi yanasawiriwa kama viumbe viovu,visivyo na huruma na vyenye kuzua fujo.Swala hili linadhibitishwa na ngano mbalimbali za mazimwi. Kawaida jamii hasa iliyoendelea huwasaidia wanyonge au wanaokandamizwa kama vile:watoto, kina mama, walemavu namaskini.

Mama aliyetaka moto alinyolewa huku akikatwa vipande vya nyama kichwani hadi akabaki fuvu kabla ya kupewa moto. Ingawa kuna matumizi ya chuku, tukio hili linadhihirisha ukatili kwa vile twajua rafiki wa dhati ni yule ambaye humfaa mtu wakati wa dhiki. Aidha katika ngano ya Mvulana na Zimwi, tukio hilo linaoneka likitokea zimwi linampa mvulana maharagwe kidogo wabadilishane na ng'ombe wa mama maskini. Umaskini wa mama huyu ulikuwa umetokana na kunyang'anywa mali yao na zimwi lilo hilo.

Ukatili wa mazimwi sio tu kwao tu bali hata kwa mazimwi yale mengine ambapo mazimwi yenye nguvu yanayala yale yasiyo na nguvu. Katika jamii iliyo na utu, wanajamii huwalinda, huwajali na kupanga mikakati ya kuhakikisha wasio na uwezo wanaishi kama waliobahatika. Jamii ya mwenye nguvu mpishe au mnyonge msonge ni ya kikatili kwa vile wanyonge hudhulumiwa na wenye nguvu na uwezo. Ukatili huendeleza dhana ya mnyonge msonge lakini jamii zilizostaarabika huwadhamini wanyonge kama kina mama, watoto na walemavu.

Wema au msaada unaotolewa na mazimwi huwa si kwa nia ya kusaidia bali huwa ni chambo cha kuwapata na kuwaangamiza. Mazimwi hufurahia shida na mateso ya watu au wenzao wakati wa shida. Katika baadhi ya ngano, mazimwi yanaonekana kudhulumu mazimwi mengine yasiyo na uwezo au kuchangia kukandamiza wenzao. Ngano ya mvulana inatufunza kuwa unafiki wa wenzetu huweza kusababisha madhara kwa wenzetu. Mkewe zimwi ndiye aliyechangia katika kifo cha mumewe labda kutokana na kutofurahia matendo yake ya kikatili.

Kilichofanya mazimwi kuogopwa ni kutokana na ukatili wao. Watu walihofia kupatana na mazimwi kwa kuwa yalijulikana kwa unyama waliokuwa nao yaliyoenda sambamba namaumbile yao. Katika jamii ya Gikūyū, mazimwi yalionyeshwa kama yaliyokuwa na vinywa viwili kama vile katika ngano ya Msichana na Zimwi. Wanajamii wanayasawiri mazimwi yakiwa ya kutisha ili kuwafanya watu kuyaambaa na kudharau maovu wanayowakilisha. Hivyo mazimwi ni ishara ya ukatili katika jamii hii.

4.5.1.3 Kifo / Mauti

Mazimwi yaliashiria mauti kwa sababu kila ngano ya mazimwi iliishia kwa mauti. Mhusika aliyejipata mikononi mwa mazimwi ilibidi atumie ujanja wake kujiokoa lau sivyo angeliwa na nayo. Zimwilingeweza kumla mtu mmoja au likameza kijiji kizima au familia nzima. Katika ngano ya Mvulana na Zimwi, zimwi lilikuwa limemeza jamaa zake isipokuwa yeye na mamake waliokuwa wamekwenda ugenini. Mvulana alijawa na huzuni alipowaza kuhusu ndugu na babake waliomezwa na zimwi.

Mkewe zimwi alimficha mvulana na kulidanganya zimwi kuwa harufu aliyoisikia haikuwa ya binadamu. Hii ni kwa kuwa zimwi lilisema kuwa lilitaka kumla mtu akiwa hai au akiwa maiti. Yeyote aliyejipata mikononi mwa mazimwi alitafakari kuhusu kifo. Mfano ni katika ngano ya Mama Aliyefungua aliyekuwa akisubiri kuliwa siku moja. Alikuwa akisubiri kifo kwa vile hangetoroka na mumewe alikuwa hana habari kuhusu yaliyokuwa yakiendelea. Uwepo wa zimwi uliashiria mauti kwa wahusika.

Vijana wawili walipoliua zimwi lililokuwa limewameza watu wote na mali yao, watu walitoka ndani ya viungo vya mwili wake kama ishara ya kufufuka baada ya kufa. Hali hii inaonekana pia katika ngano ya Zimwi na Mvulana. Hakuna uhusiano wowote kati ya binadamu na zimwi ulioishia kuleta mema mbali ulileta Mauti.

Wahusika waliodanganyika na kufuata au kuingia mtegoni mwa mazimwi waliishia kuliwa kama hawakupata mtu wa kuwaauni. Ndugu zake wawili Thome walidanganywa na zimwi lililokuwa limejifanya mama mzee na wakaishia kuuawa na kurushwa uchagani. Mambo yalikuwa mawili mtu alipojipata mikononi mwa zimwi: auawe na zimwi au zimwi liuawe ili aweze kuokolewa.

Kwa mujibu wa maelezo haya, inadhihirika kuwa zimwi liliashiria mauti popote lilipotokea. Kifo ni adui mkubwa wa binadamu na binadamu hujaribu juu chini kupambana nacho kama anavyopigana na mazimwi katika ngano hizi. Hata leo neno zimwi linapotumika huleta maana ya jambo linaloleta maafa au maangamizi.

4.5.1.4 Tamaa

Tamaa ni hamu au uchu mkubwa wa kupata kitu. Mazimwi yamesawiriwa kama wahusika walio na tamaa kubwa kupitia kwa ngano za mazimwi zilizoteuliwa. Mfano katika ngano ya Mama Aliyejifungua, zimwi lilikuwa na tamaa kubwa ya chakula na kumla kama mama kama windo lake. Halikusubirimama aweze kupata nguvu baada ya kujifungua ili apate hamu ya kula. Lilibugia chakula chote na kumuacha mama akiwa mnyonge sana. Sababu ya kutomla akiwa mja mzito ilikuwa labda kumfanya anenepe ili waweze kumfanya kitoweo kizuri. Tamaa ilifanya zimwi kukosa subira.

Tamaa inayafanya mazimwi kumeza kijiji kizima au familiayote. Katika ngano hizi, mazimwi hayakushiba na yalikuwa na uchu wa kula watu, kuchukua mali yao na hata kula mazimwi mengine. Ngano ya Njiru inaonyesha zimwi likijitapa kwa kuweza kula watu wote pamoja na mifugo wao. Kama ingalikuwa kwa sababu ya kushiba, halingekuwa limemeza kijiji chote. Yalisawiriwa kama yasiyotosheka mbali yalitaka zaidi.

Katika ngano ya Vijana Watatu, zimwi lililokuwa katika mfanowa mwanamke mkongwe aliwauavijana wawili na lilikuwa katika harakati ya kuua kijana wa tatu. Halikutosheka kama vile mazimwi mengine yalionekana kutotosheka na kula watu. Pia tamaa ya mali ya wakwe wa Thome ulifanya watake kumuua ili wabaki na mali yake. Tamaa ilileta Mauti kwa mkewe Thome na jamaa yake na hivyo kuafikiana na msemu usemao tamaa mbele mauti nyuma.

Kuyasawiri mazimwi yakiwa na vinywa viwili ni ishara ya umero na tamaa iliyowafanya kutoridhika na kile walichostahili. Mwanasanaa husisitiza kile ambacho huona muhimu na kinachowasilisha ujumbe kwa urahisi. Aidha uwezo wa kunusa na kupata harufu ya watu kama inavyoonekana katika ngano ya Mvulana na zimwi inatilia mkazo tabia ya ulafi na tamaa.

Leo hii watu wanaoonekana walafi hulinganishwa na fisi au nguruwe katika mazungumzo, michoro na hata ngano za kiistiari. Mazimwi yalikula hata wasichana waliowapenda na kuvutiwa nao ambao walikusudia kuwa wake zao. Hii ni kuonyesha kuwa tamaa inaweza kudhuru hata wale watu wa karibu sio tu wa mbali.

4.5.1.5 Janga / Baa

Janga ni tukio la hatari ambalo husababisha maafa kama vile kupotea kwa maisha au mali. Katika ngano zote za mazimwi, uwepo wa mazimwi ulikuwa ni mwanzo wa mikosi na nuksi katika jami hiyo. Maisha na hata mali yao yalikuwa hatarini na ilibidi waishi kwa tahadhari na wasiwasi wasije wakajipata katika taabu.

Wanajamii waliungana ili kukabiliana na mazimwi na kuwaonya wale wadogo kama watoto na wasichana waliotarajia kuolewa wasije wakajipata katika mikono ya mazimwi. Ngano ya Msichana na Zimwi ilionyesha msichana aliyekaidi ushauri anajipata katika hatari. Masaibu yake yanakuwa ni shida ya kila mtu wanapojaribu kumuokoa kutoka kwa zimwi lililotaka kumwangamiza.

Ngano ya Njiru alipojulikana kuwa ni zimwi, aliwaangamiza watu katika kijiji kizima na kuleta maafa akianza na mchungaji. Kumuweka nyumbani kulisababisha dhiki kubwa kwa jamii. Babake kijana mchungaji alifaa kuchukua hatua kabla ya janga kutokea kama wahenga walivyosema: tahadhari kabla ya hatari. Zimwi hilo kwa mfano wa mbuzi ndilo lilikuwa hatari. Zimwi katika jamii liliashiria baa au dhiki wakati wowote.

4.5.2 Tamathali za Usemi

4.5.2.1 Misemo

Misemo maneno au fungu la maneno lililo na maana fiche. Hutumia mmaneno ya kawaida kwanjia isiyokuwa ya kawaidana huhitaji mtu kufikiria kwanza ili afichue maana ya maneno husika. Misemo hubuniwa na jamii na hutofautiana na jamii nyingine kwa sababu hutungwa

kutokana na mazingira pamoja na itikadi za jamii inayohusika. Misemo hutumika kwa lengo la kuficha maana, kueleza ujumbe kwa njia rahisi au kufanya lugha ivutie.

Wamitila (2003), anaeleza kuwa semi ni neno lenye upana ambalo hutumiwa kuelezea matamko fulani yanayoelezea ukweli fulani. Aidha, semi nikauli za maneno kadha yenye maana iliyofichika. Katika ngano zilizoteuliwa kutoka kwa jamii ya Gĩkũyũ, misemo imetumika katika ngano hizokuelezea hali fulani zinazowakumba wahusika. Misemo hii ni:

Gikũyũ	Tafsiri ya Kiswahili
(i) <i>Marũturi-inĩ mokĩte-</i>	Waliokwenda uhunzi wamerejea
(ii) <i>Kũhaata mahĩndĩ-</i>	Kufagia mifupa.
(iii) <i>Gũtheca njira</i>	- kuchoma njia (kushika njia)
(iv) <i>Gũkaua kĩenji</i>	- kubeba 'kienji' (jisu kubwa)
(v) <i>Akĩnyita njĩra</i>	- kushika njia

Msemo huu ulitumika katika ngano ya Mama Aliyejifungua, msemo: '*Marũturi -inĩ mokĩte*' umetumiwa. (kama waliokwenda uhunzi wamerejea). Msemohuu hutumiwa kumwambia mtu mwoga na mnyenyekevu na mara moja akaonyesha ujasiri ambao si tabia yake. Watu wanapoona mtu amenza kudhihirisha tabia ngeni ambayo si kawaida yake huuulizwa kwa msemo huu. Ulitokana na ngano hii ya mazimwi ambapo baada ya mama kujifungua na mumewe kupashwa habari na ndege, alirejea nyumbani kwake na kujificha na silaha zake. Alimwambia mkewe alijibu zimwi kwa ufidhuli ili litakapotaka kumla aliue. Huu msemo ulitokana na zimwi liliposhuku tabia za yule mama kwa kuwa lilimjua kuwa mnyenyekevu na mwoga.

Msemo huu ni maarufu hadi leo ukitumiwa kwa muktadha kama ule wa zimwi. Mtu anayejulikana kuwa asiye na uwezo akionyesha ukakamavu na ujasiri ambao anafahamika kutokuwa nao tunastahili kuchunguza kwa sababu kila jambo hufanyika likiwa na sababu. Unatahadharisha watu kutopuuzwa watu walio dhaifu unapowaona wakionyesha ujasiri kwa vile huweza kuwa wana mtu anayewasaidi ama hawako tena katika hali yao ya zamani.

Msemo mwingine uliotumika na bado watumika hadi leo unatokana na ngano ya Msichana na Zimwi. Msemo huu ni *Kũhaata mahĩndĩ* uliotokananakile kisa cha msichana kwenda na

zimwi mpaka wakafika nyumbani. Kabla ya zimwi kuingia ndani ya nyumba, likaharakisha ili kuiondoa mifupa ya binadamu iliyokuwa nyumbani ili yule msichana aliyekuwa mgeni wake asije akajua kuwa lilikuwa zimwi na lilikula watu.

Msemu huu hutumika hadi leo. Hutumika pale mtu anapotaka kujitayarisha na kunadhifisha makazi yake ili mgeni wake asije akaona mambo ambayo yangemwaibisha. Mgeni hafai kujua siri za nyumbani au akaona mambo ambayo huweza kuleta aibu kwa mwenyeji. Pia msemu huu hutumika kuwashauri watu umuhimu wa kujiandaa kwa ajili ya wageni wasije wakarudi kwao na kupeleka sifa mbaya.

Katika ngano ya Njiru kuna matumizi ya misemo ‘*Gũtheca njira*’ na *Akũnyita njũraukirejelea* vile kijana alivyokuwa akitoka sehemu moja hadi nyingine. Misemo hii unaonyesha vile alivyotembea kwa miguu kwa muda. Msemu hii huifanya ngano kueleweka vyema na kuchora taswira ya safari. Aidha huifanya ngano ivutie na isiwe chapwa.

Msemu mwingine uliotumika katika ngano zilizoteuliwa ni: ‘*Gũkuuakienji*’. Asiliyamsemu huu ni ngano za mazimwi. Iliaminika kuwa mazimwi yalikuwa na ala hii ambayo iliaminika kuwa ilipotupwa ingefyeka sehemu kubwa. Hii ndiyo silaha ambayo zimwi lilichukua ili kumtafuta msichana aliyekuwa ametoroka lakini halikufanikiwa kumpata. Msemu huu hutumika mtu anapobeba jisu kubwa kuliko inavyotarajiwa kufanyia kazi fulani.

4.5.2.2 Tashibihi

Tashibihi ni mbinu ya mlinganisho wa vitu viwili au zaidi vyenye hulka tofauti kama vile sitiari. Hata hivyo tofauti na sitiari, tashibihi hutumia viungo vya ulinganishaji. Msokile (1992) anafafanua kuwa aina hii ya tamathali hutumia ulinganisho wa mambo ama vitu kwa kutumia viunganishi ‘ja’, ‘mithili ya’, ‘mfano wa’, ‘sawa na’ na ‘kama’. Mtunzi hutumia ulinganishi huu kusisitiza sifa fulani na pia kujenga picha ya aina fulani akilini ambayo athari yake ni ya kudumuzaidi. Zimetumiwa ili kusisitiza sifa fulani na pia kujenga picha ya kitufulani akilini katika ngano. Katika lugha ya Gĩkũyũ neno ‘ta’ humaanisha kama katika Kiswahili.

Mfano katika ngano ni kama :

Gĩkũyũ

Tafsiri ya Kiswahili

- (i) *Ta marũturi-inũ mokũte*– Kama waliokuwa uhunzi wamerejea.
- (ii) *Mwana no ta ũria ũngi* –Mtoto ni kama yule mwingine

- (iii) *Marimũ mahaana ta andũ* – Mazimwi yalikuwa yanafanana na binadamu
- (iv) *R̄kinye mūt~in~ ta ur̄a* – Lifike kwenye mti kama ule

Katikangano ya Mama Aliyefungua na Zimwi, zimwi lilitumia tashbihi ‘*Ta mar̄ūturi-in̄ mok̄te*’. Ilitumiwana zimwi likimwambia mama liliposikia jinsihuyo mama alikuwa na ukakamavu usiokuwa wa kawaida. Lilifananisha ujasiri wa mama hiyo na ule wa mtu aliyejua kuwa ana msaidizi. Zimwi lilijua kuwa wanawake waliokuwa na waume zao karibu hawangetishwa na yeyote. Uwepo wa mume uliwakilisha ulinzi. Mazimwi yalikuwa na tabia ya kuwashambulia wanawake na watoto hasa waliokuwa peke yao.

Asili ya msemo huu ni kisa hicho katika hadithi ya Mama na Zimwi. Hutumiwa kurejelea watu wanaobadilika na kuwa wakakamavu ilhali awali walijulikana kuwa waoga. Pia huambiwa watu wanasikika kuongea kwa ufidhuli bila kujali matokeo ya matamshi yao kana kwamba wanafanya hivyo ili kuchochea fujo.

Tashibihi nyingine iko katika ngano ya Vijana Watatu na Zimwi ambayo ilitumiwa na zimwi lililokuwa mfano wa mwanamke mkongwe. *Mwana no ta ũria ũngitashibihi* hiiilitumiwa ilikuwaambia vijana aliokuwa wamekwenda kuomba moto kwa zimwi na kuwaonyesha kuwa watoto wote walikuwa sawa. Kwa kulinganisha kila kijana na mtoto wake lilitaka vijana wasishuku kuwa lilikuwa na nia mbaya ili wakubali kuingia ndani ya nyumba aweze kuwafumania na kuwaua bila waokutarajia.

Katika ngano ya Msichana na Zimwi, msimulizialitumia tashibihi hiyo kutoa maelezo ya jinsi zimwi lilikuwa. Hii ni mojawapo wa sifa za mazimwi katika baadhi ya ngano ambapo mazimwi yalijifanya binadamu wa kawaida ili kuwalaghai watu kwa urahisi nakisha kuwala. Vijana hao waliishia kudanganyika na kuingia mtegoni mwa zimwi na wawili wakauawa. Kijana wa tatu Thome hakudanganyika na ndiye tu alinusurika.

Katika ngano ya Msichana na Zimwi, tashibihi ‘*R̄kinye mūt~in~ ta ur̄a*’ imetumiwa na msimulizi wa ngano kulinganisha umbali. Msimulizi aliitumia kuonyesha kuwa palikuwa Mahali ambapo si mbali wala karibu lakini ni umbali ambao ungemwezesha msichana kutoroka na zimwi lisiweze kumfikia. Pia ilikuwa ni njia mojawapo wa kuwashirikisha hadhira katika usimulizi.

Mwanzoni mwa hadithi, msimulizi alieleza sifa za mazimwi na kuzilinganisha na binadamu wa kawaida. Tashbihi ‘*Marimū mahaana ta andū*’ inalinganisha mazimwi na watu kama vile: kuoja, kuimba na kufanya matendo yote binadamu anaweza kuyatendo. Katika ngano za mazimwi, kuna sifa nyingi zinazoshabihiana na watu katika jamii ya Gĩkũyũ.

4.5.2.3 Tanakali za Sauti

Kimani na Chimera (1999) wanasema kuwa hiki ni kipengele cha fani ambacho kinatumika katika ngano ili kuzua taswira za mambo yanayosimuliwa akilini mwa msikilizaji. Pia huwapa makini wasikilizaji ili wahisi kuwa wamo ndani sio nje ya kisa kinachosimuliwa. Zinaiga milio, kueleza hali mambo yanatendwa na pia kutilia mkazo. Tanakali zilizotumika katika ngano zilizoteuliwa ni kama:

Gĩkũyũ

Tafsiri ya Kiswahili

- (i) *Irimū rĩgũka kaba! kaba! kaba! rĩteng’erete-* Zimwi likakimbia kaba! kaba! kaba!
- (ii) *Ngũgũtinia ng’we ng’we!*- Nitakukata ng’we! ng’we !
- (iii) *Gĩtinũke ng’wee* - Likatike ng’wee!
- (iv) *Akĩnyita njĩra kaba! kaba! kaba!* - Akashika njia kaba! kaba! kaba!
- (v) *Rĩkĩrũ ũta ka!* - Likafumwa mshale ka!
- (vi) *Akĩoya magũrũ o kuku kuku!* - Akachukua miguu kuku!kuku!
- (vii) *Ĩkĩmanina othe bũrũ!* - Akawamaliza wote buru!

Tanakali za sauti zinajitokeza katika ngano kwa wingi kwa kuwa kila ngano imezitumia kwa wingi. Mfano katika ngano ya Zimwi na Msichana, kuna Tanakali kama: ‘*Rĩgũka kaba! kaba! kaba!*’, ‘*Ngũgũtinia ng’we ng’we!*’, ‘*Gĩtinũke ng’wee!*’ Tanakali zinaigiza jinsi matendo yanatendwa kama jinsi ya kutembea kama kimbua kaba! kaba! kaba!, sauti ya matendo kama kukata ng’we! ng’we!, kuonyesha jinsi titi lingekatika Ng’wee!

Katika ngano ya Mama na Zimwi, Tanakaliya sauti ‘*Rĩkĩrũ ũta ka!*’ inaiga sauti jinsi Zimwi lilifumwa mshale na mwenye nyumba. Kuna tanakali ambazo zinatilia mkazo mfano, zimwi lilikula watu likamaliza ‘*Ĩkĩmanina othe bũrũ!*’, ‘*Akĩoya magũrũ o kuku kuku!*’ Katika ngano ya Njiru. Sauti hizi zinatoa uhalisia wa matendo na pia kuibua hisia zinazokusudiwa na msimulizi. Tanakali hizi za sauti pia zinachangia kwa kiasi kikubwa kuchora taswira mbalimbali zinazofanikisha usimulizi wa ngano za mazimwi.

4.5.2.4 Taswira

Taswira ni picha ambazo humjia msikilizaji akilini anapoisoma au kusikiliza kazi fulani ya kifasihi. Picha hizi hujengwa kwa maelezo fulani. Aidha hujengwa kwa matumizi ya tamathali za usemi kama tashibihi, chuku, tanakali za sauti, sitiari n.k. Sababu moja ya kutumia taswira ni kumfanya msomaji aelewe vile mtu au kitu kinavyoonekana. Taswira hujengeka kutokana na matumizi ya lugha ya msimulizi anapoeleza matukio.

Mazimwi yalivyosawiriwa katika ngano hizi yanaibua taswira akilini mwa hadhira. Mfano katika upande wa maumbile. Ngano ya Kijana na zimwi inatuonyesha zimwi likiwa na sura ya kuogofya. Lina jicho usoni, kimo kinene, vifaa vya kiajabu kama kinanda kinachozungumza, kuku atagaye mayai ya dhahabu n.k. zimetumia taswira sana kuanzia kwa sifa za mazimwi, taswira ya mti wa haragwe uliokuwa mkubwa kupita kiasi inajitokeza pia katika ngano hii.

Ngano ya Njiru na Zimwi imesheheni taswira mbalimbali kuanzia mwanzo hadi mwisho. Mfano ni mbuzi aliyekuwa na upembe mmoja utosini na aliyekuwa akiongea na mvulana aliyekuwa akimchunga, Njiru anapogeuka na kuwa zimwi linalowameza watu kijiji kizima na kisha linapouawa linawatoa wote liliowameza. Taswira ya mama aliyenyolewa na kutolewa ngozi kichwani pia inajitokeza kiasi cha kuweza kutambuliwa na wanajamii waliokuwa wamemezwa na zimwi.

Mama Aliyejifungua alikuwa amedhoofika kiafya kwa pakubwa katika ngano ya 'Mama Aliyejifungua na Zimwi'. Kuna pia taswira ya zimwi likija na kujishasha kama kawaida yake na pia likiuawa na mumewe mama aliyedhulumiwa kwa kufumwa mikuki na kukatwakatwa kwa panga.

Tanakali za sauti zilizotumiwa pia zimechangia kwa pakubwa kuibua taswira kwa kuwa tunapata kuona jinsi zimwi lilikimbia, kufumwa mishale, lilivyowabwia watu katika kijiji bila kusaza mtu. Kando na picha za mawazoni, zimetumiwa kuendelezwa taharuki katika ngano hizi kwa kumfanya hadhira kutaka kujua yatakayojiri baada ya matukio yaliyojitokeza. Mfano katika ngano ya Njiru, mama analiwa kwa kubambuliwa ngozi ya kichwa na hadhira

angetaka kujua jinsi wanawe wangelichukulia swala hilo, kama wangelipisha kisasina kama wanajamii wangemtambua baada ya kuokoa jamii nzima.

Taswira pia inaendelezwa na tashibihi ambazo zinalinganisha sifa za viti viwili. Ulinganisho huo unaibua taswira akilini mwa hadhira ili maana kamili ya kile kinalinganishwa kijitokeze. Mfano katika ngano ya Msichana na Zimwi ambapo msimulizi anasema kuwa mazimwi yanafanana na binadamu. Picha inayojitokeza akilini ni jinsi zimwi linafanana na binadamu kwa kuwa katika ngano zingine mazimwi yanasawiriwa kama viumbe wa ajabu.

Aidha Tanakali hizi za sauti zinasaidia kujenga tasira mbalimbali kama vile: taswira za mwendo zinazolenga hali ya kutembea au safari *'Ak~nyita nj~ra kaba! kaba! kaba!'* kama alivyofanya muwe mama alipopata habari kuhusu kujifungua kwa mkewe na uwepo wa zimwi.

Kuna taswira za usikivu ambazo huunda picha zinazolenga hisia ya kusikia, yaani picha zinazohusiana na sauti. Kwa mfano, zimwi lilipokuwa likiimba vile lingemkata titi ng'we! ng'we! kwa sauti nzito. Zimwi lilikuwa likijitapa vile lilivyokula watu pamoja na mifugo wao kwa wimbo na kisha kusema kuwa ni nzi aliyemsakama kooni. Maumbile ya mazimwi kama kuwa na vinywa viwili, mbuzi kuwa na upembe mmoja kichwani, mti wa haragwe kuwa mkubwa sana mpaka ukatokea katika chi ya kigeni, janajike kuwa na sura mbaya iliyitisha na kadhalika yanaimbua taswira muono katika akili ya msikilizaji au hadhira.

4.5.2.5 Tashihisi

Wales (2001) anafasili tashihisi kuwa; 'Ni tamathali ya usemi ambapo kitu kisicho na uhai, mnyama, kisicho binadamu au chenye sifa zakidhahania kinapewa sifa za binadamu.' Tamathali hii hutumiwa kuleta mvuto wa kisanaa na athari fulani za kihisia. Katika ngano ya Mvulana na Zimwi, kinanda kinapochukuliwa na mvulana akitaka kukiiba kinapofika mlangoni kinaanza kuliana kuzungunza kama binadamu. Mbinu hii ilitumiwa kuonyesha jinsi zimwi lilikuwa na uwezo uliozidi wa binadamu. Inaonyesha dhana ya ukiamabile katika ngano za mazimwi.

Ngano ya Njiru, mbuzi aliyejulikana kama Njiru alikuwa akiongea na mvulana aliyekuwa akimchungu na kisha akammeza. Baadaye alitorokea msituni na kisha kumeza kijiji kizima

akiwa zimwi. Tukio hili linaonyesha kuwa zimwi linaweza kuwa katika umbo lolote sio tu binadamu kama ngano ya zimwi na msichana.

Ngano ya Vijana Watatu imetumia ndama kama mhusika ambapo ndama aliyejulikana kama “Gacau Mündü” alikuwa akimwarifu Thome kuhusu njama ya kutiliwa sumu kwenye chakula ili afe. Zaidi ya hayo, ndama huyu alikuwa akimwambia Thome jinsi angefanya ili aweze kupata siri zao na pia vile angeangusha uji uliokuwa umetiwa sumu.

Kama katika ngano ya Mama aliyejufungua, wahusika ndege na ndama ni wahusika chanya wanaotenda mema ili kuwaokoa binadamu waliokuwa katika hatari ya kuangamizwa na zimwi. Mhunzi aliarifiwa na ndege ambaye alikuwa mhusika katika ngano ya ‘Mama Aliyejifungua na Zimwi’. Mbinu hii imetumika pamoja na mbinu zingine kama nyimbo na takriri ambapo wahusika wanaimba wimbo kwa kurudiarudia ili kuwasilisha ujumbe. Ndege alitumia wimbo kumpasha habari kuwa mkewe alikuwa amejifungua na alikuwa akidhulumiwa na zimwi na ilimlazimu aharakishe kabla ya mkewe kuliwa na zimwi.

Ngano zilizoteuliwa zimedhihirisha matumizi ya wahusika wa kila aina kama vile: ala ya mziki, wanyama na ndege. Wametumiwa kwa njia mbalimbali kama inavyoonekana katika matendo yao. Aidha tanakali za sauti zinasaidia kujenga taswira mbalimbali kama vile: taswira za mwendo zinazolenga hali ya kutembea au safari mfano, ‘*Ak~nyita nj~ra kaba! kaba! kaba!*’ kama alivyofanya muwe mama alipopata habari kuhusu kujifungua kwa mkewe na uwepo wa zimwi.

Kuna taswira za usikivu ambazo huunda picha zinazolenga hisia ya kusikia. Taswira hii inahusiana na sauti kama inavyosikika. Kwa mfano, zimwi lilipokuwa likiimba vile lingemkata titi ng’we! ng’we! Taswira ya sauti nzito na ya kutisha inajengeka akilini mwa msikilizaji au anayesimuliwa ngano ya mazimwi.

4.5.2.6 Chuku

Chuku ni mbinu inayotumika kueleza hali ya kukipa kitu, mtu au hali sifa kupita kiasi. Matumizi ya mbinu hii hudhamiriwa kusesitiza sifa. Kauli zinazotumika katika mbinu hii huwa ni za kutiliwa chumvi ili kusesitiza na pia kuchekesha. Kwa kutumia chuku, sifa za kawaida za kitu kinachohusika hukiukwa. Kitu hicho huweza kudunishwa au kukuzwa. Matendo mengi katika ngano za mazimwi zilizoteuliwa yamekiuka hali ya kawaida.

Katika ngano ya Njiru, tabia za mbuzi za kukaidi mambo aliyostahili kufanya kama mnyama mfanokutoroka nyumbani na kwenda kuishi mwituni kimepigwa chuku. Njiru anaonyeshwa kuwameza watu wa kijiji kizima bila kushiba. Ulafi wa mazimwi chuku katika ngano ya Njiru, na ile ya Mvulana na Zimwi. Zimwi halishibi kula watu na hata baada ya kuwala, hawafi. Kitendo hiki kinatumiwa kuonyesha ukatili wa mazimwi na hivyo kuibua hofu kwa wanajamii.umepigwa

Mazimwi hatimaye wanauawa na wahusika dhaifu ambao hawana weledi wa vita kama inavyotokea katika ngano ya Mvulana na Zimwi. Ujasiri wa mvulana kwenda kwa zimwi na kurejea hata baada ya kuponea chupuchupu ni kitendo kilichopigwa chuku. Anahatarisha maisha yake mara kadhaa anapofukuzwa na zimwi na kulihepa. Kijana analikwepa zimwi kwa njia rahisi sana jambo ambalo si la kawaida.

Kisa cha mama aliyekwenda kuomba moto kwa zimwi na akaambiwa ni lazima angenyolewa kwanza kimetiwa chumvi. Mama alinyolewa huku akikatwa vipande vya kichwa na vikaliwa na zimwi. Mama alinyolewa bila kulalamika mpaka akabaki fuvu kichwani. Ni vigumu kubambuliwa kichwa mpaka ukabaki fuvu bila kufa.

Upumbavu wa mazimwi pia umepigwa chuku katika baadhi ya ngano ambapo zimwi linashindwa ujanja hata na watoto. Ngano ya Msichana na Zimwi inaonyesha zimwi likiwa pumbavu kwa mfano, linamfunga msichana kamba kiunoni na kumwambia atoke nje bila kuandamana naye. Lilipouliza alipokuwa amefika, liliridhika na kusubiri huku msichana akiendelea kukimbia. Ukweli ni kwamba sauti ya mtu aliyekwenda mbali huweza kujulikana kwa urahisi na kwa hivyo tungetarajia zimwi litambue hivyo na kutoka punde tu sauti ilipokuwa ikisikika kwenda mbali.

Mapuuza ya mazimwi katika baadhi ya ngano yamepigwa chuku. Kwa mfano katika ngano ya Mvulana na Zimwi, zimwi lilikuwa likisahau viti juu ya meza na baada ya kulala mvulana alitoka mafichoni na kuvichukua. Zimwi lilipoamka halikushughulika na vitu hivyo. Ni nadra mtu kusahau vitu vyake na kukosa kufuatilia baada ya kuvikosa. Pia liliridhika na majibu ya mkewe bila ubishi ilhali lilikuwa na uwezo wa kunusa harufu ya binadamu.

Matumizi ya chuku ni maarufu sana katika ngano za fasihi simulizi. kwa kuwa hadhira huwa haiulizi maswali na kusaili ukweli wa matukio. Ngano hizi huegemea sana katika upande wa funzo au maadili inayofumbatwa na ngano husika. Hadhira ya ngano nyingi za fasihi simulizi huwa ni watoto ambao hawakuuliza maswali kuhusu ukweli wa ngano hizo. Dhima kuu ya ngano hizi ilikuwa kuadilisha jamii hususan watoto wadogo nahivyo basi zilitekeleza wajibu wake.

4.5.2.7 Majazi

Hii ni mbinu ya kuwapa wahuusika majina kulingana na tabia au matendo yao. Kama ilivyoelezwa hapo juu, neno “*Irimū*” katika lugha ya Gĩkũyũ lina maana ya “ukubwa.” Kutokana na msuko wa ngano hizi za mazimwi, wahuusika hawa wamesawiriwa kuwa na sifa ya kiumbe kikubwa na yanayodanganyika kwa urahisi. Katika ngano ya Mvulana na Zimwi, liliposema kuwa lilihisi harufu ya binadamu katika nyumba, lilidanganywa kuwa ni harufu ya mbuzi na kuku na likiridhika bila kuchunguza zaidi. Katika lugha ya Gĩkũyũ, neno linalotumiwa kurejelea zimwi ni ‘*Irimū*’ au ‘*k̄rimū*’ likiwa na maana ya “-kubwa”. au jitu. Jina *Wairimū* lilitumika kwa binti wa saba wa Gĩkũyũ na Mumbi kutokana na kimo chake kikubwa.

Ngano hizi kama zingine za fasihi simulizi zimetumia majazi katika kuwapa wahuusika majina kama inavyodhihirika katika ngano ya Vijana watatu ambapo ndama ametumika kama mhusika. Ndama huyo alijulikana kama “*Gacau Mũndũ*” neno linalomaanisha ‘ndama mtu, Ndama huyu alikuwa akiongea na kutenda matendo ya kama binadamu kwa mfano, anamwarĩfu mwanawe wa ThomeThome kuhusu njama ya kutiliwa sumu kwenye chakula ili afe na kumshauri atakavyofanya ili kumuokoa.

4.5.2.8 Kinaya

Hii ni mbinu ya kusema ua kufanya mambo kunyume na matarajio. Ngano za mazimwi zinawasawiri kama wahuusika walio na uwezo kuliko binadamu wa kawaida lakini kwa upande mwingine yanaonekana yakiwa mapumbavu. Wanadanganyika kwa urahisi kwa kushindwa kung’amua masuala mepesi kama ujumbe katika ngano. Mfano ni katika ngano ya Msichana na Zimwi ambapo msichana anapoimba akiomba msaada, zimwi halinkug’amua ujumbe katika wimbo huo ilhali ujumbe huo ulikuwa wazi.

Mazimwi yanaonyeshwa kuwa maadui wa binadamu lakini yanaonekana kuishi na binadamu na yanakuwa kama sehemu moja ya wanajamii. Katika ngano ya ‘Mama Aliyejifungua na Zimwi’, mama mjamzito aliishi na zimwi huku akidhulumiwa bila kujali au kuomba msaada kutoka kwa binadamu wenzake. Kwingi mazimwi yanaonekana kutenda wema kiasi cha kuwafanya wapewe nafasi katika jamii zao licha ya maovu wanayoyatenda.

Licha ya uwezo walio nao, mazimwi yanauawa na watu wasio na ujuzi wa kivita kwa urahisi. Wanaonekana kuwaogopa binadamu katika baadhi ya ngano. Mfano ni katika ngano ya Mama Aliyejifungua ambapo zimwi linahofia kupatwa na mumewe mama. Mvulanamdogo pia analiua zimwi lililokuwa limemuua hata babake kijana aliyekuwa shujaa kwa kuukata mti zimwi lilipokuwa linateremka.

Mazimwi yalimeza binadamu pamoja na mifugo yao na hawakushiba. Walipouawa watu waliokuwa bado wamo mwilini mwa zimwi bula kufa. Tunatarajia watu na mifugo wao wafe lakini waonekana kutoka viungoni mwa zimwi kama vidole. Mbinu ya kinaya imechangia na kuendelezwa hali ya kukiuka uhalisia au kuleta uhalisia mazingaombwe.

Ni kinaya kuwa watu waliendelea kuishi na mazimwi ilhali yaliwadhulumu. Kama Nandwa (1983) anavyosema kuwa wanaweza kuishi miongoni mwa watu au yakaishi mapangoni. Kutokana na madhara waliyoyapata kutoka kwa mazimwi, ingetarajiwa watu waungane na kuyasaka na kuyauwa kabla ya mazimwi kuwaangamiza.

4.5.2.9 Maswali ya Balagha

Hii nimbinu ya matumizi ya maswali yasiyohitaji majibu. Maswali haya hutumika kuchochea hadhira kuliwazia suala linaloulizwa, kuibua hisia kutokana na maelezo na pia kusisitiza ujumbe. Mfano, mbinu hii imetumika katika ngano ya Njiru ambapo mama mwenye vijana alipoenda kuomba moto aliulizwa na zimwi, “Kwani wewe waishi wapi kwa vile nywele zako zilivyorefuka?” zimwi lilikuwa likimdhihakiki kwa vile alikuwa na nywele ndefu zilizoonyesha dalili ya kutochanwa kwa muda mrefu.

Balagha imetumika katika ngano ya Mama na Zimwi. Zimwi liliporejea na kugundua kuwa mama alikuwa na ujasiri siku hiyo usiokuwa wakwaida na akashuku kulikuwa na sababu. Zimwi lilimuuliza, “Kwa nini umekuwa na ujasiri mwingi kama walioenda uhunzi

wamerejea?” swali hili halikutaka kujibiwa mbali lilidhamiria kuonyesha kuwa haikuwa kawaida yule mama kumjibu hivyo. Labda kulikuwa na mtu aliyemfanya ajasirike.

Katika ngano ya Msichana na zimwi, msimulizi anashirikisha hadhira yake kwa maswali ya Balagha anapouliza swali ili kuonyesha zimwi lilivyokuwa likifanya. Anauliza, 'si wakati huo msichana alikuwa akijifungua zimwi lilipokuwa likimuuliza kama amefika? Swali hili lilidhamiria kumshirikisha hadhira na kuteka makini ya hadhira.

Zimwi lilipoanza kushambuliwa na mumewe aliyekuwa amejificha uchagani, lilianza kulia na kusema, “Si nilisema kuwa waliokuwa uhunzi wamerejea?” Maswali hayo hayakuhitaji kujibiwa mbali yalitaka kuibua hisi za kujutia matendo yake kwa kutofanya jambo baada ya kushuku kuwa kulikuwa nanjama. Balagha hii ilikuwa ikionyesha majuto.

Katika ngano ya Njiru, kijana mmoja aliyefuja mali yake na akaamua kwenda kuwatapeli watu, alipowapata aliwauliza maswali ya balagha ambayo alidhamiria kuwapa changamoto ili wakubali kuingia mtegoni. Kwa mfano aliwauliza, “ mnavaa manyoya kwa kukosa ngozi? Hebu chukueni hii yangu.” Maswali hayo yalimsaidia kutimiza lengo lake la kuwatapeli. Haya maswali hayakuhitaji jibu.

Maswali mengine ya yanaulizwa na msimulizi ili kushirikisha hadhira katika usimulizi. Kuna yale yalioulizwa na kujibiwa na msimulizi mwenyewe hata baada ya kujibiwa kama usemezano wa watu wawili. Maswali haya ya aina mbili yametumika katika ngano za mazimwi zilizoteuliwa.

4.5.3 Mbinu Zingine

4.5.3.1 Nidaa

Hii ni mbinu ambayo hutumika kuonyesha hisia fulani kama vile mshangao, furaha, hasira au kukataa jambo fulani. Alama ya mshangao zimetumiwa kuleta hisia iliyokusudiwa. Mbinu hii pia imetumika sana katika ngano za mazimwi ili kuibua hisia zinazodhamiriwa na msimulizi.

Kwa mfano katika ngano ya Mama na zimwi, nidaa imetumika pale ambapo zimwi linaangusha kuni na kusema ‘*Hu!*’ na kumwambia mama aanguke kama mwanguko wa kuni

hizo. Nidaa ilitumika kuonyesha uchovu baada ya zimwi kubeba kuni nyingi ambazo zilikuwa za kumpika na kumla mama.

Katika ngano ya vijana watatu, mhusika Thome alipokaidi yale aliyokuwa akitakikana kuyatenda na zimwi, zimwi lilimlaani na kuwambia, ‘*Urogwa hau!*’Yaani“Anguka ulipo!” naye akamjibu, “*O nawe Ũrogwa!*”“Hata nawe uanguea hivyo! Maneno haya yanaibua hisia mbalimbali kulingana na mada kama kuonyesha hasira na kulaani.

4.5.3.2 Nyimbo

Nyimbo zimetumika kwa wingi katika ngano na zinarudiwarudiwa kila baada ya muda. Katika ngano ya Zimwi na msichana, wimbo ulitumiwa kuwapasha habari jamaa zake ili waje kumuokoa asije akaliwa na zimwi. Zimwi pia lilitumia wimbo kutoa hisia zake na kutisha msichana huku likitaka kujua msichana alikokuwa amefika. Hapa wimbo ulitumika kama njia ya kuwasilisha ujumbe kati ya msichana na Ndugu zake na pia zimwi na Msichana.

Katika ngano ya Mama Aliyejifungua, ndege alipitisha ujumbe kwa mumewe akiwa mbali kupitia ndege kwa wimbo. Ndege alikwenda alikokuwa mumewe Mama Aliyejifungua na kumwambia wimbo uliosheheni ujumbe. Mumewe aliweza kufasiri ujumbe kuwa mkewe alikuwa amejifungu na alikuwa hatarini kwa sababu ya zimwi na akafungasha virago vyake hadi nyumbani.

Hii mbinu imejitokeza sana katika ngano za mazimwi ambapo wahusika wa aina mbalimbali wanatumia wimbo kupitisha ujumbe kwa wengine. Nyimbo nyingine wahusika wanajibizana na kuwasiliana ilhali nyingine zinafichua mambo yaliyofichika. Kando na kupitisha ujumbe, zinaibua hisia zinazokusudiwa na msimulizi kwa hadhira au mhusika.

Kulingana naWamitila (2003) anasema nyimbo hutumika kama kiliwazo ambapo hadhira hutulizwa kidogo hasa kwenye hadithi zinazozungumzia masuala ya kusikitisha au ya kitanzia.Katika ngano ya mama na zimwi, tunatarajia aliwe na zimwi lakini kabla ya hayo ndege analeta ujumbe kwa wimbo na hadhira inatulizwa na jambo hilo kwa kuleta matumaini mapya tena katika ngano.

Zaidi ya hayo, wimbo hutumiwa kuburudisha hadhira na kuondoa ukinaifu kwa hadhira kutonana na kubadilisha mtindo wa usimulizi. Hadhira hushiriki katika uimbaji kwa kuwa

wimbo huo huwa umerudiwarudiwa na hadhira ikaweza kuufahamu. Nyimbo zilizotumiwakatika ngano zina mahadhi tofauti tofauti kulingana na ngano. Zile zilizo na mazimwi, nyingi huimbwa kwa mahadhi yenye kitetemeshi na sauti nzito na ya kutisha ikilinganishwa na iliyo na wahusika wanawake na watoto zinazoimbwa kwa mahadhi ya kuashiria udhaifu na kutaka msaada au kuhurumiwa.

Nyimbo katika ngano huwa ni kipengele muhimu katika upande usimulizi kwa kufanikisha uganaji. Ni mojawapo wa njia ya kuonyesha umaarufu wa mtambaji bora wa ngano za fasihi simulizi. Zimetumiwa kuisitiza kiini au wazo kuu katika hadithi.

4.5.3.3Takriri

Takriri ni mojawapo wa tamathali za usemi ambayo inahusu urudiaji katika lugha. Ingawa urudiaji ni wa aina nyingi sana, kama vile: takrirri neno, usambamba na kadhhalika. Msokile (1992:61) anaeleza kuwa; “Takriri ni urudiaji wa silabi, maneno, mistari au vifungu vinavyolingana katika kazi ya sanaa”.Lengokuu la msimulizi kurudiarudia maneno au vipengele hivyo ni kulitilia mkazo jambolinaloelezwa. Usambamba wa kimuundo ni aina ya urudiaji ambao hujengeka katika urudiaji wa muundo ulio sawa. Urudiaji wa aina hii hupatikana sana katika nyimbo za ngano.

Ngano nyingi za fasihi simulizi zinatumiya urudiaji katika, tanakali za sauti. Mfano ya maneno ni kama: kukimbia kaba! kaba! kaba! na kuku kuku! kuonyesha vile zimwi au wahusika walilikimbia ua kukimbizwa. Pia urudiaji ulitumiwa kuonyesha jinsi kitendo kilitendeka kama vile zimwi linaimba na kusema lingekata titi la msichana ng,we! ng’we!. Hii ni baada ya msichana kuhepa kwa kutumia ujanja na zimwililipogundua kuwa alikuwa ametoroka lilianza kuimba kwa Vitisho vile lingefanya.

Aidha katika miktadha mingine, urudijumetumiwa kutilia mkazo kwa mfanokuonyesha mwendo ulivyokuwa mrefu kama. Akaenda, akaenda, zimwi likakimbia kaba! kaba! kaba! kaba!, akachukua miguu kuku kuku! na kadhhalika. Pia urudiaji huu unawafanya wasikilizaji kujenga taswira mbalimbali kichwani na kuteka makini.Urudiaji wa kimtindo ndio umetumika kwa wingi katika ngano hizi. Huu unahusu kurudia vifungu vya maneno au namna ngano inavyosimuliwa. Takriri hii ni ya usambamba ambapo ngano zinachukua mtindo wa aina sawa ingawa matukio ni tofauti.

Nyimbo zimetumika kwa wingi katika ngano na zinarudiwarudiwa kila baada ya muda. Katika ngano ya Zimwi na msichana, wimbo ulitumiwa kuwapasha habari jamaa zake ili waje kumuokoa asije akaliwa na zimwi. Zimwi pia lilitumia wimbo kutoa hisia zake na kutisha msichana huku likitaka kujua msichana alikokuwa amefika.

Ngano ya Mama Aliyejifungua inaonyesha ndege akitumiwa kupitisha ujumbe kwa mumewe aliyekuwa mbali kupitia kwa wimbo. Hii mbinu imejitokeza sana katika ngano za mazimwi ambapo wahusika wa aina mbalimbali wanatumia wimbo kupitisha ujumbe kwa wengine. Nyimbo hizi zinaibua hisia zinazokusudiwa na msimulizi kwa hadhira au mhusika. Ngano zinaposimuliwa, urudiaji wa nyimbo unatekeleza majukumu mbalimbali kama: kuburudisha hadhira, kuwashirikisha hadhira katika ngano husika nakuondoa ukinaifu kwa kubadilisha mtindo wa usimulizi miongoni mwa mengine.

4.6 Umuhimu wa Ngano za Mazimwi

Kutokana na maudhui, mbinu mbalimbali zinazoingiliana na msuko ni dhahiri kuwa ngano za mazimwi zina jukumu muhimu katika jamii ya Gikūyū. Mazimwi yalisawiriwa kwa njia ya kutisha na kuogofya kutokana na sifa wahusika hawa walizopewa. Mazimwi yamepewa sifa za kiajabuajabu kama kuwa na vinywa viwili kimoja mbele na kingine nyuma kama inavyojitokeza katika ngano ya Msichana na Zimwi. Mazimwi mengine kuwa na jicho utosini, kama katika ngano ya Mvulana na Zimwi, kuwa na upembe mmoja na kadhalika.

Sifa hizi zinafanya ngano hizi kutisha wahusika na hivyo basi kuwa chombo muhimu chakukanya na kuonya. Walioonywa walistahili kuwa makini zaidi hasa wasichana na watoto walioonekana kuwa katika hatari ya kudhulumwa na waliokuwa na uwezo. Kwa wasichana walikanywa dhidi ya kuolewa na watu siowajua kwa kuwa huenda wakaolewa na wavulana wa jamii nyingine na wakafichua siri za jamii hiyo. Ngano ambazo zilitumiwa na jamii kutimiza lengo hilini za mazimwi kwa kuwa ziliwafanya kuogopa kutokana na masimulizi yake. Kupitia kwa ngano hizi, mazimwi yalisemekana kujifanya vijana wazuri na wenye kuvutia na kisha kuwadanganya wasichana na kuwala. Kama ilivyotokea hatimaye katika ngano ya msichana aliyekaidi na kwenda kuolewa na kijana aliyegeuka kuwa zimwi lililotaka kumla.

Dhima nyingine ya ngano za mazimwi ni kukashifu matendo maovu katika jamii kwa kuwa wahusika hasidi au waovu waliishia kuangamia na kuondolewa katika jamii. Dhima hii inadhihirika kupitia kwa ngano zote ikiwamo ya Njiru, Vijana Watatu na Zimwi n.k. Ngano zote zinaoyesha wahusika walio na matendo maovu wakiadhibiwa na jamii na kutukuza wanaofanya matendo mema. Ngano ya Njiru inaishia vijana wakiliua zimwi na kukomboakila kitu kilichochukuliwa na zimwi. Vijana walioua zimwi wanatuzwa na kutambuliwa na wajamii kuonyesha kuwa jamii inachukia maovu.

Fauka ya hayo, ngano za mazimwi hutufunza maadili kama: uaminifu, kufuata ushauri, ushirikiano, kutii wakubwa na kadhalika. Mwangi (1970), asema kuwa ngano hizi hukuzi maadili katika jamii, kwa kutuza wanaotenda mema kama: uhirikiano, utu, utiifu na kadhalika. Haya yanajitokeza kwa kuyachora mazimwi yakiwa na tabia kinyume na matakwa ya jamii kama tamaa, ubinafsi, ukatili, unafiki na kadhalika na kuwaangamiza hatimaye kuonyesha kuwa vitendo vyao havina nafasi katika jamii pamoja na wanaotenda maovu kama hayo.

Mazimwi ni kiashiria cha watendao mabaya katika jamii ambao tunaishi na kunatangamana nao katika shughuli za kila siku lakini ni maadui wa jamii kwa vitendo vyao ambavyo huangamiza jamii. Hawa ni watu ambao hata jamii ya leo inawakataa. Wasichana walitahadharishwa dhidi ya kuolewa na watu kama hawa kwa kuwa mwishowe watawaangamiza. Hata kwa watoto, watu hawa ni hatari kwa usalama wao.

Unafiki wa mazimwi wa kuonekana kutenda mema ulikuwa ni chambo cha kuwashika wale ambao hawakuwachunguza kwa makini na kujua hila zao. Maovu ya mazimwi yalikuwa kero kwa jamii nzima na yaliangamiza watu binafsi, familia na hata jamii nzima. Kama ilivyo leo, matendo kama: ufisadi, mauaji, ulaghai, ubinafsi, usaliti ni baadhi ya matendo yanayoweza kuwa na athari kwa mtu binafsi au jamii yote.

Ngano hizi pia zinaburudisha hadhira hasa watoto wadogo ambao walitambiwa ngano hizi. Zilisimuliwa kwa kutumia mbinu mbalimbali kama nyimbo ambazo zilikuwa na mahadhi mbalimbali ya kupendeza. Matukio pia yanafuatana kwa njia inayomfanya msikilizaji kufuata kisa hadi mwisho kwa kutumia mbinu kama taharuki. Mbinu hii inafanya hadhira kutaka kujua yatakayofuata na hatima ya mambo. Msuko wa ngano hizi ni sahili na kwa hivyo unaweza kufuatika kwa urahisi kwa kuwa ulilenga watoto.

Fauka ya hayo, ngano hizi zinahifadhi historia na utamaduni wa jamii ya Gĩkũyũ. Kuna mengi yanayoeleweka na hadhira pale tu kwanza wanaelewa utamaduni wa jamii hii. Mfano ni kazi zilizotendwa na wanajamii husika kama vile uhunzi katika ngano ya ‘Mama Aliyejifungua na Zimwi’. Tunapata kujua kwa nini wahunzi walikwenda mbali na walikoishi watu wengine na faini iliyotozwa wale waliokaidi kufuata sheria. Shughuli za kijamii na kiuchumi za wanajamii pia zinaweza kutambuliwa kupitia kwa ngano hizi kama vile: kulima, kufuga, uhunzi, uchezaji ngoma na kadhalika.

Utamaduni wa jamii unadhihirika kupitia kwa ainambalimbali ya mimea waliyopanda, kama: mtama mawele, shayiri, ndizi, maharagwe n.k. pamoja na aina ya vyakula wanavyokula kama uji, nyama n.k. Mfano katika ngano ya Mama Aliyejifungua na Njiru, tunapata taswira ya chakula alicholetewa mama na kilichopandwa shambani na watu. Kando na mazao ya shambani, tunaweza kujua zana mbalimbali vya kutumia katika kazi zao kama ‘kienji’ ambazo zilitumika katika kujihami na ni sehemu ya utamaduni wa jamii husika.

Majukumu mbalimbali yalitekelezwa kulingana na jinsia, umri nafasi katika jamii na kadhalika kama inavyodhihirishwa na matukio katika ngano. Kwa mfano vijana walikuwa na jukumu la kuilinda jamii na wanawake kulea watoto. Wanaume walikuwa na jukumu la kuikimu jamii na waliposhindwa zimwi lilipata nafasi ya kuingilia jamii na kuiangamiza kwa kujidai kuwa rafiki na mwokozi. Suala hili liliwafanya watu kuwajibika na kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

4.7 Hitimisho

Surahii inaelezea fani mbalimbali zilizotumika katika ngano za mazimwi. Matumizi ya lugha katikangano za mazimwi yameangaziwa kama matumizi ya tamathali za usemi zilizotumiwa ili kutoa mvuto wa kisanaa, na zilivyochangia katika muundo wa ngano zililizoteuliwa. Baadhi ya tamathali za usemi ambazo zimegusiwa ni pamoja na tashbihi, tashhisi, chuku, kinaya nidaa, takriri miongoni mwa nyingine. Zimetumiwa kufafanua maana, kuibua hisia, kuhuisha na kuburudisha. Mbinu nyingine za lugha ambazo zimetumika ni kama: ishara,, tanakali za sauti, taswira na nyimbo.

Fani imefanikisha uwasilishaji wa ngano za mazimwi na pia zimetumika kama kipengele mojawapo cha kuhakiki ngano hizi. Ishara ya mazimwi imehakikiwa na kuonyesha uhusiano

wake na dhamira na maudhui. Mbali nahayo, sifa za mazimwi zimebainishwa kutokana na jinsi wahusika hawa wamesawiriwa. Mwisho kabisa, sura hii imetathmini jukumu la ngano za mazimwi katika jamii hii kutokana nangano aina mbalimbali.

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Surahii inatoa muhtasariwa tasnifu na matokeo ya utafiti. Ina sehemu zinazoshughulikia matokeo ya utafiti, tathmini ya maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti na mapendekezo ya utafiti zaidi kuhusiana na ngano za mazimwi.

5.2 Hitimisho

Utafiti huu umedhihirisha kuwa ngano za mazimwi katika jamii ya Gĩkũyũ zina sifa maalumu zinazofungamana na jamii husika. Kwa upande wa wahusika, mtafiti amebainisha sifa mbalimbali za wahusika kama zinavyojitokeza katika ngano za mazimwi katika jamii ya Gĩkũyũ. Sifa tofauti za mazimwi zimedhihirika kulingana na ngano. Sifa nyingi za wahusika mazimwi zinalingana na za jamii nyingine isipokuwa chache zinazotofautiana kabisa kama kuwa na sifa za pepo au jini, kutoa moto na kusababisha mabaa kama njaa yanavyojitokeza katika jamii nyingine. Mazimwi yanawakilisha binadamu wa kawaida hasa wale waovu wanaoenda kinyume na matakwa ya jamii lakini hatima yao ni kuangamia na kuwa mfano kwa wanaofanya maovu.

Utafiti ulidhamiria kubainisha sifa za ngano za mazimwi katika jamii ya Gĩkũyũ kwa vile sifa za mazimwi zinatofautiana kulingana na jamii na mazingira yake. Sifa hizi zimechangia kwa pakubwa kuendeleza maudhui na dhamira ya wanajamii kutokana na matendo na hulka wanazodhihirisha. Wahusika mazimwi katika ngano hizi wametumiwa kisitiari kuwakilisha tabia za binadamu halisi katika jamii. Wamesawiriwa wakiwa wahusika hasidi na hata wale walio na wema, wema huo ni wa kinafiki wakitafuta watu wa kuwalaghai na hatimaye kuwaangamiza. Mhusika wenye tabia mbaya hawastahili kuigwa. Hatimaye ngano hizi zinaishia kwa matumaini mazimwi yanapouawa na kufanya maovu kushindwa na wema.

Kutokana na maudhui, dhamira na msuko wa ngano hizi kama nyingine za fasihi simulizi zina jukumu muhimu katika jamii. Dhima kuu ikiwa ni kukuza maadili, kuadilisha jamii kwa kukashifu maovu, kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii na kuelimisha kando na kuburudisha. Ngano za mazimwi ni kipera mojawapo katika utanzu wa hadithi katika fasihi simulizi kinachotumiwa na wanajamii kuendelezwa na kuhifadhi utamaduni wao.

Sababu kuu ilikuwa ni kuhakiki fani na ishara ya mazimwi kutokana na usawiri wa wahusika. Sifawalizopewa na wanajamii zinaibua ishara mbalimbali kwa wanajamii. Ngano mbalimbali zilizoteuliwazilidhihirishapia matumizi ya mbinu tofautitofauti za kifasihi ili kutimiza malengo ya jamii ya Gĩkũyũ. Ili kuyafikia malengo haya ya uhakiki, mtafiti alitumia nadharia ya Umuundo na Umuundoleo. Wataalamu wa nadharia ya umuundo wanatilia mkazo uhakiki wa kifani katika kufasiria matini na kupimia kufana au kutofana kwa mtunzi katika kazi yake ya usanii. Wanakubaliana kuwa fani ni jumla ya viambajengo vya kazi ya kifasihi vinavyotumiwa na msanii katika kupitisha ujumbe wake kwa hadhira.

Wanaumuundoleo walieleza hali ya ishara moja kuwa na maana nyingi kwa kuiweka au kuikita maana kwenye muktadha wa kijamii, hivi kwamba jamii inakuwa na athari kubwa katika kutoa maana. Wasomi hawa wana mawazo kuwa kiashiriwa hakiwezi kuwa funge mbali huweza kuwa na maana tofautitofauti kulingana na jamii. Nadharia hii ilikuwa muhimu katika kubainisha ishara mbalimbali za mazimwi kwa mujibu wa usawiri wa wahusika katika ngano zilizoteuliwa. Ngano za mazimwi zimedhihirisha ishara mbalimbali hivi kwamba kupitia kwa ngano hizi, taashira ya mauti, ukatili, maangamizi, maovu na kadhalika inajitokeza. Ishara hizi zinatofautiana na kuwa na maana mbalimbali kulingana na msuko wa ngano na usawiri wa wahusika.

Ilidhihirika kuwa ngano zina matumizi changamano ya fani kutokana na mbinu mbalimbali zilizochanganuliwa katika ngano za mazimwi zilizoteuliwa kama vile: ishara, chuku, tanakali za sauti, misemo, tashihisi, tashbihi, taharuki, nyimbo, taswira, nidaa, balagha, kinaya, takriri. Aidha msuko, wahusika, maudhui na usimulizi ulichanganuliwa kama sehemu ya mtindo unaotumika kufanikisha ujumbe na dhima ya ngano hizi katika jamii husika.

Ngano hizi zimetumia msuko sahili ambao unaeleweka kwa urahisi kwa kuwa ulilenga hususan watoto ili kuwaonya, kuwatahadharisha, kuwaelimisha, kuhifadhi utamaduni wa

jamii na kadhalika. Migogoro imekuzwa kwa njia ambayo ina mfululizo unaotiririka kuanzia mwanzo hadi mwisho wa ngano. Usahili wa msuko unachangia katika kukumbukika kwa ngano hizi kwa urahisi na kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa urahisi.

Vipengele vya fani vina mchango mkubwa sana katika kuwasilisha ujumbe na kufanikisha malengo ya ngano. Hali kadhalika, vipengele vya fani kama msuko wa ngano vimesaidia kuleta picha kamili yautamaduni wa jamii ya Gĩkũyũ kwa kuchora picha halisi ya jamii katika mazingira yao. Aidha fani ina mchango mkubwa katikakufanikisha lengo la msimulizi wa ngano za mazimwi. Kutokana na uhakiki, inadhihirika kuwa vipengele vya fani ni changamano na vimeingiliana na kuhusiana katika ujenziwa umbo au muundo wa ngano za mazimwi. Ishara ikiwa mojawapo wa mbinu iliyohakikiwa imejitokeza kuwa mazimwi huwa ni wahusika waliotumika kuashiria dhana mbalimbali katika jamii. Ishara hizi hujengwa na matumizi ya mbinu nyingine kama taswira, chuku, tashibihi, taharuki na kadhalika zinazosawirri wahusika hawa wakiwa viumbe wa kutisha, katili, waovu na wenye maumbile yaliyokiuka uhalisia.

Msuko na masimulizi pamoja na uumbaji wa wahusika vimeingiliana na kujengana hivi kwamba kipengele kimoja hakiwezi kujisimamia bila kuathiri kingine. yotehatimaye yanaleta muundo wa nganouliokusudiwa. Usawiri wa wahusika hawa huenda sambamba na dhamira ya wanajamii hasa ya kukashifu maovu katika jamii. Zimwi linapotajwa, ishara ya ukatili, mauti, udhalimu na maovu miongoni mwa mengine hujengeka akilini mwa mwanajamii.

Ni dhahiri kuwa ngano hizi ziliwalenga wanawake na watoto kama hadhira na zilitumika kuwaonya kujiingiza kwenye hali hatari kwa maisha yao. Isitoshe wanawake na watoto waliokolewa na wanaume kila mara walipokuwa hatarini ya kuangamizwa na mazimwi. Lengo lilikuwa kukuza jamii katika misingi ya kiuana.

5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa ngano za mazimwini umuhimu katika jamiiya leo kutokana na majukumuyanatekelezwa na ngano mbalimbali ya mazimwi. Ili kutimiza lengo hili, ngano zimetumia mbinu changamano. Ni muhimu kufanya utafiti zaidi kuhusu suala la ubabedume kwa kurejelea ngano za mazimwi kwa vile jamii inaonekana kudhibitiwa na wanaume. Jinsia ya kiume imetukuzwa hivi kwamba hata mvulana angeweza kuliua zimwi

lakini wanawake na watoto waliokuwa hatarini. Nadharia ya ufeministi inaweza kutumiwa kuhakiki.

MAREJELEO

Adagala, K. & Kabira, W. (1985). *Kenyan Oral Narratives: A selection*. Nairobi: Heinmann Kenya.

Aguilar, J (2008). Symbolism in Literature, A Literature journal. Poetry...mhtml:file://D:\laikipia d\Symbolism in Literature\

Akivanga, S. & Odanga, B. (1982). *Oral Literature: A School Certificate Course*. Nairobi: Ibadan London. Heinemann Educational Books.

Aston, E.& Savona, G. (2005). *Theatre as a Sign System: A Semiotics of Text and Performance*. London & New York: Routledge.

Aswani, B., Mayaka, G. & Riro, M.. (2014). *Misingi ya Nadharia na Mbinu za Utafiti*. Mwanza: Serengeti Education Publishers.

BAKITA (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Banerji, P. (1994). *A Guide to Academic Writing*. Eldoret Kenya: Kijabe Printing Press.

Bell, J. & Opie, C. (2002). *Learning from Research*. Gas-gow U.K. Open University Press.

Bukenya, A.& Nandwa, J.(1983). *Oral Literature for Schools*. Nairobi: Longman.

Bukenya, A. (1991). *Oral Literature Theory*. (BEL 201(B) College of Education & External Studies. Nairobi: Nairobi University Press.

Chandler, D. (2005) *Semiotics for Beginners*. Aberyswyth University. Available at:<http://www.aber.ac.uk/media/Documents/S4/sem01.html>.

Chikati, J. (2000). *The Project Writing. Handbook*. Nairobi: Signal Press.

Elegwa, M. & Muriuki, W. (1996). *Narratives from Africa and India for Secondary Schools and College*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

- Finnegan, R. (1977). *Oral Literature in Africa*. Nairobi: Oxford University Press.
- Gail, C. (2005). *Writing for Academic Success: A Postgraduate Guide*. London: SAGE Publishers.
- Gitaru, J. (1989). "Uhakiki wa Muala Katika Ngano za Waswahili." Haijachapishwa. Tasnifu ya Uzamili chuo Kikuu cha Nairobi.
- Griffen, E. M. (1997). *A First Look At Communication Theory*. New York: McGraw-Hill Companies Inc.
- Hezel, H. (2007). *Write Great Essays and Dissertations*. Great Britain: Macmillan.
- Holman, C. & Harmon, K. (1986). *Faces of Islam in Africa Literature*. London: Heinemann Portsmouth.
- Kabira, W. & Mutahi, K. (1988a). *G'kũyũ Oral Literature*. Nairobi: Heinemann Kenya.
- Kabira, W. & Mutahi, K. (1988b). *Oral Literature*. College of Education and External Studies. Nairobi: University of Nairobi. Nairobi Press.
- Katie, W. (2001). *A Dictionary of Stylistics*. 2nd Edition. Harlow: Longman (Pearson Education).
- Kezilahabi, E. (2007). *Dunia Uwanja waFujo*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
- Keya, S. (1989). *Guidelines for the Formation of Research Project Proposal*: O.U.P. For National Council for Science and Technology. Nairobi.
- Kilanga, (2014). "Ishara Katika Kaptula la Marx na Kijiba cha Moyo: Mtazamo wa Kisemiotiki". Haijachapishwa. Tasnifu ya Uzamili chuo Kikuu cha Nairobi.
- Kimani, N. & Rocha, C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*. Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Kirumbi, F. (1975). *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Shungwaya Publishers Ltd.
- Kombo, D. & Tromp, L. (2006). *Proposal and Thesis Writing*. Nairobi: Paulines Publishers.
- Kothari, C. (2004). *Research Methodolog: 2nd Ed Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishers.

- Liyong, T. (1972). *Popular Culture of East Africa*. Nairobi: Longman.
- Maclean, I . (1986) *Reading and Interpretation*. In *Modern Literary Theory: A Comparative Introduction*, 2nd edition: B.T. Batsford Ltd.
- Matteru, L. (1979). “Utafiti, Mbinu na Ukusanyaji wa Fasihi Simulizi na Hatima Yake”.Lugha Yetu uk.34-36. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mbatia, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks, Graphics and Publishing.
- Mbele, J. (1982).*Oral Literature and the Written Tradition*. Heinemann Educational Books.
- Mghanga, J. (1984). “Fasihi Simulizi Katika Jamii: Uhakiki wa Ngano wa Kidawida.”Haijachapishwa. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.
- M’ngaruthi, T. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dare es Salaam University Press.
- Mugenda, O. & Mugenda, A. (2003).*Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches* .Nairobi: A.C.T.S.
- Mulokozi, M. (1983). “*Utafiti wa Fasihi Simulizi*, Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili” Uk. 42-50.
- Muriuki, G. (1974) *A History of the Kikuyu 1500-1900*.Nairobi: Oxford . Kenya Litho Ltd
- Murray, R. (2011). *How to Write a Thesis*. 3rd Ed.United Kingdom: Open University Press.
- Mwangi, R. (1970). *Kikuyu Folktales*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Nandwa, J. & Bukenya, A.(1983). *Oral Literature for Schools*. Nairobi: Longman:
- Ndungo, C. & Wafula, R.(n.d.).*Nadharia ya Fasihi Simulizi; Kiswahili (part 3) BSW308 (A)*. University of Nairobi.
- Ngara, E. (1985). *Art and Ideology in the African Novel*. London: Heinemann.
- Propp, V. (1968).*Morphology of the FolkTale*. London: University Press of Texas.

- Timammy, R. (1990). “Uhakiki wa Ngano Za Kiswahili”.Tasnifu na Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- TUKI (1981). *Makala za Semina ya Fasihi Simulizi*. Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam: TUKI
- TUKI (1983). *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III*.Dar es Salaam, TUKI
- TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam, TUKI.
- Odaga, A. (1984). *Yesterday Today: The Study of Oral Literature.*: Kisumu Lake Publishers & Enterprises.
- Okech, J.(2013). “Uhakiki wa Fani Katika Ngano Tano za Kiswahili”. Haijchapishwa Tasnifu na Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Okpewho, I. (1983). *Myths in Africa: A Study of its Aesthetic and Cultural Relevance*. Lodon: Cambridge University Press.
- Ross, R. (1974). *Research: An Introduction*. New York: Barnes and Noble Books.
- Saravanel, P. (1987). *Research Methodology*. New Delhi:Kitab Mahal Agencies.
- Wafula, R. & Kimani, N.(2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wales, K. (2001).*A Dictionary of Stylistics. (2nd Edition)*London: Pearson Education Ltd .
- Wamitila, K. W. (2002).*Uhakiki wa Fasihi-Misingi Na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Wamitila, K. W. (2003).*Kamusi ya Fasihi: Istilahi na nadharia*. Nairobi: Focus Books.
- Wamitila, K. W. (2003).*Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*.Nairobi: Focus Publications Ltd.
- Wamitila, K. W. (2008).*Kanzi ya Fasihi, Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi. Vide-Muwa Publishers.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO (a): NGANO ZA MAZIMWI ZA GĪKŪYŪ

(1) IRIMŪ NA MŪIRĪTŪ

Tene tene mŭno nĭkwarĭ andŭ metagwo marimŭ no marĭ tŭnua twĭrĭ, kamwe karĭ na haha thutha na gaka (ka mbere). Rŭu nĭ mahithaga mŭno kanua ga thutha tondŭ nĭkanyitaga nginya ngi. Marimŭ mahanaga ta andŭ no magagĭtwĭka nĭmarimŭ na nĭmarĭtaga andŭ. Rŭumarimŭmarĭa nĭmararĭirie rwĭmbo. Airĭtu magĭkĭona anake athaka mŭno. Magĭgĭthiŭrwĭmbo rŭu rwa marimŭ.

Rŭu mŭirĭtu ũmwe-rĭ, akĭrirĭria irimŭ rĭmwe rĭarĭ ithaka mŭno. Akĭŭra ũrĭa ũngĭ, “Nĭ nĭngŭmbwo nĭ irimŭ rĭrĭ.” Mŭirĭtu akĭŭmbwo nĭ irimŭ. Akĭŭwo nĭ arĭa angĭ ihĭ rĭrĭ nĭ irimŭ. Akĭrega akiuga ihĭ ũyŭ nĭ mwanake. Nĭmagĭikire ũguo-ĭ, marĭkia rwĭmbo na matuĭka rŭu nĭ mekŭinŭka-rĭ, mŭirĭtu ũrĭa akĭmenya we ndegŭŭtigwo nĭ irimŭ rŭu.

Akĭŭra airĭtu arĭa angĭ. Airĭtu makiuga, “Aca rŭu nĭ irimŭ!” Akĭŭra ũrĭa ũngĭ, “Nĭtŭthiŭ.” Matanakinya kŭrĭa kwa irimŭ-rĭ, ũmwe agĭtigwo na thutha. ũrĭa ũngĭ agĭtonyania na irimŭ nyŭmba. Rŭu irimŭ nĭrĭheretie mahĭndĭ ma ciongo cia andŭ rĭgŭiikia rungu rwa ũrĭrĭ. Rŭu mŭirĭtu arŭthĭrĭria ũguo atŭngirwo nĭ kĭongo kĭa mŭndŭ. Agĭkinya na agĭkunya ũrĭa ũngĭ. Akĭmwĭra, “Githĭ ndikwĭrire rĭrĭ nĭ irimŭ?” Mŭirĭtu ũrĭa ndefĭkirie tondŭ wendo nĭumŭkĭirie wa irimŭ rĭrĭ tondŭ nĭ ithaka mŭno.

Mŭirĭtu ũcio ũngĭ akiuga, “Reke thĭi kahinda njŭke.” ũcio akĭŭra. Rŭu ũyŭ ũmwe makoma-rĭ, nĭonire kanua gaka. Akĭmenya aaai! O ũrĭa nĭrĭrwo rĭrĭ nĭ irimŭ. Akĭmwĭra rŭu nĭndĭrenda gŭthĭi kĭoro. Rĭkĭmwĭra gŭkŭ mŭndŭ atonya ndathiaga kĭoro. Mŭirĭtu akĭŭrĭa, “Ekaga atĭa tondŭ tŭtithiaga kĭoro nyŭmba?” Irimŭ rĭkĭgĭra mŭkwa rĭkĭmwĭra, “Rŭu no ngŭohereire haha (njohero) ngŭnyitie ũthĭi kĭoro ũcoko” Irimŭ rĭkĭgĭra mŭkwa rĭkĭmŭnyitia bĭŭŭndŭ

atang'ohora. Mũirĩtu nake kuma-rĩ, akĩũrio nĩ irimũ, “Nĩũkinyire harĩa ũgũthiaga?” Mũirĩtu akiuga, “Ĩhĩ ndĩgairie o hanini rĩu nginye.” Rĩu arenda akinye mũfĩ-inĩ ta ũrĩa.

Mũirĩtu agĩthĩ akĩoya mũkwa ũrĩa ohirwo nagu tondũ ũrĩa irimũ nĩrĩmũnyitirie nĩgetha ndakae kwohora. Mũirĩtu nake akĩohora haha. Rĩu arorio kana nĩakinyire no kuohora arohora. Irimũ rĩtikĩrĩ na ũmwe (mũthia) na ũrĩa ũngĩ mũirĩtu no kuohora arohora? Akĩoherera gĩthukĩnĩ, oherera-rĩ, mũirĩtu withĩre. Irimũ rĩgakĩmũragia, “Nĩũkinyire?” Mũirĩtu agikira, Rĩkĩmenya mũndũ ndarĩ haha. Rĩkiuma na mũkwa wakĩo rĩgĩkũnjaga-ĩ nĩgetha rĩmũgucie. Hi! Gĩgĩthĩ o gĩthukĩ-inĩ. gĩkiuga githĩ nĩ gũthĩ athiire. Gĩkĩoya kĩrũhiũ gĩetago kĩenji gĩaikagio handũ ũguo gĩkaheria handũ hanene.

Rĩurĩ, irimũ rĩgũka kaba! kaba! kaba! rĩteng'ere na kũrĩa mũirĩtu arorire. Mũirĩtu akĩona niekũnyitwo. Arĩ na mũrũ wa nyina na mũratawe akĩmenya andũ aya nĩo ngwĩta tondũ nĩ ngũnyitwo. Akĩmeta akiuga:

“Nĩnjĩrwo-~ Thũũgĩ, Waiya-~ na Njaranga na Mweri-~ nĩ mokage ũri mũcarĩ.”

Irimũ rĩgĩcokia, “*Ngũgĩtinia-~ ng'we ng'we,
Kĩnyondo kũ ng'we ng'we,
Gĩtinũkane-~ ng'wee!*”

Mũirĩtu akĩgua harĩa irimũ rĩrĩ. Akĩina rĩngĩ:

“Nĩnjĩrwo-~ Thũũgĩ, Waiya na Njaranga na Mweri-~ mokage ũrĩ mũcarĩ...”

(Thũũgĩ nĩ mũrũ wa nyina, nake Njaranga nĩ mũratawe). Efĩrwo andũ eerĩ nĩgetha mokage na mĩgwĩ (mũcarĩ).

Irimũ rĩgacokia, “*Ngũgĩtinia-~ ng'we ng'we,
Kĩnyondo kũ ng'we ng'we,
Gĩtinũkane-~ ng'wee!*”

Arĩa anake-rĩ nĩmaiguire kayũ, magĩkĩũrana rĩurĩ, rĩu nĩ irimũ na rĩu no nginya tũtũnge mũirĩtu ũyũ tondũ nĩekũrĩo. Rĩu ũrĩgwatia ati na mwaki. Agĩgũka akĩrehana, akĩrehana, akĩrehana o makĩnaga nao anake no gũka maroka na matimũ na mĩgwĩ yao magĩũka makĩũhitha. Mũirĩtu agĩũka akĩmahĩũka, rĩu ndacokire kũina rĩngĩ. Irimũnarĩo rĩgũka, rĩgũka, rĩgũka, rĩakinya o harĩa marĩ-rĩ, irimũ rĩgĩthecwo rĩgĩkua.

Rũgano rwathirĩra hau.

(2) IRIMŪ NA MŪCIAIRĪ

Tene nĩ kwarĩ andũ matũraga tũhiũ, matimũ na mbugi cia ng'ombe na mbũri. No ũngĩacũthĩrĩrie haria matũragĩra no ũrutire mbũri. Matiefĩkĩraga. Mũturi ndangĩendire gũcũthĩrĩrio nginya nĩ mwana wake kana mũtumia wake amenye nĩkĩ gĩaturagwo. Makanagio mũno nao matiaturangĩra hakuhĩ na andũ no harĩa harĩ andũ, kũmũcũthirĩria ũguo, no ũrutire mbũri.

Mwanake nĩhikanirie na nĩgũtura aturaga tũhiũ. Ahikania agĩtiga mũtumia wake agĩta nda akĩmwĩra rĩu-rĩ, nĩngũma gũkũ thiĩ ngaturĩre kũrĩa mũtitũ-inĩ na ngacoka ũkĩtheo mwana. Nake akĩmwĩra noguo. Mũtumia agĩtiguo nake mũthuri agĩthĩ gũtura tũhiũ.

Mũthuri athĩ gũtura-rĩ, nake gũkũ-rĩ, mũtumia wake-rĩ, irimũ rĩgĩũka rĩgĩkora akoragwo arĩ wiki. Irimũ nĩrĩo rĩacokire mũciĩ wa mũthuri ũyũ. Rĩgĩũka rĩgĩkara kũu nyũmba. Mũtumia ndarĩ na wa gũkaĩra na irimũ rĩtikũmũrĩa, no rĩetagirĩra mũtumia akaheo mwana. Aheo mwana nĩguo makamũrĩa na marimũ marĩa mangĩ.

Rĩu irimũ rĩgagĩthiaga gũcaria gĩa kũrĩa nginya mũtumia akĩtheo mwana. Aheo mwana irimũ nĩrĩakenire mũno. Rĩkĩra marimũ marĩa mangĩ, “Rĩu mũrehage o ngũ. Tuunage ngũ tũkĩgaga tondũ nĩaraheirwo mwana. No kũrĩa tũrĩmũhiũhagĩria nĩndĩmũheaga.” Mũtumia arũgĩrũo gacũrũ akanengerwo nĩ irimũ. Akerwo, “Wagaciairĩ ndũke mahiuhio! Warega nganyua.” Irimũ rĩkanyua. Okorwo nĩ irio rĩkauga, “Wagaciairĩ ndũke mahiuhio! Warega ngarĩa.” Rĩkarĩa

Mũtumia ũrĩa muciairĩ akĩhuuta akĩhũta nĩ gũtura eragwo warega ngarĩa warega nganyua. Mũthenya ũmwe kanyoni gagĩtũmwo nĩ Ngai. Kanyoni gakĩra mũndũ ũyũ ũgũtura afĩri:

Mũturi ugũtura-ii tura narua tura narua,

Mũkaguon~aciarire-i tura narua tura narua,

Ag~ciarithio n~irimũ-~ tura narua tura narua

Ai, agĩkĩrĩa kanyoni kĩndũ gakĩumbuka gakĩumba hangĩ. Gagĩũka gakĩmuhe uhoru. Gagĩũka gakĩmuumba kĩongo igũrũ gakĩina:

Tura narua tura narua

Wūinūke gwaku mūci~

Tura narua tura narua

Akīmenya hī, nderwo mūtumia nīaciarīre, agīciarithio nī irimū na ndure narua? Akīoha mūrigo yake akīoya njīra Kaba! Kaba! Kaba! Agīthī mūci. Akīhingūra nyūmba agīkora mūtumia wake. Mūtumia wake akīmwīra “Nī nīndaheirwo mwana na rīu irimū nīrīo tūtūraga narīo rījīraga wagaciarī ndūke mahiūhio, warega ngarīa, warega ngayua.”

Mūthuri akīmwīra aheo ūhoru nī kanyonī. Nake mūtumia akīmūira ena kiumia kuma aheo mwana na eragwo warega ngarīa ona itaregete. Mūthuri akīūrīa mūtumia kana nīrīgūka nake mūtumia akiuga, “rīu harīa marī maunīte ngūū ici ūrona gūkū me hamwe na macio mangī. Mūthuri akīmwīra, “Rīu reke ngūrūgīre irīo wambe ūrīe. Wahūna-rī njoke ndīthithe thī itara, nawe wehere ūthī onakūu thīnī mūno rītīgagūkore nja.” Mūtumia akīūrīo kana nīaumaga nja nake akiuga atī nīakanirīo kuuma nja guota rīūa. Mūthuri agīthī o itara.

Irimū rīarekagia ngūū rīkauga, “Hu! Wagaciarī ūrīo nyūmba īno? Ūrogwa na mūrurumo ūcio! Mūtumia nīerītwo nī mūthuriwe irimū rīamuīra ūguo acokie, “O nawe ūrogwa na mūrurumo ūcio!” nake Wagaciarī akīmwīra, “O nawe ūrogūa nagūo!” Irimū rīkīmūrīa, “Īwagaciarī kaī wekinyīra atīa ta marī ūturi-nī mokite?”

Irimū rīkīrigwo ūrīa Wagaciarī ekinyīre ena ūrume ta marīūturi-nī mokīte tondū ndarī amūcokerīa ūguo. Irimū rīkīgīrīra ngūū rīgītemania rīngī rīkiuga, “Wagaciarīūrogwa na mūrurumo ūcio.” Mūtumia agīcokia, “Onawe ūrogwa nago” Irimū rīkīmenya gūkū angīkorwo biū biū marīūturinī matiūkīte ūmūthī ndangīrara nītūkūmūrīa. Rīgītonya nyūmba rīkīmūrīa, “Wagaciarī ūmūthī wekinyīra ūguo nīkī?” Rīkīmūrīka kūu ūguo rīkīona gūtīrīmūdū. Rīīarīrīkanire kūmūrīka itara kūrīa marī ūturinī maarī.

Rīgīkara thī rīkīruga ūcūrū, mūthuri akīreka rīruge ūcūrū. Rīkiuga, Wagaciarī ndugīre mahiūhio! Warega nganyua.” O rīrī rīranywa-rī rīkīrwo ūta ka! Rīkiuga to njugire, to njugire, to njugire marīūturi-rī nī mokīte!

Rūgano rwathīrīra hau.

(3) ANAKE ATATŪ NA IRIMŪ

Tene anake atatū nīmeranire magacarie airītu athaka matarī wathe. Makīrana mekuire rīgu nīguo matikahūrte njīra-inī. Makīrīkanīra o mūdū arute ndegwa īmwe īmwe na makīruta ikīhinga ndegwa ithatū. Makiuga magaathīnjīra kūdū gūtārīngī nīguo itigathahie maīrūdū mao. Mwanake ūmwe agītaha ngi, agīcīkīra thiaka-inī agīcikua arīa angī matekūmenya. Makīambīrīria rūgendo magīthī, magīthī makīguā nī mahūta makiuga maikare thī mathīnje tondū ona gūtīarī ngi kūrīa marī.

Mwanake ūmwe wetagwo Thome nīwe wakuīte ngi agīkunka thiaka ngi imwe ikiuma. Aanake acio angī makiuga, “Tūtīkūrīa nyama ici tondū cigūtambwo ni ngi.” Makīrana mathī na mbere na rūgendo. Magīthī, mathī-rī, Thome akīmeera atīrī, “Nindariganūrwo nī mīgūi īmwe yakwa.” Anake acio angī makīmwīra, “Nītūrthī, tīga gūcooka.” Thome akīrega akiuga, “Īhī, nīngūcookera ndīngīmītīga nī kumagīra ūndū.”

Agīcooka akīrīa nyama, akīrīa, akīrīa, akīmīnīna. Agīcooka akīoya maguru o kuku, kuku, agīkīnyīra arīa angī. Magīthī na mbere na rūgendo, magīthī, magīthī, makiuga mathīnje iyo īngī. Magīthīnja iyo īngī. Nīngī Thome agīkunūra atekuonwo ngi īngī ikiuma ikīnyītīrīra nyama. Anake makīrega kurīa nyama icio makīanjīa guthī. Thome akīgwatīa niatīga thīarī yake agīcooka ona thuutha akīrīa nyama irīa na akīnyua thakame na agīcooka agītēng’era agīkīnyīra acio angī.

